

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MAGHARINI
CONSTITUENCY, HELD AT MAPIMO PRIMARY SCHOOL**

ON

MAY, 2ND 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MAGHARINI CONSTITUENCY, MAPIMO PRIMARY SCHOOL
ON 2ND APRIL 2002

Present:

Com. Riunga Raiji
Com. Abdirizak A. Nunow
Com. Abida Ali Aaroni

Secretariat Staff in Attendance:

John Watibi - Programme Officer
Hilda Miranga - Asst. Programme Officer
Gladys Osimbo - Verbatim Recorder
Rose Samba - Sign Lang. Interpreter

The meeting started at

Com. Riunga: Ninafikiri kabla hatujaanza, na nikawaida yetu kuanza na maombi. Tafadhali tutauliza mtu mmoja ajitolee na atuongoze kwa maombi. Kama kuna Kasisi ama Imam anayeweza kutuongoza, tafadhali mwakaribishwa. Akuje hapa atuongoze ili tuanze shughuli yetu kirasmi.

Speaker: Tufunge macho. Baba katika jina la Yesu tunakushukuru asubuhi ya leo kwa maana Mungu umetenda ajabu

kutuamsha tukiwa wazima. Asante kwa kikao hiki, asante hata kwa yale Bwana tunayoendea. Ninakuomba utusaidie, utuongoze na ukuwe mwenyeketi katika mkutano huu. Kwa jina la Yesu tunakuomba, Amen.

Com. Riunga: Asante sana. Inaonekana upepo ni mkali kidogo lakini utapoa baadaye. Sasa wanainchi tungetaka kuanza. Kwanza kabisa kwa niaba ya Tme ya Kurekebisha Katiba tunataka kuwakaribisha katika kikao hiki rasmi cha kutoa maoni katika Constituency hii. Pamoja nami tuko na Com. Dr. Alale Nunow, jina langu ni Riunga Raiji, hata mimi ni Commissioner. Tuko naye Programme Officer John Watibini, tuko na wasaidizi ambao wanaandika hii ripoti na kurekodi maoni ambayo tutatoa leo hii – tuko na Hilda, Rose na Gladys. Na pamoja na sisi tuko na wenzenu, District Coordinator, Bw. Jefwa Kingi. Ninafikiri nitauliza Bwana Jefwa atujulisha kwa wanachama wa Constitution Committee ya hapa.

Bw. Jefwa: Hamjambo. Katika kila sehemu ya uwaakilishi bungeni tuna kamati ya kikatiba. Hiyo kamati ina watu kumi. Hapa upande wa taarafa ya Magharini, tuna Councillor Hatafu ambaye amesima pale, huyu ni mwana kamati. Tuna nafasi ya Heme, huyu ni mwana kamati anaye tuwakilisha upande wa Mwamburui na tuna Mary Menza, anaye tuwakilisha upande wa kufundisha. Hapa Mapimo tunawakilishwa na Bw. Jilo Loto ambaye atakuja karibuni, wale wengine wako sehemu ya Marafa kwa maana kesho itakuwa Marafa. Kwa hivyo tungetaka kuwa karibisha nyote.

Com. Riunga: Tunataka kumkaribisha D.O. Bw. Ali. Kwa sababu sasa hapa ni kwa Commission, hapa tunakaa karibu na Bw. D.O na tungetaka kumuambia asante kwa kuwa na sisi hata yeye ni mwanainchi isipokuwa sasa kazi yake ni kusiskiza kama sisi tunasikizwa. Kabla hatujaanza, ningetaka kumwambia ule utaratibu tutakaofuata. Kama kawaida yetu, wale wangetaka kutoa maoni, wanaombwa wajiandikishe katika kile kiti, na tutafuata wale wa kwanza ndio watazungumza kwanza (first come, first served). Tutawapatia kila mtu aliye na maandishi yaani memorandum, dakika tano, atuambie kwa ufupi tu yale yako katika memorandum. Lakini kwa sababu watu wanaendelea kuwa wengi, hatutapatia watu nafasi ya kusoma kile chote kimeandikwa kwa sababu memorandum zingine ni ndefu. Kwa hivyo, kama unayo memorandum tutakupatia dakika tano halafu utatupatia hiyo memorandum ili tuweze kuitumia wakati tunaandika Katiba. Kama ni maoni tutakupatia dakika saba hivi, ili utueleze maoni yako na tutaendelea namna hiyo.

Na tunaomba kama kawaida ya sisi, watu wa kutoka Commission, hatupendelei upande wowote, (we are non-partisan), kwa hivyo kazi yetu na hata nyinyi wanainchi ambao mumejitokeza hapa ni kusikiza kila maoni. Mtu atoe maoni yake, akuwe huru, tutaandika kila kitu, tuna tape recorder, tuna rekodi kila kitu kwa sababu yale maoni mutakayetoa ni muhimu sana ndio yametufanya sisi tuje hapa. Kwa hivyo tungetaka kuwaambia muwe huru kabisa kutoa maoni yenu, kutoka ndani ya roho zenyu na tutayaandika na kuyatumia katika kazi yetu ya kuandika Katiba. Na bila ya kupoteza wakati, ningetaka kumuita sasa mtu wa kwanza, David Nduria Ngolo. Bw. Ngolo karibu, utakuja hapa katika hiki chombo kwa sababu tuna record na utanza na jina lako ili liingie kwa machine yetu. Tukimaliza na Bw. Ngolo tutamuita Bw. Ali Kombe, atakuwa wapili, kwa hivyo awe akijitayarisha. Karibu Bwana.

Bw. David Nduria Ngolo: Nikiwa mbele yenu, naitwa David Nduria Ngolo, ninatoa maoni ya kikundi au maoni ya sub-location ya Ngomeni. Tumezungumzia habari ya mashamba.

Mashamba yamekuwa na matatizo kwa muda mrefu sana na tumelalamika na hatujapata mwangaza wowote. Ndivyo wanainchi wakazungumza ya kwamba ingelikuwa vizuri serikali, ichukuwe jukumu la kuwapatia zao wakaazi wa sehemu hiyo yote au wakaazi wanaohusika katika ardhi kwa sababu wengi wao huwa wanakuja kufukuzwa mashambani mwao kwa sababu ya hati ambazo zinatolewa huko Nairobi. Akiwa masikini hawezi kuchukua hatua yoyote ambayo anaweza kupata haki yake. Na hati zote zinachukuliwa na wale ambao wana uwezo.

Pili, tukazungumzia habari ya elimu. Elimu imekuwa hali ya juu, pesa zimekuwa nyingi sana hata wale ambao hawajiwezi watoto wao hawawezi kujiendeleza, kwa sababu pesa zimekuwa nyingi. Nategemewa kutoka sehemu za nursery tunalipa karo kidogo, lakini hata hivyo wengi wao wanakaa majumbani kwa sababu ya ukame wa pesa au kazi. Hivyo tukazungumzia kwamba kama ingewezekana serikali ingechukua jukumu kutoka nursery mpaka secondary school, at least, kama ni secondary zipunguzwe lakini kuanzia primary ziwe za bure, wasomeshwe kama zamani walivyokuwa wakisomeshwa na serikali ikiwa inachukuwa jukumu la majenzi na kila aina ya vifaa vilivyokuwa vinahitajika.

Tukazungumzia habari ya haki za watoto. Kuna wamama wengi wanaosumbuka kwa sababu ya kuwachwa na mabwana zao. Wanaona kama wanathulumiwa, kuwachiwa familia akiwa yeye hajiwezi na baba anaoa mwengine ama anakimbia na kwenda sehemu za mbali akiwa anaachiwa mzigo wa malezi. Hivyo akina mama wakasema kuwa kama ingewezekana haki za wamama pamoja na watoto serikali ifikirie.

Pia vile vile kwa sababu ni kikundi na mimi ni kiwa kama Asst. Chief, maneno haya yamezungumziwa na wanainchi wenyewe. Pia vile vile wakagusia sehemu ya kwamba kama ingewezekana serikali ikawa ya majimbo – hayo ni maoni ya wanainchi. Pia vile vile ya mwisho ni kwamba wamezungumzia hali ya usalama wakiwa sehemu za mwituni. Watu wanasumbuliwa na wale majangili, wanauliza serikali kama ingewezakana kungewekwa vituo vya usalama ili wanainchi wakapata uhuru wa kuishi mahali kule kwa sababu wanaishi katika matown wanapofukuzwa na kule hakuna mashamba ya kulima. Hivyo maoni ya wanainchi wa sehemu ya Ngomeni sub-location, yakawa ni hayo kama sita na iwapo kuna wengine wamekuja kuchangia kwa upande wa Ngomeni na anamaoni yake ya kibinafsi, basi anaweza kuja na kuandikwa ili apate kuzungumza yale yote ambayo pengine yalibaki. Kwa hivyo asanteni, maoni ya wanainchi ambao walikuwa huko ni hayo na Mungu awabariki.

Com. Riunga: Asante sana ukimaliza kutoa maoni, tungetaka ujiandikishe kwa record zetu. Kwa hivyo asante sana Bw. Ngolo, wa pili atakuwa Bw. Ali Kombe. Atakuja baadaye. Bwana Karisa Mangi, karibu. Kama ungetaka kuzungumza kwa lugha ya mama tunawatu wa kutafsiri, karibu mzee.

Bw. Karisa: Hamjambo. Kwa jina ninaitwa Karisa. (Talked in vernacular) lakini kuanzia mwaka wa 1999 nikaja nikanyang’

anywa. Sasa lile shamba lina limwa na watu wengine hata hivi ni mwaka wa tatu.

Translator: Nina shamba langu ambalo nililipata mwaka wa 1960. Ilipofika mwaka wa 1999 nikapokonywa lile shamba mpaka sasa linawatu wengine tofauti. Kwa hivyo ninataka shamba niregeshewe mwenyewe. Hayo ndio maoni yangu.

(Inaudible)

Tunataka serikali ya majimbo watu wa magharini, pwani nzima na Kenya nzima. Utawala ulioko sasa hautusaidii hata kidogo kuanzia mwaka wa 1963 mpaka sasa tunaishi kwa umasikini miaka thelathini na tisa. Kwanza kila jimbo iwe na governor wake. Governor awe na uwezo wa kuajiri wafanyi kazi wote na awe na uwezo wa kukopa mikopo kutoka nje kusaidia wanaichi wa jimbo lake. Tatu, Rais achaguliwe kutoka kwa ma-governor hao wanane watakaenda kupigania urais. Na katika magovernor hao wa uchaguzi, hamsini kwa mia governor atakayepata awe rais na rais asiwe na mamlaka ya jimbo lolote lile kutoka kwa governor. Lingine ni ya kwamba kuwe na watu watacao ajiriwa katika kila jimbo kuangalia mishahara ya wafanyi kazi, kutoka mahotelini, wabunge, ma-governor na kila mfanyi kazi anakatwa pesa nusu (50%) kutoka kwa mshahara wake kuingia katika hazina ya maendeleo ya jimbo ndio njia moja ya kuondosha umasikini. Si mbunge au mtu anafanya kazi anarundikwa pesa na wengine wanaishi nyumba za mchanga, wanaishi kuuza makaa na maisha ya taabu, wao wanalala nyumba za maghorofa na kutembea na magari ya fahari. Hiyo hatutaki, serikali iwe namna hiyo. Sasa watu kama wale wanaajiriwa, zinakatwa pesa kila mfanyi kazi wa jimbo, anayefanya kwa kampuni, kwa hoteli, hata akiwa ni governor hata wale ambao watakuwa wameajiriwa, wanakatwa hamsini kwa mia zinaingia katika mfuko wa maendeleo ya jimbo zipate kutengeza barabara, shule, ma-hospitali na hata elimu.

Tatu, elimu kuanzia nursery mpaka university, iwe ni bure. Zile pesa ambazo zinakatwa zinagharimia kila gharama ya watoto wa shule na kila mtoto kuanzia darasa la kwanza hadi la nane watakuwa wanasoma wakirudi nyumbani. Lakini kuanzia form one mpaka form four, wanakuwa bwenini na mabweni ya wasichana mbali na wavulana mbali. Na kila mtoto ana pocket money anapewa kila mwezi kwa ajili ya mahitaji ya dharura. Tatu, wanaosoma chuo kikuu itakuwa ni mchanganyiko kati ya wavulana na wasichana na wawe na pesa za mfuko za kugharamia mahitaji yao.

Lingine ni juu ya ukulima. Kila mkulima alazimishwe kulima angalau acre mbili kwa kilimo cha kisasa. Governor ana uwezo wa kukopa hata matrakta nje, na wakulima wakiwa wanalima kila baada ya kulima, mavuno yale wanalipa pesa katika ile gharama na mkulima hapo ndio njia ingine ya kuondoa umasikini. Kila mkulima aruhusiwe kufuga ngo'mbe za grade, kila mwanamkulima aruhusiwe afuge kuku wa grade. Vitu kama zile zitapelekwa kwa ma-hoteli.

Kumiliki mashamba, mwananchi unauwezo wa kumili shamba pwani yote katika jimbo lake, kusiwe na pingamizi lolote. Mgeni haruhusiwi kumiliki shamba katika jimbo lingine. Nne, mgeni haruhusiwi kumiliki mashamba ya beach au mgeni haruhusiwi kufanya biashara bila kushirikiana na mwenyeji wa jimbo hilo. Sita, ni kwamba n'gombe wa kienyeji wanatakikana wapelekwe

ranch, wafugwe kule. Zinapouzwa maziwa na nyama, watatoa statement zao kila mwaka na faida yao maanake hao wanaanza kusumbua kula mashamba ya watu, mimea yao na kusiwe na matatizo yoyote.

Saba ni kwamba, hali ya uhalifu. Wale wanaopatikana wakilima bangi, miraa, wanaouza marijuana, heroine, brown sugar, hukumu yao ni kupigwa risasi hadharani. (*applause*)

Hakuna njia ingine ya kubembeleza, tunataka serikali ya namna hiyo, wanawekwa juu ya mti wanapigwa risasi kumi, akipona anaambiwa nenda zako. Lngine ni kwamba uhalifu, wanao najisi wanawake na watoto adhabu yao wanafungwa kifungo cha maisha. Wachawi wakishikwa wanafungwa kifungo cha maisha, hana muradi wa kukaa na raia, anatengwa akafanye kazi kule. Ndipo tunataka serikali ya majimbo. Maoni yangu ni hayo na mengine yatakuja baadaye.

Com. Riunga: Asante sana. Huyu ni Samuel Chengo Baya, karibu.

Bw. Samuel Chengo Baya: Kwa jina naitwa Samuel Chengo Baya, chama ni Shirikisho majimbo, youth leader wa Gongoni Location. Yule aliyotoka hapa saa hii ni mwanakishini wangu. Tuna memorandum tuliyoandika mimi na yeye ambayo itaenda kusomwa huko, ijulikane vizuri yale maoni yetu kuhusu vile tunavyotaka wanapwani wote. Mimi sitazungumza sana lakini nasikia uchungu kiasi ambacho siwezi kuzungumza yale ambayo yanafanyika hapa pwani. Kama juzi hapa Tana River vile ilivyofanyika, ile yote imefanywa na serikali ya umoja, kama ni serikali ya majimbo ni jimbo lake peke yake haingefanyika vile, watu hawangepotea namna ile kwa sababu ni ya umoja wa kushirikiana na watu wengine ambao wana unyama. Kwa hivyo tunataka serikali ya majimbo, kila jimbo lijitawale lenyewe, vile linavyoona ni sawa. Na hiyo ndiyo ambayo inafanya hata nyinyi leo mumekuja hapa kutaka maoni ya wanainchi. Tunataka serikali ya majimbo, kila jimbo lijitengemee lenyewe. Mengi mutakwenda kuyaona katika memorandum yangu. Mimi ni hayo tu. Asante.

Com. Riunga: Asante sana. Mwengine ni Karisa Ngala. Karibu mzee.

Bw. Karisa Ngala: Asante sana bwana mwenyekiti. Mimi ninaitwa Karisa Ngala Kazeha. Nikiwa hapa nilipo ni mzee wa miaka sitini na saba na ninataka kutoa maoni yangu wakati huu ambao tunatembelewa na hii Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya. Bwana mwenyekiti, ningetaka sana kuanza kwamba mchukuwe maoni kama tunavyotoa sisi. Mimi kama mzee ambao uhuru ukiingia hapa, mimi ninaweza kukuambia juu ya uchaguzi tuliofanya hapa Kenya. Ni juu yenu sasa kuiweka Kenya sawa sawa wakati huu ambao sisi tuko hai watoto wetu na wajukuu wetu. Tuchukue maoni ya sawa sawa hata kama mtu moja anasema maoni lakini yafuatwe, sio kufuata mambo ya watu wengi ambao watasema urongo. Kama maoni ya watu elfu moja ni ya ukweli, yafatwe, tunataka amani Kenya. Bwana Ngala alivunja KADU kwa sababu ya kutaka amani Kenya. Hatutaki umwagikaji wa damu Kenya na kuepukana na umwagaji wa damu, hii katiba ya majimbo iwekwe sawa sawa kabisa. Kwamba tuwe na amani, wazee kwa watoto, tuweke msingi wa wajukuu wetu wanaokuja wakati ujao. Sio kuweka Katiba ya kiholela holela kama vile ilivyofanywa na Kenyatta. Kenya hii ulipofanya mazungumzo huko Lancaster mwaka wa 1962, wakaleta katiba nzuri kabisa, masikini anaye umasikini wake, tajiri anaye utajiri wake, lakini kwa uadui na tamaa ya Kenyatta na watu

wake akatayarisha Katiba yake iliyo sasa ambao hasa watu wa pwani ni kama watumwa, watumwa. Lakini ninashukuru mzee Moi na wenzake ambao wamekaa chini wakafikiria ya kwamba tunaenda wapi sisi wa Kenya?

Mzee wetu Moi tunamshukuru sana kwa maoni hayo ambayo mpaka sasa tuko hapa tunazungumzia maoni yetu sasa. Kenya ni nchi ya amani, lakini hakuna wakati tutaendelea ukiwa nimelala njaa hatuwezi tukaendelea kabisa. Amani inakuja kwa sababu wewe unashiba na mimi ninashiba. Amani inakuja kwa sababu wewe unashiba na mimi ninashiba, unakula haki yako lakini wewe ukila haki yako na yangu unakula hakuna amani hapo. Kwa hivyo, natumaini sasa Mungu huu nchi yetu anaipenda kabisa, kwa kutoa maoni haya ya leo, ninashukuru sana. Majimbo ndio msingi wa ulimwengu mzima, wacha wale hawataki wanaosema ni serikali moja, anataka kushiba yeye peke yake, haki yake achukue yeye na haki yangu pia achukue yeye, hiyo haiwezekani kabisa. Vita vinaendelea ulimwengu mzima kwa sababu ya haki yako unakula na haki yangu unakula, haiwezekani kabisa. Mimi hivi unavyoniona nimekaa Mombasa miaka sitini na saba na nimesoma mambo mengi ya ulimwengu vile ya inavyofanyika, Katiba ya majimbo ndio msingi wa mwanadamu wa sasa. Bila Katiba ya majimbo, urongo.

Com. Riunga: Kama huna maoni ukae.

Bw. Karisa: Sasa maoni yangu ninataka majimbo. Na mimi ninasema ya kwamba ni juu yako uchukue maoni haya – Kenya ni nchi majimbo, hakuna katiba ingine. Asante.

Com. Riunga: Asante mzee, lakini ningetaka kuwajulisha ya kwamba shughuli ya leo ni maoni kwa sababu tunaandika na mapendekezo yenu vile mngetaka tufanye katika Katiba ili tutatue shida zile munazo. Hii ina tofauti kidogo na hii ingine tunayofanya ya siasa, hii ni ya maoni na mapendekezo ile ambao munataka tuandike ili tutatue shida ambazo tukonazo.

Com. Riunga: Sasa tuko na Harrison Ngala.

Bw. Harrison Ngala: Asante sana Commissioners wa Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya na vile vile asante Bw. D.O, wanachama wote na wananchi, hamjambo? Mimi ninaitwa Harrison Chome Ngala. Ninazungumza kama mwenyeji wa eneo hili la Magharini na vile kama kiongozi ama mtu mzima ambaye anajua uzuri na ubaya. Kulingana na yale yalizungumziwa, mimi kwanza katika hali ya kutaka kutoa maoni kidogo ningeonelea kwamba ma-Commissioners wetu ambao wamekuja Gongoni kwa sababu ya kuchukua maoni ya watu na kutoa dakika saba, hiyo nikutuchezea. Kwa sababu kwa dakika saba mtu atajitambulisha na amefikia pahali pakusemea la muhimu, muda wake umeisha, hivyo amekuja hakusema kitu. Nasi kuiokoa Kenya ni kufanya yale ambayo yataifanya Kenya iokoke na ikiwa tunataka kuiokoa na tuifanye yale ambayo yatazidi kuiangamiza, basi huwa tumepoteza wakati, asante. Kwa upande wangu kimaoni nimechunguza tangu uhuru kupatikana, umi wangu wakati huo nilikuwa nishakuwa mpigaji kura na kura hiyo yakupokea uhuru ndio ya kwanza mimi kupiga.

Tumeona yale yaliondelea. Kenya ikipata uhuru ilikuwa na Katiba ya majimbo. Ilitumika kwa miezi kumi halafu baadaye

ikawekwa kando na kiongozi mwanzilishi kwa faida yake yeye mwenyewe na watu wake na imetuletea maafa ya kutosha ndiposa leo tuna marekebisho. Binafsi ninasema iregeshwe moja kwa moja na Katiba hiyo ni ile ya Lancaster House, 1960 kule uingereza ambayo imebeba furushi la majimbo lenye haki za kila mtu bila kubagua dini, kabila, uwezo wa kielimu, kimapato ama nguvu hata za kumenyana. Katika hali kama hiyo kutaka kuregesha mambo kama hayo. Wakati huu vita hivyo tunavyojua sote vilipambanwa sisi sote tukiwakilishwa na Kanu iliyotawala na Kadu. Katika huu mfumo wa vyama vingi, ninayo mapendekezo na maoni yanayoweza kukubaliwa na wengi, lakini ninayachukua kuwa ya kibinafsi kwa sasa. Kadu pia ipewe nafasi ya mfumo wa vyama vingi kwa sababu ulifanya kazi nzuri pamoja na Kanu na tukapata uhuru ambao ndio tumeuchezea sisi wenyewe na kutupa janga la kurekebisha. Hata nikitaka kusema zaidi nashangaa ni kwa nini serikali imeamua kuweka Tume ya Kurebisha Katiba na Katiba nzima iko pale pale. Watu hawa wanalipwa pesa nyingi ambazo serikali mambo mengi imeshindwa kufanya ikisema haina pesa na kile chakutumika kiko pale kinaachwa huku watu wanakula pesa. Pesa hizo zingetumika kwingine – kwa madawa hospitalini, hata vyakula kwa zile sehemu ambazo watu hawana chakula wanakufa njaa.

Lakini kwa sababu serikali imetupatia nafasi tusipoteze wakati. Mtu unapoulizwa maoni, mimi ninaonelea ya kwamba Katiba ya majimbo ikirudi, suluhisho la mambo yote limepatikana. Na kama sio, basi labda kuna nia mbaya katika kurekebisha kwamba wale waliumiza wengine, wanyonge bado wanatafuta vipengele katika marekebisho, waendelea kutuumiza ndiposa tunaita Katiba ya majimbo ile ya Lancaster House ya 1962 moja kwa moja, ambayo itatoa haki kwa wote kuhusu ardhi. Hiyo Katiba imezungumza kila kitu na kimewekwa mikononi mwa wananchi. Leo hii, Commissioner yuko Nairobi, hajui Gongoni iko vipi anapeana ardhi akisema hakuna watu huko. Mamlaka hiyo ikiwa kwa majimbo inabaki kwa jimbo na huwa inasimamiwa vizuri na raslimali hiyo inagawiwa kulingana na wenyeji. Pili, serikali haistahili kuuza ardhi ya Kenya. Wageni wanaokuja kutafuta ardhi wakodishiwe kwa muda ule wanaotaka, ukiisha wenyeji wachukue na ikifika wakati wa kuhitaji waiharamishe. Huwezi uza kitu kile unahitaji halafu mwenyewe udanganye kosa la kufanya. Na hii haingefanyika kama Katiba ya majimbo ingekuwako kwa sababu kila mtu angekuwa anauza chake, lakini kwa sababu hao wengine wamepata nafasi ya kuuza vya watu wale ndiposa imekuwa ni biashara na watu wanabaki bila makao.

Kuhusu elimu, imezungumziwa kwa muda mrefu, watu wengine wana maoni kwamba mtu kuwa kiongozi ama kuwa mbunge awe na degree ama awe na kiwango fulani wa elimu ni sawa, lakini kiongozi achaguliwe kulingana na maadili yake ama ubora wake, msingi wa elimu ifuate baadaye. Na ile inaendelea sasa, kufanya mtihani ili mtu aonekane anaweza kuongea kule kingereza na kukifahamu kinacho zungumzwa na wenzao, yatosha. Tukimpata mwenye vipaji vizuri na elimu nzuri lakini sio kikwazo kwa mtu anayefaa akosekane halafu tuweke watu elimu kubwa na ni elimu peke yake, hakuna kitu kingine katika uongozi. Huwa tunapoteza wakati na kuwafanya wananchi wajute baadaye kwa sababu kama mumelazimishwa mtu awe na kiwango fulani watafuata kile kiwango fulani cha elimu peke yake, lakini maongozi Mungu hakumpatia. Ninafikiria mimi kwa upande mwingine, haki ya uraia iwe ya wakenya wenyewe asili, hasa ya waafrika na kama wako makabila mengine ya asili hapo, wale wengine wawe ni raia wa kujiandikisha, na wapigwe darubini kabla hawajakubaliwa na wakishakubaliwa pia isiwe dhamana, wafuate kanuni za nchi. Kama sio hivyo, kuharamishwa ni sawa. Hivi sasa nchi yetu kulingana na usimamizi wa haki ya kumpatia mtu uraia, kuachwa mikononi mwa watu wachache imekuwa ni biashara. Mgeni akiingia leo kutoka asubuhi

kufikia jioni ameshakuwa raia, ameshapata ardhi ya Kenya na ana kila kitu mwenyeji bado hajapata hata nusu-nchi wala haki zile mgeni amepata. Hatubagui, lakini kama ni mgeni aingie ale, halafu mukufe njaa kuna hekima gani hapo? Ikiwa ni ashibe, tushibe sote, yeye akifurahia kwamba amekaribishwa vizuri na mwenye kumkaribisha amekula. Lakini imekuwa sasa wenye kubeba mamlaka hayo ni wachache walioachiwa, ni biashara, ndiposa mkazo unaingia.

Katiba ya majimbo ya 1962 iregeshwe nzima bila ya marekebisho, kwani hayo marekebisho tulionayo ni kutokana na yale mageuzi yalioingizwa na wale waliokuwa na tamaa zao na kwa sababu hiyo ndio imetenda dhambi, itupwe moja kwa moja, ile safi iletwe. Ninafikiri kwa vile mumefika hapa kukusanya maoni ya wengi, mtapata mengi kutoka kwa wenzangu, lakini mimi ninahimiza mambo mawili tu au matatu. Kuregeshwa kwa katiba ya majimbo ile ilileta uhuru moja kwa moja bila kukwaruzwa popote ili ikifika wakati wa kuirekebisha endapo itatokea tufanye hivyo, tusipoteze wakati kuwa na marekebisho huku na huko kuwatafutia maadui nafasi ya kuumiza wengine. Heshima ya vyama vingi iliyopatiwa Kenya, Kanu ikiwa ndiyo inayoongoza, Kadu nayo ifuate, isiwekewe vikwazo vyovyote kufufuliwa kwa sababu haikutenda dhambi yoyote kwa Kenya wala watu binafsi.

Tatu, haki ya uraia iwe kwa wakenya wenyewe na wale wengine watimize masharti ya kisawasawa ndipo waruhusiwe, sio kuwapatia watu kibiashara kiholela, wenyeji wanaachwa taabani, wageni wanafurahia wanaachwa kwenye raha. Hii katiba iliyoko itupeni kabisa sio kuibembeleza, imetenda maovu, hasa kwa makabila madogo na pwani zaidi. Asante sana kwa Commissioners na wananchi wenzangu kwa kunisikiza, mungu endapo ataongoza Commissioners wetu vyema watachukua maoni yaliyobora sio yale yamesemwa na wengi ili kwamba Kenya iokolewe kwa janga la vita, misukosuko na wengine kuomboleza haki zao zikichezewa na wengine. Asante.

Com. Riunga: Asante sana mzee. Mwingine atakuwa ni Bw. Tenga Chalo. Na ningewaomba kwa heshima kwa sababu kuna watu wengi wangetaka kuzungumza tusiwe tukirudia zile point ukilenga point ile unataka ili wengine wapate nafasi. Sisi Commissioners tuko hapa siku yote, lakini tungetaka kama ingewezekana tupatie watu wengi nafasi. Asanteni. Tenga Chalo hayuko? Bwana Mohamed Sefu.

Bwana Mohamed Sefu: Commissioners ndio wageni na wenyeji. Jina langu ni Mohamed Heri Sefu kutoka kijiji cha Ngomeni. Maoni yangu ama mapendekezo ningependa yafanyiwe katika Katiba ni kuwekwa kifungu fulani ambavyo vitarahisisha na kurekebisha mambo fulani ambayo sisi wenyeji wananchi wa Kenya tumenyanyaswa, tumedhalilishwa na pia tumeseketwa. Jambo la kwanza ningependa katika Katiba kiwe na kifungu ambacho kitarahisisha bila ubaguzi wa dini wala ukabila wala ubaguzi wa akili, rangi wala hisia irahisishwe kwa wananchi ambao ni wenyeji, wapewe cheti cha kuzaliwa, kitambulisho na passport na hati ya kumiliki ardhi. Hii ikarahisishwa itasaidia kuondosha thuluma, rushwa, hongo, ufisadi na pia kupunguza umasikini. Kifungu kingine cha pili ambacho ningependa kiongezwe ni juu ya nafasi za kwanza kwa mfano kwa upande wa kazi, wawe ni wale wenyeji wa mji ama wenye kijiji ndio wanapewa hiyo nafasi, nafasi zikiwa bado ziko nyingi. Nafasi ya pili wapewe wenyeji wa taarafa ambao ni wa constituency, nafasi ya tatu ipewe wenyeji wa mkoa huu ambao

unahusika ambao ni district. Nafasi ya nne ipewe watu ambao ni wenyeji wa wilaya hiyo inayohusika. Na nafasi ya tano kama bado imebakia, wapewe wageni ambao pia ni wakutoka sehemu zingine za nchi ama hata nikutoka nje, kulingana na mahitaji zitakayotakikana. Sio kusema kuwa hatutaki wageni, lakini kama vile wale wenzangu wanavyokuja kusema ni kuwa wazee wamesema, mgeni aje na mwenyeji apone. Hawakusema kuwa mwenyeji aumie ama afe wakati mgeni anapokuja.

Tatu, kifungu ambacho ningependa kiwekwe katika Katiba ni tukuwe na serikali ya majimbo kwa mfano Nigeria, Germany, USA, hizo ni federal governments ambazo zimefaulu. Na vile tunavyoendelea sisi tunazidi sana kuiga mambo ya kigeni. Sisi mambo ya majimbo si mageni, tulipewa wakati wa kwanza lakini sisi wenyewe hatukuweza kutumia vizuri, kwa hivyo hii ikatutoka mikononi. Tukiweza kuwa na serikali ya majimbo itatuwezesha kuendelea maendeleo yetu, elimu na kazi bega kwa bega na sehemu zingine bila kubakia nyuma. Kwa hivyo sasa kwa vile hatuna serikali ya majimbo, utapata majimbo mengine yako nyuma kimaendeleo, kielimu, kikazi, kiumasikini na shida ziko nyingi sana. Kwa hivyo serikali ya majimbo ndio suluhisho kwa watu wengi sisi wapwani.

Sehemu ya nne ambayo nigepeleka kuingilia ni katika mambo ya ardhi. Ningependa katika Katiba, serikali yetu iheshimu mikataba yote ile ilikuwako kabla ya uhuru, ili tusikuwe na matatizo kama vile ilivyo sasa upande wa Zimbabwe, tungependa tuwe na suluhisho kama vile mzee Kenyatta alivyofanya walipotaka kuchukua mashamba ya wakoloni ama the 'highlands' katika central Rift Valley na upande wa Nakuru. Hakufukuza watu wala hakunyan'ganya watu, alitafuta suluhisho akapata msaada kutoka nje, halafu zile pesa zilipopatikana wale ambao walikuwa na hayo mashamba waliridhika kwa kusikizana na wapakewa chao na kisha ardhi ikapewa wale ambao walikuwa watakiwa kupewa kama ni wapiganiaji uhuru ama kama ni wazalendo wa nchi hii. Kisha ningeluliza serikali iweze kutoa ardhi kwa wale watu ambao tunaambiwa ni squatters. Serikali ina ardhi kubwa sana ambayo ni government land, kuna trust land, wakishamaliza hapo ndio waanze kuingilia ardhi za watu binafsi bila kuwanyan'ganya. Kwa mfano ikiwa kuna mikataba na ardhi za wamaasai ama za Wazurui, au wale tunavyoambiwa maili kumi ya pwani ya Kenya. Hawa watu sio sawa kunyan'ganywa haki zao, ni vizuri wafukuzwao walipwe ridhaa halafu ndio hizo ardhi zigawanywe. Asante sana.

Com. Riunga: Asante sana Bwana Sefu kwa hayo maoni yako. Mwingine atakuwa ni Bwana Gideon Lolo. Hayuko? Jacob Mwangandi.

Bw. Mwangandi: Sisi, tuliandika memorandum yetu iko tayari na ilipelekwa tayari na Asst. Chief, lakini nitaongea tu machache halafu niende. Kwanza, jina langu naitwa Jacob Mwangandi nikiwa pia mimi ni mkaazi wa sehemu hii ya wakilishi bungeni ya Magharini, nikitoka katika sub-location ya Shomele. Kwanza, ningetaka kutoa maoni yangu kuhusu Katiba, Katiba yetu iwe na utangulizi, maana utangulizi ndio kifunguo cha yale ambayo yako ndani ama inatoa mwelekeo kuwa ni mambo gani ambayo tungetaka yawe katika Katiba yetu. Kuhusu Katiba pia, ningependekeza kwamba muundo ule wa kwamba Katiba yetu inaruhusu bunge liwe na mabadilisho ya Katiba ikiwa imepata kuungwa mkono na 65% ya kura za wabunge, hiyo iendelee. Kuhusu raia, tuliandika mengi lakini kwa kijuu juu ninasema, wanaopata kupewa uraia wa moja kwa moja ni wale wazaliwa wa

Kenya. Hali nyingine zinazo mfanya mtu akapendekezwa kuwa raia, mtazipata katika hiyo memorandum.

Kuhusu ulinzi na usalama: Walinda usalama tunapendekeza kwamba tuhakikishe kwamba wanaangalia kweli masilahi yetu kama wa Kenya na majeshi ama walinda usalama tulipendekeza kwamba waajiriwe katika ngazi za taarafa, kwa mfano, kwa wakati huu tunaweza kusikia ya kwamba maaskari ama majeshi wanaandikwa na ukifika pale unapata kwamba wale ambao wataandikishwa hata ingawaje itakuwa katika District level, lakini bado kuna uwezekano kwa wengine kuandikwa kazi wakiwa hawatoki katika sehemu zile ambazo zinahusika. Na hivyo tukianza kushambuliwa, unapata kwamba wale askari ambao ni watumwa sehemu hiyo, wengi hawatoki sehemu hiyo, na hivyo inakuwa wanachelewa chelewa mpaka watu huku wanataka kutatizika. Lakini ikiwa ni askari ambao wametoka katika sehemu hiyo, waliandikwa na kwao ni huko, basi watasikia ule uchungu ya kwamba watu wao wanateseka na hivyo ninafikiria hawatachukuwa wakati mwingi kabla ya kufika kule. Hata ikiwa ni ngazi za kitaarafa lakini tulipendekeza kwamba, hawa Asst. Chiefs wahakikishe kwamba wanatoa majina kwa wale maafisa wanaohusika, kutoka zile sub-locations zao. Kwa hivyo, ikiwa ni Magharini Division, kwa mfano, tunajua maaskari wataandikwa lakini wanatoka zile sub-location ambazo zinapatikana within that Division. Hivyo, ina maana ya kwamba watakapata ni wale wale wakutoka sehemu hiyo na watazingatia kazi zao kisawa sawa.

Halafu tukaja upande wa rais. Rais tulipendekeza kwamba aendelee kuwa na ule uwezo wa amri jeshi mkuu wa majeshi ya silaha, lakini bunge pia lihusike katika uwezo wa kutangaza vita. Katiba iruhusu uwezo wa kipekee kutangaza vita na majanga mengine lakini tukishirikiana pia na bunge. Bunge liwe na uwezo kuhusu hali ya hatari.

Vyama vya kisiasa: Katiba iwe na muelekeo katika kuhusu uundaji uongozi na hata tabia ya chama. Katiba iwe na utaratibu wa kupunguza idadi ya vyama vya kisiasa. Kwa wakati huu, vyama vya kisiasa vimekuwa vingi sana. Na hata tukiangalia nchi zingine zilizoendelea, vyama vya kisiasa sio vingi namna hii. Lakini kwa sababu kuna uhuru wa kuunda chama, katiba iwe na muelekeo wa kuhakikisha kwamba ukifuatwa huo muelekeo hivi vyama vitapungua ili visiwe ni vya mbali ama viweni ni vya kikabila, lakini chama kiwe kinaweza kuungwa mkono na angalao 25% ya wananchi, katika majimbo matano. Kule kwao kinachotoka na kiwe na sehemu pia kuungwa mkono namna hiyo, ili kiwe ni chama ambacho kinaonekana ni cha kisiasa lakini si cha jimbo moja ama sehemu moja kutoka nchi hii. Shughuli za chama zigharamiwe na chama chenyewe, kinaweza kikatafuta fadhili na hali zingine zozote zile za misaada, lakini fedha za umma zisigharamie shughuli za chama kimoja. Na ikiwa ni fedha ya umma itatumika, basi ihakikishe kwamba vyama vyote vingine pia vinapata mgao, kwa maana hizi pesa za umma zinatoka kwa wananchi wote. Kwa hivyo, haitakuwa vizuri chama kimoja kijichukulie kama kinavuna zaidi.

Uhusiano wa chama na dola uwe namna hii, kwamba vyama vya kisiasa viheshimu dola ama viheshimu ile serikali na pia serikali nayo ihakikishe kwamba inaheshimu vile vyama, kwa sababu kwa kusema hivi ni kwamba, wakati mwingine upinzani unapotoa hoja, hata ikiwa nzuri lakini kwamba imetolewa na upinzani, pengine chama kile ambacho kinachotawala hata kikawa hakitakitilia maanani, lakini kuwe na kule kuheshimiana na vile vyama vya upinzani pia viheshimu serikali. Kila kitu kizuri kinachofanywa na serikali, kile chama hata kama ni cha upinzani pia kionekane kwamba kinaunga mkono, sio kwamba ni vya

upinzani basi vipinge kila kitu hata vizuri vipingwe. Na kwa sababu mengi tuliyaandika katika hiyo memorandum yetu, hapa ninasema tu aina ya serikali ambayo tulipendekeza katika sub-location hii, ni kwamba serikali iwe ya majimbo, kwa hayo, ninashukuru. (*Clapping*)

Com. Riunga: Asante sana, mwengine ni bwana Wilson Mwaro.

Bw. Mwaro: Asante sana kwa kunipatia nafasi hii, wageni na wenyeji. Jina langu ninaitwa Wilson Mwaro, kutoka hapa Gongoni. Maoni yangu ya kwanza ni kwamba serikali itusaidie lakini sio sisi kuisaidia serikali. Ninasema hivyo kwa sababu mahali popote utapokwenda siku hizi, unaambiwa onana na wazee, unajambo kubwa kabisa na huna pesa na umeenda kwa kituo chochote kama ni hospitalini, kwa chief, polisi, unaambiwa toa mzee ndiyo mambo yako yawe sawa sawa, onana na wazee, hii ni serikali ya namna gani? Tunasaidia hiyo serikali ama inatusaidia sisi hiyo serikali. Onana na wazee, mimi sina kitu na mtoto wangu amekatakatwa na panga. Je, huyo mtoto wangu atapono kweli? Haya mambo yanachukuliwa kimateso mateso kwa nini? Tunataka serikali hii iwe na ulinzi. Katiba yetu mpya iwe na ulinzi kama ule wa mwingereza. Mwingereza alikuwa kumuotea mtu tu na kisu hivi unaenda kufungwa. Sasa tunachukuliwa kimateso mateso kabisa, mtu anakatwa panga hapo, unaenda polisi unaambiwa gari hakuna, mambo mengi, ama kama umeenda kwa chief, unapiga ripoti kwa kitu fulani, inachukuliwa mateso mateso tu, mpaka hiyo kesi uiache. (*clapping*)

Hiyo ni mambo gani, serikali gani hiyo ambayo inatutesa namna hii? Pili, tunataka ma-chief, ma-sub-chief wapigiwe kura wote kama vile madiwani na wabunge. (*clapping*) Tunataka Katiba hii yetu mpya ifanye hivyo, kwa sababu afadhali DO kama huyo anaaweza kupewa transfer akaenda kwao, akaenda pahali pengine, lakini ikiwa chief ni mbaya, mnamvumilia awatese kwa muda siui gani.

Wakipigiwa kurua hakutakuwa na kudharauliana, lazima ahudumie wananchi, lakini kule kuchaguliwa maofisini, hamjui mtu ni mzuri ama ni mbaya, nyinyi mwasema naye hapo, mnachagua nyinyi, ma-DO, na DC, mnawachagua mnajua nchi yake ni gani ama yeye ni mzaliwa wa wapi au akili yake iko vipi (*clapping*). Mnamchagua ofisini aje kusumbua watu. Tunataka tuchague wenyewe sisi, wapigiwe kura hawa ndio wataheshimu watu lakini kama hawatapigiwa kura, wanadharau watu hawa ma-chief na ma-sub-chief.

Tatu, tunataka kuundwe kamati ya kupokea misaada kutoka nje, Kenya nzima. Katiba yetu ifanye hivyo hii mpya, kwa sababu misaada hii inayotoka nje ikija ikipokewa na serikali hatuipati. Tunaambiwa mtapata lakini hampati kabisa hii misaada. Ikiwa ni chakula, ikiwa ni fedha, tunapewa kidogo zingine zinachukuliwa na serikali, ni msaada wa namna gani huu? Tunataka kuundwe kamati ambayo itapokea misaada yote inayotoka nje, katiba yetu mpya ifanye hivyo. Nne, tunataka kuundwe kamati vile vile ambayo italinda katiba yetu mpya, kwa kulingana na wale wapenda hongo, wenye matumbo makubwa, wataharibu hiyo Katiba kwa shauri ya hongo, wanaotaja zile sheria za Katiba waanze kuchukua mahongo, hiyo ndio kuharibu, tunataka kuundwe kamati itakayo linda hiyo Katiba, yetu mpya.

Tano, polisi nayo na itusaidie, kwa sababu kuna mtu amekufa ghafla, wanambeba wanakwenda naye, wakishampima kule, anawekwa mortury, halafu nyinyi wenye maiti hiyo munaanza kuhangaika na pesa za kwenda kuuchukua kule, kwa nini wasimrudishe na hao ndio watu wa kutusaidia sisi. Polisi ni wasaidizi kwa wote, je ikiwa anauchuku maiti unaenda nayo huko, na mimi nikachukue pesa niaanze kuchukua gari, nilipe gharama badala ya mazishi nianze gharama ya kuchukua mtu kutoka kwa hospitali. Hata mimi nasema kile ni zaidi ya hii. Polisi itusaidie kwa kuja kuchukua mtu amekufa ghafl, kama tuko na gari, kama amejitia kitanzi, wampeleke halafu wamrudishe. Sio wewe mwenye mtu ukamchukue mwenyewe, kutakuwa na gharama nyingi za mazishi, na kwenda kuchukua mtu mortury, kwa nini wasimlete? Ndio nikasema hii serikali tunaisaidia ama inatusaidia sisi? Umekuja kubeba mtu, mpeleke, kwa nini wewe unaniachia mimi kazi, sina gari, sina pesa, mazishi yananiangalia, hii ni taabu gani? Sasa kuna mengi ya kusema lakini nitasema la mwisho.

Serikali iwe na ulinzi mkali, sio kuchukuliwa mchezo mchezo. Katibu yetu ifanyo hivyo, hii mpya. Unaenda kupiga ripoti juu ya kitu cha maana, pengine bibi yangu ameporwa, amechukuliwa, mtoto wangu amekatakatwa, mimi mwenyewe nimeumizwa na wakora, unaambiwa angalia wazee. Hii waangalie wazee na liondoke kabisa jina hilo katika serikali hii, na katika Katiba yetu mpya. Hatuitaki, la kuangalia wazee kwani ni kutoa pesa tu hakuna kitu kingine. Lakini ninasisitiza sana ma-chief ma-sub-chief wapigiwe kura. Kwa hivyo serikali iwe ule utu na kuna mengi sana lakini wengi watataka kusema, nikisoma hizi karatasi zote, nitachelewesha watu.

Com. Riunga: Asante sana mzee, mwingeni ni James Baya Toya.

Bw. Toya: Jina langu ni James Baya Toya, kutoka hapa Gongoni. Sina mengi sana ni machache tu. Ninazungumza hivi kwamba, twanyanyaswa sana na serikali yetu kwa sababu ya machief wetu ambao hawachaguliwi na kura. Mbeleni, ilikuwa chief wanachaguliwa kwa kura za mlolongo, sasa hakuna kitu kama hicho. Ni application waandike ziende kule halafu anazunguka ili amuone yule kule, afadhali huyu, anachaguliwa mtu ambaye hata hatufai, akirudi hapa anatumiza sisi. Mimi ninapigwa panga au napigwa magongo, nifika pale ninaambiwa toa pesa ushtaki yule mtu aliyekuumiza. Ninatoa pesa pale, baada ya kutoa pesa kumpa chief, ananiambia hebu zungumza na askari pale. Nikumuona askari ananiambia toa shilingi mia nane kumfuata mtu wako huyu, huna pesa basi baki hivyo hivyo. Kwa hivyo, tunapenda serikali yetu ambayo tunayo sasa, lakini inatumiza, mukirudi kule waambieni tunaumia sisi huku. Mambo yale yanafanyika hapa pengine hata huko Nairobi hawajui, lakini hapa ndani msituni, tunaumizwa na hawa ma-chief. Baada ya kula pesa anakuambia zungumza na aksari kule, ndipo mtu wako atafuatwa, ukimfuata askari, anakwambia utoe pesa mia nane kutoka hapa mpaka kamada ndio ufuate mtu wako. Je mimi sina kitu, atafuatwa kweli mtu huyu? Itabaki hivi hivi mpaka mwisho wake utaacha umehadhirika kwisha. Kwa hivyo, Katiba yetu inasema hawa machief ikiwa hawawezi wakapigiwa kura kwa sababu wao wamekuwa serikalini kwa muda mwingi sio sawa, ma-chief wapigiwe kura kama zamani. Sasa serikali ichunguze ma-chief wapigiwe kura. Haiishii hapo, baada ya miaka mitano akiwa anafanya kazi vizuri, tumrudishe tena, akiwa amekosea, afutwe kazi apendekezwe mwingine. La sivyo, afanywe transfer kama vile inavyofanywa ma-DO, wanatoka hapa mpaka Bungoma na kutoka Bungoma mpaka Nairobi. Kwa

nini hawa hawawezi kuondoka hapa, kwa nini na hapa wanaumiza watu baada ya miaka hamsini na tano ndio anaacha kazi? Inafanya wale sasa wanajivuna wanasema ukitaka, usitake ni mimi tu mpaka miaka yangu ifike ndio nitafute retire. Tumechoka na hayo, serikali ichunguze sana ya watu hawa.

Yangu ni machache tu, ma-chief wapigiwe kura na ikiwa hawatapigiwa kura, ataandikwa tu kichinichini basi awe na mkataba kwamba akikosea kabla ya miaka hiyo kufika atashtakiwa. Hivi sasa ikiwa chief alinikosea, nikitaka kushataki chochote, ananiambia nitoe pesa, baada ya ku-retire nikitaka kumshataki huyo chief ama hata kabla ya ku-retire, wale wakubwa wananiuliza, nina haki gani ya kumstakai Chief? Kwa hivyo, tumechoka, nikitaka kumshtaki chief amekula mali yangu, ninaambiwa, wewe unashtaki chief, utatuachia nani hapa? Tumechoka, wale ma-chief wawe wakipigiwa kura au wawe wakipigwa transfer kuenda mahali kwingine kule.

Com. Riunga: Asante mzee. Ingesaidia sana kwa sababu sasa tuko na watu wengi, kama watu labda wasirudie neno moja mara nyingi kwa sababu tumeandika mara ya kwanza. Sasa tuko na bwana Alfonse Changawa. Hayuko? Karisa Mwakiti, karibu mzee.

Bw. Mwakiti: Asante sana kwa kunipatia nafasi hii. Mimi ni Karisa Mwakiti, kijana kuzaliwa kadu. Katiba yangu inasema, vile ninavyotaka mimi na wala nitauliza wenzangu, sisi watu wa huku Malindi au coast, hatuheshimiwi na mali zetu kwa sababu gani? Kwa sababu, mali yetu ni kama mti wa mkaua ule. Nikataka kula, sifai kula mimi, kesho ninaweza nikaaambiwa wewe lete hii mali yako, inachukuliwa inaenda. Nikifika kule, yule mtu akifika pale anaambiwa, eh umekuja wewe toa uchukue, ni sawa? Kwa hivyo mimi ninaomba niheshimiwe na mali yangu, ikiwa ni mti wangu kama huu, ikiwa ni mahindi yangu, ikiwa ni maembe zangu, mti wowote wangu, niwe ninatumaini nao. Ikiwa mti wangu sina tumaini nao, itakuwa ni sawa kweli? Kwa hivyo ninataka katika Katiba, iheshimiwe na mali yangu pia. Yangu ni hayo.

Com. Riunga: Asante sana mzee. Bwana Hamisi Omar.

Bw. Omar: Kwa jina ninaitwa Hamisi Omar. Ninashukuru sana kwa hii nafasi. Nilikuwa naomba katika hii Katiba iwe ya majimbo, maanake ukiangalia siku hizi ukienda kwa wahindi hapo, ukitaka kutafuta kazi, mwanzo unanyanyaswa sana, halafu ile kazi ambayo utapew sio kama wenzetu kule bara wanavyo pewa. Utafanya ile futi ya shilingi mia sita, kwa shilingi mia tatu. Kwa hivyo mimi ninaomba Katiba ibadilishwe iwe ya majimbo. Pili, ninaomba sana hivyo mambo ya shule iliyosemwa iwe ya bure, iwe hivyo kabisa, kuanzia nursery mpaka Std. Eight. Kule kwingine tunaeza endelea wenyewe. Tatu, tunanyanyaswa upande kwa wa ardhi. Unaweza ukwenda kwa shamba ukapata hilo shamba umenyanganywa ukapewa mtu mwingine, unaambiwa hiyo iko na title deed, na wewe umekaa hapo kwa muda wa miaka mingi kuanzia babu yako, mpaka wewe mwenyewe umekuja kukaa, unakuja unaambiwa hiyo ardhi ni ya mtu mwingine, ametoka nje unaambiwa hiyo ni ya mtu mwingine, sio ya kwenu hata ondoka kabisa. Utakuja kuta hapo pamewekwa mawe umelala nyumbani ukija hapo asubuhi unapata hiyo shamba yako imewekwa mawe, ukienda kuuliza unaambiwa hata hujulikani hapa. Yangu sio mengi, ni hayo tu.

Com. Riunga: Asante sana. Bwana Rajab Mwasalu?

Bw. Rajab: Asante sana bwana Commissioner mwenyekiti, wanatume wa marekebisho ya Katiba. Kidogo macho itanitiza, ningomba bw. Tinga ambaye ndio msaidizi wetu katika District na katika Division, aje anisaidie kidogo kwa kusoma hizi makaratasi. Miwani yangu nimesahau kule nyumbani. Ningomba msaada kutoka kwa Kingi ambaye ni coordinator wa marekebisho ya Katiba. Ninaomba unisomee ndio liingie kwenye recorder.

Maoni yangu kabisa niipendayo ni hii ambayo tunatarajia kuiunda sasa. Katiba hii tuliyonayo hivi sasa, haituongozi vyema katika masilahi yetu sisi wakenya. Inasaidia viongozi wetu na matajiri wakubwa, sisi tuliowadogo hata tumesahaulika katika budget ya masilahi, ukulima na ufugaji, na huu ndio uti wa mgongo wa mwanachi wa Kenya. Hii Katiba tulio nayo sasa haimsaidi mtu, inasaidia matajiri, haisaidii mwajiriwa wala mfanyi kazi wa kampuni yeyote, hii katiba tulio nayo sasa inatunyanyasa, haitupe uhuru kufanya jambo lolote. Ninaunga mkono kubadilisha Katiba na sheria. Bunge liwe likichaguliwa baada ya miaka mitano kwa jimbo lote la Kenya. Kwa hivyo kuwe na majimbo, kwanza kumchagua waziri mkuu, naye achague katibu wake na serikali tumchague Rais, naye achague makatibu wake, rais ashirikiane na waziri mkuu. Muundo wa mseto ambao mamlaka ya nchi yatagawanywa baina ya rais na waziri mkuu. Waziri mkuu awe na mamlaka ya kunagalia majimbo yote ya serikali ya majimbo maalum. Muundo wa serikali ya majimbo ambapo mamlaka ya nchi na bunge yamegawanywa baina ya serikali kuu na majimbo maaluma ni kumchagua governor wa kila jimbo ili awe ana uwezo na wabunge na macouncillor wa kila jimbo. Ninaoimba serikali tunayo sasa isiende kwa uchaguzi wa kitaifa kabla ya maoni yetu sisi wanainchi kukaguliwa kwanza kwa sababu ikiwa ni Rais wa Kenya tunaye, na kila division tuna mbunge na councillor. Kwa hivyo, mambo ya Katiba yawe na muda mzuri. Tukimaliza Katiba ndipo tuchague serikali mpya ya majimbo. Ahsante.

Com. Riunga: Asante sana Rajab. Sasa ni John Simiyu

Bw. Simiyu: Kwa jina ni John Simiyu. Mimi maoni yangu ni haya. Serikali ya Kenya, kwa mfano, kulikuwa na sheria ya Mazurui zamani, ambayo ilikuwa inasema ya kwamba wamazurui wawe na haki ya kilomita kumi ndani. hiyo ningeaona kama ingebadilishwa itupiliwe mbali, kisha isahaulike kabisa. Mtu awe na haki ya kuishi mahali popote, kufanya kazi mahali popote, mtu wa bara awe na haki ya kumiliki shamba hapa na mpwani awer na haki ya kumiliki shamba, awe na haki ya kufanya kazi hapa, awe na haki ya kufanya kazi bara, awe na haki ya kuoia hapa, awe na haki ya kuoia kokote kule, sheria hiyo iendelee. Kuna haki pia ambayo ninaona kama kidogo tunanyanyaswa haki ya binadamu, mwanadamu ana haki ya kuzaliwa, ana haki ya kuoia, ana haki ya kufurahi vile anavyotaka, anywe vile anavyotaka lakini hapa tunahaki ndio ya kuzaliwa na haki ya kuoia, lakini hatuna haki ya kutengamana. Unapata wazee wamekaa wawili watatu, wanakusanywa, wananyang'anywa vile vidogo ambavyo wanavyo. Hiyo pia ichunguzwe kisha itengenezwe kabisa. Hii sheria ambayo inanyanyasa sana mwananchi, ni hii ya haki ya mtu anauzia mwingine shamba kisha ashamaliza siku mbili, tatu ndani ya hiyo shamba, amezaa watoto wake pale, unaona anakuja kufukuzwa na yeye mwenyewe ndio aliuza hiyo shamba kwa sababu masikini hana haki. Hiyo sheria iangaliwe

sana kisha itiliwe maanani zaidi. Mtu atakaye muumiza mwengine kidole, hata afungwe miaka ishirini. Ni hayo tu.

Com. Riunga: Asante sana. Bwana Charles Karoki, inaonekana hayuko. Tafadhali tukimye kidogo ili tuweze kisikiza mapendekezo ambayo yanatolewa. Florence Baya karibu.

Bi Florence: Kwa majina ninaitwa madam Florence Baya. Mimi ninayo machache ya kusema. Kulingana na Katiba iliyoki sasa, ni yule tajiri azidi kuwa tajiri na masikini azidi kuwa masikini zaidi. Na hii inaletwa na mambo ya ufisadi. Tunaona kila sehemu ufisadi umejaa, kwa hivyo tungeomba kila sub-location iwe na kamati ya kuchunguza ufisadi, yaani kuanzia kule chini kabisa kuwe kuna kamati ambayo itachaguliwa iwe inachunguza mambo ya ufisadi peke yake. Kwa upande wa hata kwa ma-chief na hizi departments tunazo huku kwetu Magharini. Hapo hapo hivyo, nikisema upande wa ufisadi ndio umezidi kutudidimiza zaidi, yaani umetunyanyasa sana hata kwa upande wa uajiri. Mtoto amesoma, amemaliza masomo anataka kwenda kutafuta kibarua, utakuta kama ni upande wa hizi forces, tuseme Kenya Police, ni lazima utoe kitu kidogo, unakuta mtu ametoa hata elfu tano ama hata kumi ndio aajiriwe hiyo kazi ya polisi.

(Tape 2)

Ukienda upande wa afya, unakuta mahospitali tuko nayo, hizo facilities ziko lakini haziwezi kutusaidia kwa ajili kama wewe ni masikini, nimnyonge unapitishwa huku unaambiwa hivi, unakuta kama hujaonana na daktari kimlango wa nyuma, mgonjwa wako anaachwa, anapitwa anaangaliwa mtu ambaye ana kitu, mwishowe hata pengine utakufa mlangoni kabla ya kupata matibabu. Lingine ni kama lile lililozungumziwa, kwamba ma-chief na manaibu wao wawe wakipigiwa kura, kama ni wenyeji wa huku ama ni wazaliwa wa huku tuchunguze hali yake, tabia zake tunazijua, tutampigia kura na tunajua atatuhudumia kivipi na akiwa anakosea wakati wowote hatimizi yale mahitaji ya raia, tuwe tunauwezo wa kumuondoa wakati wowote natuchague mwengine.

Tukienda kwa upande wa mashule, sisi wanawake kwa jumla, tunanyanyaswa kwa upande wa elimu. Kuwe na haki ya kila mtoto, yaani watoto wasibaguliwe, wasichana na wavulana. Ikiwa mvulana ametunga mimba msichana na ikiwa bado wote wanasoma, unakuta kwamba kuna gharama ya yule mtoto anahitaji kutunzwa. Sasa yule mvulana ambaye atakuwa amekifanya kitendo hicho, agharamie hiyo gharama, kuandikwe maid atakaye angalia huyo mtoto, tena atoe maziwa ya mtoto na mama yake aendelee kusoma mpaka amalize. Lingine ni hili, ikiwa mwanaume wameoana na mwanamke, umemueka kinyumba, hata kama ni miezi miwili, halafu uje ukosane na yeye, useme unataka kumuacha, unahakikisha kuwa unampatia usaidizi wote, hata kama nikugawanya vyombo, ama kumpatia hata kitu chochote cha kuweza kuanza business yake. Sio umemtumia, badala ya kwenda kufanya kazi unakaa na yeye anakufulia, umemuweka nyumbani anafanya kila kitu halafu ukienda unamuachilia hivyo hivyo anaenda kuanza maisha nahizo taabu zake huko mbele. Kwa hivyo umpatie hata kama ni kitu fulani umgawie na yeye aende akaanze maisha huko mbele. Maoni yangu ni hayo, asanteni.

Com. Riunga: Asante sana mama. Tunafuraha kumkaribisha sasa makamu wa mwenyekiti wa Tume, mama Abida Ali Aaroni

ambaye ni Commissioner, tutakuwa na yeye katika kikao cha leo alikuwa safarini kidogo, karibu. Sasa yule mwingine ni Bwana Safari Chalo, kama hayuko tuko na Hamisi Baya.

Bw. Hamisi: Nilikuja kitambo hapa na tangu nije sijashiba hata leo, hivi munavyoniona basi sijashiba na sijafungwa hata leo. Kwa hivyo, mimi Katiba yangu ninataka majimbo, democracy ya (inaudible) haifai. (applause) Munipe nafasi tukienda mashamba, mimi nilikuja kitambo zaidi ya miaka arobaini, na elfu milioni ninaambiwa hii shamba sio yako. Kwa hivyo, Katiba yetu ituangalie vizuri sisi tunanyanyaswa kubwa sana wazee wetu wa kilimo. (clapping)

Com. Riunga: Justus Kazungu, kutoka hapo tutaenda kwa Ali Kombe.

Bw. Kazungu: Maoni yangu haswa ningependa rasilimali ziweze kuwafaidi wale wenyeji. Sababu zangu ni kwamba, utakuta rasilimali badala ya kuwafaidi wale wenyeji, zinazidi kuwazorotesha, mfano mzuri ni hapa tu. Ukiingia upande huu mwingeni utakuta kwamba hii rasilimali haswa hata ukienda nyuma bibiliani, utakuta kwamba hiyo ni baraka kutoka kwa Mungu. Wana wa Israel waliaambiwa nenda kule, wale wakaenda na wakapatiwa ile ardhi na ile ilikuwa ni rasilimali yao, waishi kulingana na vile ambavyo watakuwa wamepatiwa. Lakini utakuta badala sasa itufaidi sio hivyo, inazidi kutuzoretsha. Hapo chumvi, iko tajiri anatoka huko na pesa zake zote, nyingi kabisa, anakuja hapa Gongoni, hii ni rasilimali ambayo tunatakiwa sisi wenyeji ambapo hiyo ni itufaidi, lakini badala yake utakuta kwamba analipwa penine shilingi mia moja au pengine mia moja na hamsini kwa siku, ambazo hizo haziwezi kumtosheleza mahitaji yake. Sasa hili ni jambo la kusikitisha sana ambapo serikali ya wakati huu haiangalii hiyo hali ya wale raia lakini wanachukua ili ifaidi kutoka kwa wale matajiri. Ambapo sasa ningependa hii Katiba ambayo inataka kuundwa ihakikishe kwamba wale ambao wanajisikia kwamba wanauwezo wakutumia rasilimali, kama ni chumvi, wahakikishe kwamba rasilimali ile inasaidia wale wenyeji. Kuwe kuna percentage kama, 20%, na ile 80% achukue yeye kwa sababu amegharamika, lakini hii 20% ihakikishe kwamba inaenda kwa raia ambapo hiyo itawasaidia kwa kama shule yetu hapa, au shule tofauti tofauti katika hiyo area. Dispensary, bara bara, hiyo utakuta kwamba hiyo rasilimali ingesaidia. Sasa utakuta, ukija kwa mtu binafsi ambapo yeye analipwa shilingi mia moja kwa siku, utakuta kuwa anaenda pale anafanya kazi, na hiyo ataondoka na maumivu na hiyo mia moja haiwezi kumtosheleza, manaake akitoka hapo akifika nyumbani hana kitu. Kwa hivyo, ningependekeza kwamba, rasilimali kama chumvi, msitu, mfuo, tuhakikishe kwamba kinachotoka pale kwamba 20% inasaidia raia. Bahari, itusaidie, chochote ambacho kinatoka pwani ihakikishwe kwamba hicho kinatusaidie.

Pili, hiyo ni upande wa rasilimali, hii ni upande wa majimbo. Mimi ningependekeza majimbo. Na sababu utakuta kwamba, ikiwa si majimbo kama hii serikali ambayo tuko nayo kila kitu inatatiza, hata kama ni ile chumvi itaenda huko, lazima iende huko ndio tugawanyiwe tena. Sasa hiyo utakuta kwamba inagawanywa katika sehemu tofauti tofauti ambapo wewe mwenyeji hupati chochote lakini kama ingekuwa ni ya majimbo, yote ingalikukwa hapa Mombasa au pengine makao makuu ambapo ingetusaidia sisi wageni. Ninapendekeza majimbo kwa kila hali, utakuta kwamba hii majimbo itatusaidia kwa sababu (haya ni maoni), na hata ikienda huko inaweza maoni yangu yakakubalika au pengine yakakataliwa. Sasa ikikataliwa, sasa kama serikali itabaki ile ile ambayo iko, basi ningependa ule uwezo wa rais, kwa sababu rais ndio anauwezo wa kuchagua waziri katika serikali. Sasa

utakuta kuwa kila jimbo la pwani unaweza kutkuta pengine tuko na marais pengine ishirini ama thelathini, hiyo idadi siju, lakini utakuta hili jimbo la hapa pwani, ukiangalia hivi, utakuta kuwa mawaziri ni wawili, hakuna ile hali ya kugawanya kisawa sawa. Ikiwa serikali itabakia ile ile ambayo iko, tuhakikishiwe kwamba, wale viongozi ambao watachaguliwa na rais, wahakikishe kwamba kila jimbo linapata namba sawa sawa kulingana na jimbo lingine. Hii itatusaidia pengine kwenda juu kidogo. Asanteni, maoni yangu hi hayo.

Com. Riunga: Asante sana, jiandikishe tafadhali. Nilikuwa nimempatia nafasi Bwana Erick Kombe.

Bw. Kombe: Asante sana, ndungu Commissioner, bi Commissioner na wale wote waliohudhuria. Kwanza kabisa ningependekeza Katiba mpya iweze kuleta serikali ya majimbo. Katika serikali ya majimbo, ni hiyo pekee ambayo itahakikisha kwamba kila mtu ni mtu na kila mtu ana haki. Bila ya hivyo ni kinyume cha yote, kwa sababu yatakuwa yale yale ya kwamba mimi nitakuwa na pahali pa kuishi maanake Mungu amenibariki, pia vile vile nitakuwa na mahali huko Eldoret pa kuenda kuuza na kuja kujinufaisha hapa. Jambo ambalo limezorotesha hasa mkoa huu wa pwani, tuko na mali nyingi katika mfuo, lakini huyo ni n'gombe ambaye tukonaye hapa na anakamuliwa na watu wengine, sisi wenyewe tumebaki vile vile. Kwa hivyo, serikali ambayo ingefaa, ni serikali ya majimbo. (*clapping*)

Tukiendelea hapo hapo kwenye hali ya kumiliki ardhi, ni lazima tuangalie hawa wanaodaiwa kwamba wana ardhi, mtu anachukua ardhi kisha haihudumii, kwa miaka baadaye watu wengine wanaishi pale na kitukuu chake kinakuja kuzuka na kudai sehemu ile. Baada ya kuwa tayari muda mwingi umepita, watu kama wale au hati kama zile zinastahili kukatwa baada ya miaka kumi na miwili. Kama ilivyo sasa ingewekewa mkazo zaidi, kama mtu ameishi pahali zaidi ya miaka kumi na miwili, sehemu hiyo awe na haki moja kwa moja hata bila ya kwenda mahakamani aweze kupewa hati kumiliki ardhi hiyo.

Tukirudi kwa uchumi, kabla sijasahau ningetaka kuongezea yale yaliyo zungumzwa na msemaji aliyetoka hapa. Rasilimali za kila sehemu zinastahili kuwa mikononi mwa wananchi wenyewe. Hivyo basi yeye amependekeza 20%, hiyo 20% ningesema iende hivyo hivyo kwa maendeleo ya wananchi wote kwa jumla. Lakini, tukija hasa kwa upande wa viwanda vya chumvi, ingekuwa katika Katiba kwamba ni lazima wananchi wenyewe wawe na hisa ya 60%, yule mgeni tumuachie 30% hata kama amegharamika namna gani. (*clapping*) Na hali hiyo si kwamba ati tutatowa wapi pesa, sisi tunadhulumiwa pale. Kampuni ile ikianza, nilifanya kazi pale, futi moja ambayo ni ya chumvi ya kuzaliana mara tatu, ikikuwa ni shilingi sita, unazoa unavunja na unazoa kwa shilingi sita. Leo hii imefika shilingi mia mbili, lakini hiyo yote bado haijatosheleza maanake ile futi moja peke yake ikivunjwa, zile elfu inazingiza kwa kampuni haiwezi kulinganishwa na gharama ile ya yule mtu anayelipwa baada ya kufanya kazi hiyo. Hivyo basi, ningependekeza ya kwamba, kampuni kutoka sehemu yoyote, mfanyi kazi yeyote pale, nusu ya ile sehemu anayoifanyia kazi kama ni mia mbili, mia moja iwe inaingia moja kwa moja kununua hisa katika kampuni hiyo. (*clapping*) Ikiwa kampuni ya Mombasa Salt italetfa faida ya bilioni kumi na tatu kwa mwaka, ifanyiwe hesabu kwa kila mtu ambaye anahisa pale ndani. Sasa ile shilingi mia moja mpaka ikifika miaka mitano, bila shaka utakuwa na hisa elfu tano na wewe ikifanywa hesabu, hutakosa elfu zako kumi utatia mfukoni, na hiyo utakuwa umesherehekea matunda ya uhuru, lakini hivi sasa wewe ni mtumwa. Katiba ya sasa iweze kutuondolea utumwa huo.

Pia vile vile zile sehemu za kazi kwanza ziende kwa wananchi wenyewe, 80%. Halafu ile asilimia 20% kama ni kazi ambazo zinahitaji ufundi zaidi wawe watatoka nje, lakini wale waajiriwa wote wawe wanatoka sehemu ile ile. Na sio tu kwamba wale wa vibarua, hapana, hata wale walio na ngazi za juu, hata kama ni manager, awe anatoka sehemu ile ile bora tu awe ana ule ujuzi ambao unahitajika katika sehemu hiyo. Pia tukiangalia rasilimali au uchumi wa nchi nzima kwa jumla, ningependekeza katika Katiba kuwe na sehemu au mipango kamili katika serikali kwamba kila mwananchi ambaye hayuko mikononi mwa wazazi wake, mwenye miaka kumi na nane kuendelea, awe ana sehemu fulani au malipo fulani anayolipwa kufidia maisha yake, alipwe moja kwa moja na serikali ikiwa ana kazi asiwe kazini, lakini kuwe kuna fungu fulani ambayo anapata. Hiyo, itapunguza hali ya ufisadi na hata hali ya uhalifu kwa sababu nikijua mwisho wa mwezi niko na shilingi elfu mbili zangu, sitakuwa na fikira za kwenda kuvunja duka la mtu, ninajua serikali inanifidia chakula changu, mpaka pale nitakapo pata kazi ya kujitegemea. Hiyo ningependa Katiba ya sasa iweze kujumulisha sehemu hiyo.

Nikiendelea kwa upande wa utawala, madhambi mengi yamepata kutendeka kwa sababu ya kwamba wanao tusimamia, wengi wao hawajui hata mipaka ya zile sehemu tunazozikalia, lakini iwapo ni mwenyeji, anajua kabisa sehemu hii imepakana na sehemu ya akina fulani na sehemu ya akina fulani na sehemu ya kina fulani, kwa upande fulani wa kwa chini pia vile vile. Hapo hakutakuwa na kusema hapa ni pangu ondoka, maanake kama ni hati ya kumiliki ardhi imetolewa kisawa sawa na imeanzia kutoka kwa Sub-chief, kwa DO, kwa DC, mpaka kwa PC ndio hadi itoke, ni lazima itoke hati ya sawa. Hazitakuja zile hati bandia. Mimi nimepanda minazi yangu, mpaka sasa nimeanza kula, mtu anakuja na jikaratasi lake anasema hapa ni kwangu. Ni kwako namna gani? Miaka hii yote thelathini nikihimarisha hapa, wewe ulikuwa wapi? Ati mimi ni waziri kutoka serikali ya Somalia, ni huko Somalia basi, sio hapa. Kwa hivyo hali kama ile tunahitaji kwamba tulindwe na Katiba yetu, mtu asije kutuingilia hivi hivi. Basi hiyo inamaanisha ya kwamba Asst. Chief lazima atoke katika ile sehemu anayowakilisha, Chief, DO, awe ni mkaaji na ni mwenyeji wa sehemu wanayowakilisha. DC kadhalika, awe anatoka katika wilaya ile ile na hata PC awe anatoka katika mkoa ule ule, ninafikiri hakutakuwa na hali yoyote ya kunyanyasana, ama leta kitu kidogo. Mtoto wa shangazi wako utaenda kumuomba kitu kidogo ndio umfanyie maneno, hakuna.

Upande wa elimu, ningependekeza katika Katiba iwekwe kwamba serikali lazima ianzishe vituo vya kuwahudumia vijana waliotupwa (machokora), katika ngazi za taarafa ili waweze kuhudumiwa nao. Ni aibu wageni wakiingia hapa Kenya, watoto wanaonekana wakirandaranda huku na huku, wakipokonyana mabaki ya mikate yaliyo okotwa kwenye mapipa. Ni aibu kwa serikali ya Kenya. Hivyo basi, Katiba iweze kuwachukulia ama kuwaweka maanani vijana kama wale ambao hawana wazazi, hawana mbele wala nyuma.

Kwa upande mwingine vileo. Ikiwa vileo ni haramu, vyote viwe haramu. Hakuna kileo kilicho halalishwa katika Kurani au Bibilia. Bangi ni haramu, miraa ni haramu, munazi ni haramu, Pilsner ni haramu, Tusker ni haramu, whisky ni haramu kwa maana hakuna tofauti ya mlevi wa Pilsner na mlevi wa Tusker na mlevi wa mnazi. Wote kama wamelewa hoi, watakuja kukoja hapa hadharani. (clapping) Hivyo basi Katiba iweze kutilia maanani kama ni kuhalalisha vileo, vileo vyote vihalilishwe, kuhangaishwa

hatutaki. (clapping)

Kumalizia, nitamalizia na urais. Mtu yeyote kuwa Rais, ningependekeza awe na umri wa miaka thelathini na kuendelea mpaka sitini na tano. Ikifika sitini na tano, hata kama una vipindi vya kuendelea wewe ustaafu, maana wakati huo ndio wakati ambao unajua unaelekea ukingoni na unafanya madhambi mengi zaidi kwa maana hakuna wakati tena utachaguliwa. (clapping) Pia Rais akichaguliwa, ningependekeza achaguliwe sio kwa wingi wa kura ati amepata 35%, basi hiyo haitoshi. Maanake mimi kama ni mbajuni na wabajuni katika mkoa wa pwani ni laki mbili na hamsini, na waliopiga kura katika Kenya nzima ni milioni moja, mimi ni Rais wa robo ya wale watu wa Kenya. Hivyo basi kama wabajuni ni laki mbili, mimi nitakuwa Rais wa wabajuni, sio Rais wa Kenya, maanake 75% wote hawanipendi. Kwa hivyo nitakuwa ninaongoza wale wachache, hatutaki namna hiyo. Ningependekeza Rais apate 51% kuendelea ndipo aweze kuitwa Rais wa Kenya kutoka mikoa yote, na kama hatakuwa amefikisha 51%, yule wa kwanza na wa pili wajibwage uwanjani hadi yule atakayepata 51% awe ndiye Rais wa Kenya. (clapping) Pia vile ningependekeza katika Katiba kwa sababu uhuru tulipigania kutoka kwa mikoa yote, haingefaa rais atoke pwani saa zote, iwe ni kwamba urais unazunguka Kenya nzima, mkoa baada ya mkoa, ili kila mmoja apate kusheherekea matunda ya uhuru. Kapsabet ama sehemu zile ametoka Rais kwa wakati huu, nilipata kutembelea sehemu hiyo wakati hajakuwa Rais, lakini baada ya miaka michache alivyokwa Rais, nilifika kule na nikashangaa. Sikuweza kuona vibanda vya mavi ya n'gombe tena. Kila kitu kilikuwa kimegeuka maana ni mta wa rais. Hivyo navyo tunataka mwaka ijao, rais aweze kutoka katika kijiji cha Gongoni, na hatuta pata mabanda mabanda kama haya, tunapata nyumba ambazo zimejengwa na vigae. Kwa hivyo urais uwe unazunguka kwa Provinces zote ikiwa ni imeenda Central, ienda Rift Valley, iende Western ama ije Pwani, kila moja aweze kupata. Kwa hayo machache ningepomba kukomea hapo.

Com. Riunga: Asante sana, jiandikishe. Mwingine atakuwa ni Bwana Daniel Mwanyare. Inaoneka ametoka, Samule Kazungu.

Bw. Kazungu: Asante kwa nafasi hii. Ingawa mengi yamekwisha zungumzwa na sitaweza kurudia hayo, nitazungumza kidogo sana. Jina langu ni Samuel Kazungu. Kitu ambacho wakati huu kinanishangaza ni kimoja tu, kutoka mwaka wa 1963 mpaka sasa, pwani yetu hakuna University. Watoto wetu wanasoma kweli, lakini anayepita kwenda University lazima aende bara huko akasome. Na huko kwa sababu kuna watu wengi, kuna utajiri mwingi hapati nafasi kirahisi yeye. Neno kama hilo limetufanya watu wa pwani kuzoroteka kielimu kwa sababu hapa kwetu hakuna shule kuu za kuelimisha watoto wetu, kwa nini? Serikali hii ambaye tuliitafuta kwa udi na uvumba, wabunge hawa ambao tumewachagua kutoka hapo mpaka sasa, hawajawaza chochote kuhusu University za hapa pwani. Hii bahari inaleta watalii wengi kabisa, hakuna hata chuo cha utalii hapa pwani hata kimoja, wote wanaosomea utalii ni huko bara. Mahoteli yote hapa pwani, wale wakubwa wote ni watu wa bara. Sisi tukienda watoto wetu hawapati kazi, ni kwa nini, hakuna chuo cha utalii hapa pwani. Aliye hapa ni yule wa bara na wabara wanauwervevu sana. Anamuandika mtu wa kwao anamtia hapa akitoka anamtia mtu wao, atapata wapi huyu mtu wetu? (clapping) Basi kwa hiyo, ninaona ya kwamba majimbo yangefaa.

La pili ni hili, linatuhuzunisha sana. Tuna beach plot hapa, ukitega sikio, mawaziri karibu wote wanasehemu wanazozimiliki hapa, hawana haja kujenga majumba, wanaenda kwa Commissioner of Land, akifika huko, yeye ni rahaman peke yake anaangalia, anasema hapa mimi nitachukua, anachukua. Sasa basi, sisi tuko hapa lakini ni kama hatuna chetu hapa, beach plot zote hapa, yana watu huko bwana. Wanauza wanapata pesa, sisi vizolola. (*clapping*) Nikitaka kutumia lugha yetu kuna msemu wetu ambao ni mbaya sana “mwaangalizi aharibu mambo, sasa kule kuangalia akiharibu mambo basi kule kuangalia hakuna haja kwa sababu huna unacho kifanya wewe, ni kuangalia peke yake”. Tumeangalia miaka hii yote, lakini sasa sehemu yetu ya Pwani hakuna imemalizika na watu kutoka huko, tumechoka basi, tunataka kama inawezekana serikali hii ya majimbo iwekwe. Marehemu Ngala, neno lake la mwisho, ni mimi nilimshikilia mwavuli pale merikebuni, kulikuwa kunanyesha siku hiyo, tarehe nimeisahau, alisema hivi, “munamuona yule mtu kule, kuna mtu kule anakuja, tafadhalini nyan’ganyirani”, yaani kila mtu ajaribu awezavyo aweze kushika kitu. Tafadhalini wazee wenzangu, serikali yetu ya Kanu hatuiambii vibaya hapana, lakini vile vitendo tunavyotendewa na wale wengine vinatuharibu kabisa., ndipo basi tunaona ya kwamba, majimbo yangetufaa. Kuna mama mmoja ambaye amezungumza maneno hapa naona nitarudia kidogo. Hizi nafasi za kazi ya upolisi na vile vingine, wale wanaoandikisha wale watu wa kazi, wale maofisa wanaokuja kuajiriwa ni watu kutoka kule nje, na wale watu kwa sababu wanajua, wanakuja kujiandikisha hapa, na wanachukuliwa wale wale waende huko, hapa wanachukua wawili ama watatu peke yake, wale wengine wanakosa kazi. Hiyo inafanyika basi, ndio tunasema, si afadhali majimbo basi kama ni hivyo?

Ninataka kuwaambia nyinyi waandishi tafadhali, neno hili ingawa kuna wengi walio lipinga lakini tunaona kwamba sisi watu wa pwani tumenyanyaswa kiasi kikubwa mno. Tunaomba ya kwamba ikiwa itawezekana neno hili muliangalie vizuri, juu ya mtu huyu wetu hapa mpendwa, ingawa anasaidia kidogo. Tunakilindi hapa cha Mombasa, kinachotoka hapo ni hapa kwetu, hatujasikia chochote ya kwamba kina rasilimali inayoweza kusaidia sehemu hii ya hapa pwani. Wacha hivyo basi, wale watu ambao wako hapa siku hizi, hapo hapo kilindini, mtu wetu atoke hapa akafanye kazi pale, hapati kazi kabisa. Wote walioko hapo ni wa kutoka juu, sisi tukienda hapo hatupati kazi, hata kile kibarua hatupati kwa sababu wale maofisa na manager wote ni watu wa huko juu, ndiko kulikosomwa, huko kwetu hakukusomwa. Si afadhali majimbo basi ikiwa ni hivyo. (*clapping*) Kwa sababu tuko hapa na hatupati kitu, hicho kilindi hakitufaidi, na huo uchumi nao waliofanya kazi hapa ni wanawake na wanaume, basi ukienda ukiangalia ule mshahara wanaopewa ni mbaya sana na pato lolote haliwasaidii watu wetu mpaka hivi leo. Ndipo tunasema tafadhalini, tafadhalini, tuangalie hii Katiba ya majimbo. Mimi ninajua (*inaudible*) na sababu ya majimbo kuwekwa wakati huo ni kwamba Ngala amesema, sisi mataifa madogo, wale mataifa makubwa, tukiwa hatutakuwa na majimbo tutamezwa sisi, utakuwa unataka choo, kuchimba choo lazima barua itoke Nairobi, je tutafanya maendeleo gani? (*laughter*) Ndipo Ngala akasema, ndungu zangu kueni chonjo afadhali majimbo ndipo tukaunda majimbo. Sasa basi, hakuna lifanyikalo mpaka Nairobi na Nairobi kuna wenyewe. Ndipo sasa tunasema afadhali majimbo na sisi angalao tuonje hii dakika ya mwisho. Tukifanya hivyo, Mungu atubarikie. (*clapping*)

Com. Riunga: Asante sana mzee, jiandikishe hapo. Gabriel Kazungu.

Bw: Kazungu: (In vernacular)

Translator: Asante kwa kupatiwa nafasi hii fupi kuzungunza mambo ya Katiba. Mambo haya ya kugeuzwa Katiba hayangukuwa, na vile mtoto wa kwanza alikuwa mwerevu sana, ndiposa twataka majimbo. Ya kwanza, hii Katiba mpya tunataka iwe ya majimbo. Pili ni mashamba, serikali itoe amri kwamba kila mtu apate kipande chake cha ardhi na maendelezi, title deed hatupati. Kuna wale ambao wanaenda huko juu, wanahonga honga halafu wanakuja pale kwangu na kunifukuza. Mtu yule tumfanyie nini?

Bw: Kazungu: Tatu, wale wazembe, Katiba yetu ikiuundwa ilingane na wale wazembe, wale walaghai wanaitwa wafisadi. Mtu akijaribu, akishikwa na zile pesa au akila pesa za watu wengi, yeye anafikiria anafanya werevu na serikali inaona, hatuoni hata mtu mmoja ameshikwa, ni kwa sababu gani? Mtu yule akiwa ameshikwa, why are you very broke? (laughter)

Translator: Wale wanyanganyi wa pesa wanaenda kuvunja bank wachukue ile pesa wewe uliyoweka na halafu hawashikwi. Katiba ya sasa ninataka ilingane na majimbo na watu kama wale wakishikwa wapelekwe tu jela, kuanzia miaka sita kuenda mbele. Katiba itengenezwe, mtu yule mnyan'ganyi na mwenye kuvunja nguvu zako, kuninyan'ganya mimi mdogo, ukipatikana huna kesi. Hayo ni maoni ya Katiba, ninataka tuyatengeneza yawe sawa sawa maanake ni mambo ya kesho lakini ya sasa yanafanyika hapa yameharibu mtoto yule mkubwa ule wa kwanza. (in vernacular)

Translator: Hii ardhi iliumbwa na mwenyezi Mungu, kwa hivyo wale wanaotoka kule kuja kutunyan'gaya mashamba yetu hapa hatutaki tena. Sina bunduki lakini mimi nina mshale, kwa hivyo ninaweza kufanya kitu, ukinisumbua na shamba langu nitakundunga tu na mshale. Hiyo nchi haujui wewe, unakuja na karatasi yako, hapa unasema mimi hapa ni kwangu. Hapo uliposimama, jizuie tafadhali, usichukue mashamba kwa sababu mshale utaingia kwa mwili. Katiba ichunguze hayo.

Com. Riunga: Bwana Harry Jira atafuatwa na Bwana Ngowa Chalo.

Bwana Jira: Asante bwana chairman, Commissioners, DO, DC, mabibi na mabwana. Kwa majina ninaitwa Harry Jira. Leo nina furaha sana ndani ya mwili na ninataka kuwaeleza ile furaha ninayoisikia, kwamba tumepata fursa baada ya miaka thelathini na nane ama tisa tuweze kuanzisha Katiba ambayo tunaipenda sote hapa nchini. Basi ma Commissioners muliochaguliwa mukiwa ishirini na tisa, munalo jukumu kubwa mbele ya wananchi na wananchi wote wako na imani kwenu. Ningeomba kumekuwa na matatizo ambayo mumukuwa nayo, hili ninalozungumzia ni jambo la maana sana ambalo limekuwako na nina furaha kwamba vice chairman yuko hapa pamoja nasi leo. Katika matatizo ambayo ilikuwako ndani yenu, lakini mukaweza kuyasuluhisha vizuri sana, hapo ninashukuru sana.

Kuna vipengele fulani ambavyo vinaweza kutuzorotesha katika hii Katiba yetu. Ningeomba vipengele kama hivyo vifuatiliwe ili hii Katiba iweze kufaulu kulingana na mahitaji ya wananchi wa Kenya. Katiba yetu ambayo tunaipenda, ni ile Katiba ambayo inaangalia masilahi ya watu wote pahali pote walipo Kenya. Kila mtu ana haki ya kuishi, kula, kusoma na haki ya kufanya kila

kitu ambacho anastahili kupata. Haki hizi zilipeanwa na mwenyezi Mungu. Ni haki kabisa haki zile ziwe zitatumizwa, kwa hivyo, tunapendelea Katiba yetu iangalie juu ya haki za wanadamu wote. Katika Katiba yetu ya sasa inaangalia tu haki za civil na political, tunataka haki zote ziwe zitakuweco, zitalindwa hapa Kenya. Kitu kingine, tumeona ile Katiba iliyoko iko na mamlaka fulani ambayo yamelundikizwa katika serikali ya Executive na zile area nyingine yaani Parliament na Judiciary hawana mamlaka ya kutosha. Ni mapendekezo yangu kwamba, mikono hii yote mitatu ya serikali, iwe huru, yaani independent, kuwe kuna separation of duties, separation of power, na pia wawe wanaweza kujisimamia kama nilivyosema, kipesa na kiuamuzi. Lazima kila mkono uwe nakuwa na checks and balances. Ninafikiri nikizungumza hivyo, wenzangu munanielewa sana. Hili ni jambo ambalo ndilo limesababisha hii Katiba yetu kuwa watu wanalalamika, kuwa haitoshelezi wananchi. Lakini kukiwa na mambo haya matatu, yaani separation of power, checks and balances na independence, basi shida hizi hazingekuweco. Wanaosema kuwa kuna uchunguzi wa kutosha. Mara nyingine sio kuwa tu itakuwa na kusikiza malalamishi ya watu, lakini hiyo yenyewe itakuwa na uhuru wa kufuata kazi zinazofanywa na maofisa wa serikali, maofisa wa ngazi tofauti tofauti ili kuona kuwa kuna uhaki kwa kila mtu.

Mambo ya ardhi: Ardhi kama mjuavyo, watu wengi wamekuwa wakililia haki ya kumiliki ardhi, wengi hasa wa area kama hii ya hapa, hawana titles. Titles ziko katika watu wachache, na sasa kwenda benki mtu wetu apate mkopo aweze kujistawisha kwa mambo ya kilimo, serikali ama benki zinatambua hizo tiles. Kwa hivyo, tunapendekeza kwamba, kila mtu mahali pale alipo, ikiwa ataweza kupimiwa, apewe title, ili awe ana uwezo kuendeleza maisha yake. Kitu kingine, ninaomba katika Katiba hii ambayo tunalinda hivi sasa, wengi tumeshasema kuwa ni aina gani ya serikali tunayoitaka, tumesema tunataka serikali ya majimbo, mini pia ninaunga mkono hilo. (clapping) Tukiwa na serikali ya majimbo, kila jimbo litajitawala na mapato ama rasilimali ambazo ziko pale kwa jimbo watatumia wenyewe pale, wataajiri watu kulingana na mahitaji yao, na pia mapato yale, kiasi fulani, pengine 20% itapelekwa kwa central government ili iweze kuwa na mambo ya kutekeleza kwa Kenya nzima kwa mambo ya usimamiaji wa mambo ya international relations, mambo ya security au defence. Hili ni jukumu ambalo litakuwa ni la serikali kuu ili na sisi tutambuliwe huku nchini, kwani hii nchi ya Kenya si nchi ambayo imegawanyika vipande vipande lakini ni serikali moja. Kwa hivyo, ndungu zanguni, singependa kuchukua muda mrefu manaake hili sio jukwaa la siasa, lakini ni kupendekeza yale mambo muhimu, ambayo tumekuja nayo tuwapatie hawa Commissioners ili wayaweke katika taratibu zao na watatuletee tena sisi tuyasome, ili yakiambatana nayo tuweze kuyakubalia. Kwa hivyo, nilikuwa tu ninaomba hakikisho kupitia kwa mac-ommissioners kama haya ambayo ninasema, lakini wasiwasi yetu sisi wananchi juu ya yale ambayo nimeyataja kwanza, Commission hii iwe independent. Hii ni kwamba pesa pengine hamna zakutosha, mnangoja mpaka budget ije mpewe pesa. Je, kama hamkupata pesa, mnaweza kuwasilisha haya mambo ili tukapata hii katiba tunayotaka? Na mambo mengine ni pale kipengele cha Bunge. Bunge pengine ni litoe approval katika kupitisha hii bill, halafu Bunge livunjwe. Mutafanya aje? Ni lazima tuangalie mipango hiyo yote, ifuatiwe ili wananchi wasije wakawa wamedhoofika safari ya mwisho. Kwa hayo machache ninawashukuru tena na ninawaomba kila na heri katika kupewa utajiri wetu hapa liwe ni jambo ambalo litakuwa na mwangaza kwa siku za mbeleni. Asante.

Com. Riunga: Asante sana kwa hayo maoni. Sasa tumpake ugowa chalo, hayuko, basi. Bwana Karisa Katana.

Bw. Katana: Mimi kwanza ninatoa shukurani kwa mwenyekiti waTume na bwana DO, Commissioners wetu na maofisa wengine waliokuja hapa. Kwa hivyo ninatoa heshima kwenu kwa kunipa nafasi hii ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuongea kwa maoni ya Katiba. Kwanza, ninataka niongee machache sitaenda zaidi sana maanake kutoka mwaka wa 1962 Katiba vile ivyopangwa na Rais Ngala, Rais Kenyatta na mwingine aliyekuwa na anasimamia hiyo ni Koinange. Muliwekeana ahadi ya kwamba, mutalinda mashamba ya wananchi wa Kenya baada ya kwamba yametoka mikononi mwa Waingereza. Mutalinda na mali zao zote, na hakuna fujo itakayo tokea. Lakini sasa je, mbona sisi twan'golewa mimea yetu, mashambani? Ilikuwa aje? Hili ni swali la kwanza na ninataka niliwasilishe kwenu. Swali la pili ni kwamba, kulingana na mkataba vile mlivyopeana katika wakati huo ni kwamba mliahidi ya kwamba shule, watu wote ambao kwamba ni wakenya, watoto wao na hata wale ambao wako kidatu cha juu, watasoma bure. Je, huduma hizi mbona zapotea? Hatuzioni. Kwanza majimbo ndio ninataka.

Jambo la tatu, tunaona tunarudi nyuma sana kwa sababu kwa upande wa afya pia, tunaona huduma hiyo ya afya imeanza kutuletea shida sana. Mlisema kwamba mutaahidi kwa vyovyote wananchi hawatapata shida kwa kila aina ya njia yotote na sasa tunaona kwa upande wa afya pia tumeanza kurudi nyuma maanake ukienda katika hospitali unaitishwa pesa, je mimi mgonjwa ambaye kwamba kutoka juzi ama mwezi nzima niko kwa nyumba ni mgonjwa, hizo pesa zitatoka wapi? Hilo ndilo sababu mimi ninapenda shirikisho, tena si shirikisho, basi mimi ninataka majimbo, tena majimbo sana.

Hilo lilikuwa swali ni langu la tatu.

La nne ni kwamba, wale ambao walikuwa ni wazungu walikuja wakaondolewa hapa, watu wa bara walipigana na yeye, wakati huo sisi hapa mkoa wa pwani ilikuwa iko pamoja na Tanzania na ilikuwa sio ati ni coast, ilikuwa imekaliwa na mazrui. Mazrui walipokwenda kufanya mkutanao wao na Rais Tanzania, ninafikiri hapo Governor aliwauliza waafrika akasema, sasa nyinyi wale wazungu mnataka watoke kule bara. Je, mutawalipa? Sasa Rais mwenyewe aliyekuwa wakati huo, kuna Ngala, Kenyatta, Tom Mboya na Koinange wakakaa. Governor akasema, eliwaneni mukiwa nyinyi mtawalipa ridhaa wazungu ili watoke, basi mukielewana nyinyi, mimi nitatia saina. Na tukaelewana ya kwamba wazungu walikuwa walipwe ridhaa ya mashamba yao ili watoke. Lakini ajabu ni hiyo pesa zilipokuja, zilikuja kwa mkubwa wa mji ambaye kwamba alikuwa ni Koinange. Pesa hizo zikaja hapa ili kuwalipa wale wazungu. Pesa hizo vile zilivyotumiwa ndio sasa hapo naona kwamba afadhali mimi sasa niwe katika majimbo, na majimbo damu mpaka sasa hivi. Zile pesa zilikomboa wazungu kweli. Kule wakarudi, wakalipwa pesa zao, wazungu wakaenda zao. Sasa ikabakia ni upande huu wa mkoa wa Pwani amboa ulikuwa umechukuliwa maili kumi na mazrui. Sasa ikabakia zile pesa pia wale waliokuwa ni wageni huku Pwani pia nao walipwe ili watoke, halafu hii Kadu na Kanu iwe tutachanganyika tuwe kitu kimoja. Huku pwani hawakutoka, na zile pesa wakatolewa wale na huku pwani wakabakia. Walipobakia, yale mashamba wakazuia waarabu kwa sababu hawakukombolewa maanake hawakupewa pesa. Sasa kule kubakia kwa yale mashamba mapaka dakika hii sasa, ndio sisi hatuna makao kwa sababu unakuta mtu umekaa mahali kwa muda mrefu halafu unakuja unfukuzwa kabisa. Na hilo jambo lilikuwa limekatwa kabisa. Katiba imesema itatuchunga na mashamba yetu, ilikuaje mpaka sisi tunasumbuliwa? Sasa hapo ndipo tunaona afadhali majimbo, pengine inaweza kutufaa sisi sote wale ambao ni wakaaji wa jimbo la pwani.

Kwa hivyo, kutoka leo ningependa kimaoni, Tume iende ikakae vizuri sana na mwenyekiti wahakikishe ya kwamba mkoa wa pwani uwe na jimbo lake kwa sababu tumepata mateso makubwa, kwa hivyo sasa tumefika mwisho, huko mbele hatuwezi kwenda zaidi. Kusumbuliwa, tunasumbuliwa sana, kwa sababu utakuta mtu amepanda vitu vyake shambani, mazao yetu hayaendi nje, utakuta kahawa inaenda nje, majani chai, sukari inaenda nje, lakini pombe, nazi, makuti, korosho, hazitoki, tunanyanyaswa hapa hapa, ni kwa sababu gani? Ndio ninataka majimbo mimi. (*clapping*)

Kitu kama hicho ndicho kinafanya jimbo la Pwani linarundi nyuma sana. Kwa hivyo ningependa Tume iende ikakae vizuri ili ihakikishe kwamba wale ambao ni wageni katika huu mkoa wa pwani, kama hatujapiga hizo kura watolewe wote, tubaki wenyewe kwanza tupate yale makao yetu sawa na wale watu wa bara, mali yetu na sisi iende nje. Halafu tupate hiyo kura tupige ili tuone tumekalia mashamba yetu, halafu tutaunda sisi wenyewe jinsi tutakavyoishi. Lakini sisi tupige na wageni wako hapa, hawa wageni ndio wanatunyanyasa, hatuwataki, watolewe kuanzia hivi sasa leo. Hayo ni maoni yangu. (*clapping*)

Jambo lingine ambalo kwamba ningependa kuzugumzia ni kuhusu upande wa elimu. Kusema ukweli upande wa elimu tumenyanyaswa kwa muda mrefu sana. Kwanza isitoshe, tuliahidiwa kwamba watoto wetu watapewa maziwa huku, kumbe ilikuwa si maziwa, ile ilikuwa kama kuzibwa tu macho. Sasa kwa wakati huu hatupati tena ile maziwa, basi tunapata shida kwa sababu imekuwa nikupigwa na kupokonywa ile mali ikienda huko bara huku tumebaki tu hivi hivi. Hilo jambo ndio sababu mimi ninataka majimbo, na hiyo majimbo sio kwamba ninataka kwa njia gani, ninataka kwa sababu ya kwamba, tumechoka, na sote tumechoka na watu hawa wakutudanganya kila wakati. Mashamba tunayopewa sio yale ya kwamba yanatakikana vile vilivyo, kwa nini watu wabara wanaweza kusafirisha vitu vyao nje na sisi watu wa pwani tukiwa tuko sawa, tunasema tuko sawa gani? Mara tumeshikwa, pombe haifai, mtu anaenda kuuza nazi umeshikwa huku. Sasa hiyo mambo ndio sisi hatutaki, ndio sababu tunasema majimbo ikiwako, pengine huenda ikatusaidia. Kwa hivyo, hilo ni jambo ambalo kwamba ninataka tume ikaenda ikaketi na iangalie Katiba pia ili ihakikishe tumelindwa kisawa kama hivyo ilivyoahidi Katiba ya kutoka mwanzo kwa uhuru. Kwa hivyo sina zaidi isipokuwa la mwisho.

Ikiwa Katiba hii mpya itachukulia maanani kwamba majimbo ifanyike, basi sitaki iwe ni majimbo ya jimbo la Pwani peke yake, majimbo mpaka huko bara nao pia tuwachukue pia waingie kwenye majimbo. Maanake ikisemwa ni majimbo ya hapa peke yake, kutakuwa na fujo kwa sababu kwa ufupi ni kwamba, kuna watu ambao kwamba wamemiliki ardhi zao na ni wabara, sio hivyo kwamba tugawanyane, lakini majimbo yawe ni yale ambayo mwanakenya apate haki yake hapa hapa Kenya. Kwa hivyo, mimi langu sina zaidi la kusema, langu ni hilo. La mwisho, watu ambao kwamba ni wageni waliotupokonya mashamba, warudishe sehemu zile. Vipingo estate ni kubwa hizo, shamba za chumvi ziko hapa kubwa, ni kwa nini zile rasilimali zetu tumepokonywa na sisi hatuna pahali pa kukaa, watoto wetu hawana pahali pa kukaa? Inabidi mtu usomeshe mtoto wako, akifika darasa la kumi, unakata kipande cha ile shamba unauza, akimaliza University huna pahali pa kukaa. Unakuja unabaki hivi, na mtoto wako ni manamba anatembea unachekwa tu. Watu wa bara wanakuja, wanachukua ile pia pesa umeweka benki, pengine unataka kujenga kijijumba, inakuja kubwakuliwa pale benki inapigwa mkono zinaenda zote unabaki kitupu, hilo jambo hatulitaki. Kwa hivyo ndio sababu ninataka majimbo na mimi ni majimbo damu mpaka nife na kufa kwangu pia hata pale

kaburini andika kibao majimbo, kwa hivyo asanteni. (clapping)

Com. Riunga: Asante sana. Samson Kisau hayko? Haya tumpate Jonathan Baya.

Bw. Baya: Asante sana Commissioner kwa kuja kuchukuwa maoni yetu. Mimi ni Jonathan Baya Mwanyule. Niko hapa Mapimo village, na maoni yangu ni haya; Utawala, ninataka wa majimbo na utawala wa majimbo ule, Rais kwanza awe kwa kipindi kimoja cha miaka saba pekee. Kwa hivyo, hatutaki ufalme, mtu unakaa pale mpaka unamea mizizi, hapana. Tunataka akishamaliza miaka saba, mwingine achaguliwe baada ya miaka saba aondoke. MP, tunawaandika kazi, wanakwenda kupewa kazi kule za uwaziri za nini, huku wanatusahau. Kazi za mawaziri wasipewe ma-MP, zipewe watu wengine, wafanyi biashara na tuna wafanyi kazi wengi walioacha kazi ambao wana akili wanaweza kupewa hizo kazi za mawaziri. Kwa hivyo, sioni sababu ya kwamba tuwe na mtu tumemuajiri hapa kama MP kwenda kututetea kule, anaenda kupata kazi ya waziri na inakwa ni kazi ingine, hapa tunamtaka, kule anatakikana. Hapana, serikali ni ya majimbo na Governor achaguliwe na raia kutoka government. Ikiwa tutakuwa na serikali ya majimbo, hatutaki ma-PC, ma-PC out, kwa sababu tutakuwa na Governor. (clapping) Kuanzia DC mpaka mzee wa kijiji wawe wakichaguliwa kama vile madiwani. Hizi eneo za utawala zirekebishwe sababu utakuta DC yuko Malindi, kuja huku inakuwa ratba, tuna taka DC hapa. Hii taarafa iwe district, na kila taarafa ikiwa district, DC atakuwa hapa hapa Gongoni na kila kitu itakuwa sawa. Hata wale maafisa wake tunaowataka, agriculture, wanyama (livestock), wote watakuwa hapa hapa, na haitakuwa kazi na desturi ile ya kwamba, oh sina gari ya kwenda huku, sina petroli, kidogo itarahisishwa.

Afya, ninataka iwe bure mpaka hospitali za kitaifa, kutoka hapa petu location, hospitali iwe bure mpaka hospitali ya kitaifa, mtu anatibiwa bure. Tuliahidiwa lakini hatujapata, tunataka hiyo ifanyike. Elimu, tunataka iwe ya bure, kutoka nursery school mpaka University. Na kama vile mwezangu alisema hatuna University hapa Pwani, miaka arobaini ya uhuru, hatujapata University na tuna viuo vikuu vingi hapa ambavyo vinaweza kugeuzwa kuwa Universities kama Mombasa Polytechnic.

Com. Riunga: Tafadhali tumpatie nafasi pia yeye aweze kutoa maoni yake. Asante.

Bw. Baya: Utakuta ya kwamba sisi hapa hatujui maana ya Katiba au hatujui haki zetu, hivyo basi, hii elimu ya ngumbaru iweze kustawishwa vizuri na kila kijiji hata ningesema ya kwamba yale makanisa yawe na nafasi ya kufundisha wale wazee, kina mama, kina baba, waweze kujua kusoma na kuandika. Hivi basi utakuta ya kwamba hizi Katiba zitakazo kuja tutaweza kuzisoma vizuri sana.

Ardhi, kuna wengi waliochukuwa ardhi kiholela, hivyo basi serikali katika Katiba yetu, hii Commission ya Njonjo iimarishwe na iweze kuchunguza vizuri kabisa kwa nini hawa watu walipata ardhi kiholela. Biashara, ningesema biashara iwe bure, isiwe ya licence. Utakuta mama anauza nazi zake za shilingi mia moja hapo na anatakiwa banda. Tunataka ile biashara ya shilingi kumi mpaka ya shilingi elfu mia tano isiwekewe licence, Katiba iseme biashara ya namna hii iwe bila licence, ili tuweze kupata kazi.

Kwa sababu hakuna kazi ya kuandikwa, unasoma mpaka University hakuna kazi, hata serikali inasema twende nje kutafuta kazi. Hizi county council, inaonekana zinafanya duplication. Mimi ninasema county councils ziondolewe kabisa katika Kenya. (laughter)

Inafanya kazi mara mbili, kwa hivyo ibaki tu mabaraza ya miji, kama vile Malindi municipal, city council, town council, urban council na village council. Kwa mfano, hapa sisi hatuna council, watu wanajenga kiholela holela na baada ya muda tutataka mji, itakuwa wale watakao kuja kuendesha mji huu wanapata taabu. Kama tuna village council hapa, ingeweza kupanga mambo kisawa sawa. Kwa hivyo kuwe na village council.

Kina mama wanafaa, maanake, ndio wanazaa kila mtu duniani, hakuna mtu alizaliwa na mwanume. Wanafaa wahudumiwe kisawa sawa, lakini swali langu ni kwamba, haki yao ni nini? Ningeomba Katiba iangalie Katiba ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu Mungu aliiweka Katiba kwa mwanaume na mwanamke na hiyo Katiba ichunguzwe sana, tusije tukapotea. Hiyo Katiba mwenyezi Mungu aliyotupatia iangaliwe vizuri sana lakini ni haki wakina mama tuweze kuwahudumia vilivyo. Maji: Tuliambiwa ya kwamba baada ya mwaka wa elfu mbili, kutakuwa na maji kila mahali, mpaka leo Gongoni hatuna maji. Tulikuwa na miradi wa maji, imekufa na mto uko hapa karibu tu na hapa pia panatoka maji mengi sana, lakini hakuna maji, tunataka serikali iweke kwenye Katiba kwamba, maji hapa yapatikane haraka iwezekanavyo.

Majeshi: Ikiwa majeshi wanaajiriwa utakuta ni huko bara tu kama wenzangu walivyosema. Ikiwa majeshi wanatikikana elfu moja, kila mkoa upewe nafasi ya kuwa na majeshi sawa sawa. Sio upande mmoja wanapewa majeshi mia tano na Pwani wanapewa wanajeshi watatu. Utamaduni: Utamaduni udumishwe katika Katiba yetu, utamaduni ni muhimu sana, asiye na mila ni mtumwa. Kwa hivyo, utamaduni katika Katiba udumishwe haswa zile utamaduni za kienyeji. Ziko tamaduni zile hazifai, sawa zitupwe, lakini ziko zingine zinafaa sana na zafaa kuhifadhiwa. Pamoja na misitu, mali ya asili, maji haya ya chumvi, tuweze kutumia wenyewe hapa. Lakini tunasema ya kwamba elimu ni kidogo, tuna kitu ambacho kinaharibu elimu hapa, Gongoni. Kumejaa video chungu nzima na utakuta video watoto jioni ndio wamejaa katika hizo video. Katiba iweke kwamba video zisiingie watoto wadogo kama vile bar, watoto wa miaka chini ya 18 hawaingii. Kwa nini hizi video watoto wa miaka mitano wanaingia? Kwa hivyo, video zipigwe marufuku kwa watoto wadogo, isipokuwa awe na miaka 18 ni sawa anaweza kuenda huko kuna video kwa sababu zinaharibu. Yule mwenye video anapata pesa, watoto wanaharibika, tunaenda kushika kina mama wanaouza tembo lakini hatushiki wenye video ambao wanaharibu watoto, mambo gani hayo? Kwa hivyo video zichunguzwe sana, zinaharibu watoto wetu.

Mimi ninaunga mkono uridhi kwa akina mama. Bwana anawachana na bibi yake na yeye anaenda zake, kwa hivyo hilo jambo la uridhi kwa bwana na watoto lichunguzwe sana, kwa sababu watu wengi hawajui habari ya uridhi. Ninarudia Katiba iweze kufundisha watu katika elimu ya ngumbaru, makanisani, hata ikiwezekana kama kuna nafasi misikitini ili watu waweze kujua Katiba ni nini, haki yake. Hiyo Katiba kufundishwa watu kila mahali iweze kupanuliwa. Nina hii memorandam nitatoa.

Com. Riunga: Asante sana, sasa tutawaita akina mama. Sofia Joseph, atafuatwa na Esther Murakesi. Karibu mama.

Bi Sofia: Mimi ninashukuru sana siku ya leo kwa sababu niko huru kuchagua Katiba ile ninayoitaka. Mimi niaonelea kina mama sana wananyanyaswa sana kulingana na vile ilivyo Katiba ya siku hizi. Wanamama hawana haki ya kuridhi mali yeyote hata kwa mababa zao, hata mabwana zao. Ningeonelea Katiba ichunguze ile wamana wawe na haki yao ya kuridhi. Lingine ni kwamba kuna wamama ambao wemezaa bila kuolewa, na wamama hao utakuta hawana nafasi ya kusomesha watoto, na hii Katiba ya sasa ningeonelea ichunguze wamama wale ambao hawajiwezi watoto waowakaweze kusomesha na serikali. Na nikisema ya kwamba ninahitaji majimbo ni kwa sababu ya vile watu wananyanyaswa kutoka nje, utakuta hata maaskari ambao wameajiriwa kuwa na kielelezo chetu, utakuta ya kwamba ukienda pale kwa ofisi ya chief, ya maaskari, huna uwezo wa kuhudumiwa mpaka utoe pesa. Hapo ni kwamba tunataka watu ambao watakuwa wakichunguza vile ambavyo askari wanavyofanya, kwa sababu wananyanyasa wananchi.

Jambo lingine ni kwamba utakuta wabunge ambao wanasema ya kwamba, tunawachagua wataleta miradi ya maji, watajenga mahospitali, watajenga kila kitu, lakini utakuta anapoenda humuoni hapa, huyu mbunge anastalihili hata kama ni miaka mitano asimamishwe, aondolewe kabla ya miaka hiyo tano. (*clapping*)

Jambo lingine ni kwamba, utakuta wahindi wamejaa sana katika mji huu wa Gongoni, na wanakuja bila sisi wenyewe kujua wanakuja namna gani. Lakini ukichunguza utakuta ni wakubwa walioko Nairobi ndio wanajua vile wamekuja. Wenyeji hapa hawana haki kabisa kwa sababu utasikia barua imetoka Nairobi bila wenyewe kujua hapa, wanapewa ma-plot, wanapewa kila kitu. Hilo ni jambo Tume ichunguze Katiba hiyo irekebishwe kwa sababu watu wananyanyaswa sana. Jambo lingine ni kwamba kuna waalimu ambao wanaingilia watoto wa shule, ambao utakuta yeye ni mwanafunzi wake na anaenda kulala naye. Wakati analala naye utakuta yule msichana anapopata mimba hatamuhudumia, anataka yule msichana aende wapi? Ikiwezekana hawa walimu na wafanyi kazi wote wa serikali ndio wanaleta watoto chokora. (*clapping*) Kwa hivyo ni haki hiyo ichunguzwe sana kwa wafanyi kazi wa serikali.

Lingine utakuta kwamba machief wale wetu ambao wanatusaidia hapa, unasema unakimbilia kwa chief ama kuna mababa watoto waliowekwa kwamba mtu awe anasaidia watoto. Unapoenda huko utakuta ya kwamba, yeye pia anapopata hongo, huwezi kusaidiwa kwa sababu mtoto hana uwezo. Hilo pia Tume iangalie sana, Katiba ikiundwa hiyo iwe moja wapo. Na wamama wawe huru kila mahali wanapoweza kuandikwa kazi. Jambo lingine ni kwamba utakuta msichana hakumaliza form four, amebakia darasa la nane, utasikia hakuna kazi unaweza kuajiriwa. Hapo Tume ichunguze sana, wamama wengi hawamalizi shule lakini wanahitaji msaada wa kupata kazi. Hiyo ni kwamba lazima tuwe na viwanda vyetu tuvimiliki wenyewe. Majimbo peke yake ndio itakuwa kielelezo cha mwanakenya. (*clapping*)

Jambo lingine ni kwamba, sisi tunakaa hapa lakini ni kama ambao hatuko, unakuta kwamba mama mzima ambaye hajiwezi, na utakuta watu wanasoma kwa sababu wanasema ati watu bara wanasoma, watu wa coast wanasema hawasomi. Lakini unapoandikwa kazi, unataka kazi ya polisi, unaambiwa lete elfu tano kwanza ndio uajiriwe kazi, na kama huna pesa hiyo kazi huwezi ukaipata. Hiyo Tume igundue sana na ichukue kielelezo kwamba, kila mmoja anastahili kufanya kazi mahali popote.

Jambo lingine, kati ya ma-chief kuwe na kamati ambayo itachunguza wale wafanyi kazi wa serikali, wanapokosea wawe wanaweza kushtakiwa mahali popote. Utakuta sub-chief yeye hajachaguliwa, anajichagua kwa elimu yake huko na hajui watu hapa wanaishi namna gani, kwa hivyo, tunataka Tuwe na kamati ya kutuwezesha kumshtaki hata kama amekula pesa za ofisi, (*clapping*) na hao ma-chief tuwachague sisi wenyewe.

Tunahitaji wabunge kama wanachaguliwa, Mbunge akiwa ni mwanamke, councillor awe ni mwanaume na mbunge akiwa ni mwanaume, councilor awe ni mwanamke. Kwa kila pahali ambapo kuna wafanyi kazi kwa idara za serikali, mwanamke pia awepo, wanaume wakiwa ni wawili, mwanawake awe ni mmoja, wanaume kama ni kumi, wanawake wawe watano. Ni hiyo tu, sina zaidi.

Com. Riunga: Asante sana, mama andikisha. Mwingine ni Esther Mwakesi, Paula Kazungu, hawako? Josephine Kazo, Elina Mbaru. Tafadhali tuwapatie wanawake nafasi kwa sababu tumekuwa na wanaume tangu asubuhi.

Bi Mbaru. Asante sana. Mimi nina maoni haya. Katiba ambao tunataka sisi kuliunda..... Jina langu ni Elina Mbaru, ninatoka Bomani sub-location, Magharini Division. Maoni yangu hasa sisi akina mama, la kwanza kabisa, ninawasikitikia sana wale ambao ni wazee wana-rape wale watoto. Hicho kifungu cha sheria, ningaliomba kila mzee ambaye atafanya hivyo mtoto wa kike, kwa maana sheria imewekwa lakini haifuatwi, ninaomba ile mishipa ambayo yanamfanya yule mtoto mpaka anaenda kufanywa mambo mengine hospitali, yeye in'golewe. (*clapping*) Abaki tu bwana wa kawaida lakini mishipa mingine iwe haifanyi kazi. Sisi akina mama tunadhulumiwa sana hasa kwa upande wa uridhi, hatutambuliwi na mabwana zetu. Sisi mabibi ni viumbe vya kukusaidia katika nyumba sio kuchukuliwa kama punda, mwanamke si punda ya wanaume. Mwanamke ni msaidizi katika nyumba, lakini utaona hapa, hasa mgiriana, tunatumiwa sana. Bwana anapoaga dunia, at least ile mali ibaki na yule mama pamoja na watoto, lakini anapoondoka yule mzee, wale ndungu zake wanasema hukuja na mali, utaondoka hivyo hivyo. Tunataka hicho kifungu cha sheria kirekebishwe tafadhali. (*clapping*)

Pili, tumekuwa akina mama hasa ni waoga kabisa, kwa mambo ya serikali ya Kenya, utaona hata wakati watoto wanapoandikwa vibarua ama kazi zimeandikwa, announcement zimekuja katika DC's office, ya kwamba kunatakikana Kenya Army, Kenya Air Force, ni vigumu yule mtoto kwenda kuomba kwa sababu anahakika, hatapata hiyo kazi kwa sababu hao invigilators watakao simamia ile interview pale, watakuja na watu wao kutoka pahali pengine. Hata yule mtoto hataipata ile kazi, ukisema ni watu wa coast nyinyi hamkusoma, hatukusoma tuna kazi gani kwani sisi twafundishwa.

Tunataka sheria irekebishwe, na ikiwa wakati tunaandikisha hawa watoto vibarua, tunataka kila mkoa au district iwe na number yake, kama ni kumi Malindi, tujue watu kume wataenda lakini si kudanganywa na askari ambayo hayaeleweki. Serikali hii inatunyanyasa sana sisi akina mama, utaona mama amedhulumiwa hapa, sasa anataka msaada pale polisi, ili aandikishe mambo yake ili afile case yake kortini, utaona yule mama anaulizwa, umebeba pesa ngapi? Useme unamkimbilia chief, chief wangu atanisaidia, ukienda kule kwa chief, Commissioners, tuko na shida sana.

Mimi pia ningeliomba, serikali tutakayoiunda, kwa sasa iwe ya majimbo ili kila jimbo lijitawale lenyewe. (*clapping*) utaona hiyo

kilindi hapa Mombasa, ni njia moja ambayo ni source ya Kenya inaleta mapato mengi sana, lakini mapato yale si mwananchi wa hapa anayefaidika. Wale ambao wanafaidika pesa zikusanywe hapa zipelekwe serikali kuu, na huku kwetu hakuna chochote. Ma-dispensary zenyewe, nituzisimamie sisi wenyewe, mtu ukienda pale kama Malindi hospital, mama ni mja mzito pengine mtoto anatoka vibaya, unatajikana elfu tatu ndio aingie huko theatre. Bila elfu tatu haingii, sasa yule mama na yule mzee hawana chochote, ni serikali ya kulala ama ni serikali ya kuundana hii? (*clapping*) Kwa hivyo, mimi ningeliomba maoni yangu kila jimbo litawale lenyewe.

Kwa upande wa kazi, mkituambia hatukusoma, kama mzee Rimba alivyozungumza ya kwamba colleges zote ziko Nairobi, basi kama sisi hatukusoma hata kule kuinua mgongo mkubwa aingie ni vibaya. (*clapping*) Wanatoka huko, mnakuja kutunyanyasa kila siku, sasa inakuwa sisi ni tuwafuutilize nyinyi. Mambo ya ardhi, mimi nimezaa niko na bwana wangu pale, najiona mwenyewe niko huru, kesho ninaambiwa, nyinyi sio wenye hii title deed, ondokeni kwa sababu hii ardhi ina mwenyewe. Sasa mama anaanza tena kun'gan'gana na watoto, yule anafanya hivi, hapa kuna askari rafiki yangu, wamemshika yule ambaye anayesema ndio bwana, ameshikwa kiuno amevutwa. Ondoka, aliyekuambia ukae hapa ni nani? Kama aliyeiba lakini yote ni ardhi peke yake. Sasa tunataka ardhi iwe ya mwanakenya yeyote, hakuna mambo ya maili kumi, hakuna mambo ya sijui ni ya nani, iwe ardhi ni ya mwananchi wa Kenya, amiliki mwenyewe. Kwani sisi tuna laana? Sisi hatuna laana wapwani, Mungu alitubarikia, alitupa hizo factory za chumvi, ni vile serikali haisimamii vizuri. Pengine jambo lile lingewasaidia wananchi wa area hii kwa hivyo mimi ningeleomba serikali ijayo iwe ya majimbo, ili kila jimbo litajitawala lenyewe. Kuandika ma-askari, ma-chief, tunachagua wenyewe na mlolongo, maana kusema ule ukweli, basi hizo idara ambazo zinaambiwa zina mahongo ama ya kitu kidogo, lakini idara hii ya ma-Asst. chief to chief zimezidi. (*clapping*) Nikifika tu pale, mimi nimekosana kwa mpaka twende unisaidie kule, utasikia huo mpaka niwe na mbuzi na shilingi mia tisa za kiti cha mzee. Kwa hivyo, ningaliomba serikali iwe ya majimbo.

Tatu, uwezo wa Rais ni mkubwa, upunguzwe, kwa sababu akiwa yeye Raisa na amezidi kabisa, nialale asubuhi na hatugawanyiwi ile haki. Ona kama ministers, Rift Valley wakona waziri kumi, huku kwetu ni wangapi? Wawili, Nassir na Ngala, ile haki iko? Hatuna haki sisi, kwa hivyo tunaomba hii serikali inayokuja, hata kama ni watatu lakini Rift Valley ni kumi, wametushinda, tunaomba wale wa Rift Valley ni wakenya, hawa pia ni wakenya. Tunaomba zile haki zigawanyiwe kila mtu, ili tuweze kujivunia nchi yetu ya Kenya. Na tunaunda hii Katiba kama alivyozungumza Harry Jira, mambo haya nyinyi Tume ambayo mumetumwa, muwe munatusikiza na mnayanakili halafu munatuletee tusome. Lakini tusiwe tunazungumza hapa halafu mambo yenyu yatajibiwa baadaye baadaye, tutarudi pale pale, ya kwamba hakuna chochote ambacho kitaendelea, mwananchi wa hapa coast aendeleo kubaki vile alivyo na sisi hatutaki kubaki vili tulivyo. Kwa hivyo, tunaomba, mnapoenda na wale wenzetu vile watatoa yale maoni yao, ule uwezo wa Rais wa kusema, fulani nimeitoa, nimeweka mwengine, uwezo ni huu, hiyo nayo ipungue, hata kama haita pungua sana lakini at least iwe kidogo, uwezo wake ni mkubwa sana maanake ile atakalosema yeye ni hilo hilo. Kwa hivyo, tunawaunga mkono kama mlivyokuja lakini tunawaomba mambo haya muyanakili, mutuletee tena.

Haki zetu sisi akina mama ziweze kuzingatiwa na waume wetu pia waweze kututilia maanani, ya kwamba kiumbe cha mwanamke ni mke ambaye ni msaada, lakini si mwanamke wa kupigwa. Na akiwa atapiga bibi yake mpaka azirai, mwanaume

yule awekwe jela miaka saba. Asanteni. *(laughter/clapping)*

Com. Riunga: Bila shaka akina baba wamesikia hayo maoni. Tungali bado na akina mama. Edna Mwandoe, hayuko? Anna Samuel, Elizabeth John. Akina mama mungetaka tuwapatie nafasi tuzungumze mtuambie mambo yenu tukiwa hatuna akina baba ama mnataka muwe pamoja? Kanze Katana, Felista Kerema, Sidi Baya, Paskarina Mweni, Sidi Masha, Mapenzi Ngoa, Nyevu Masa, Kazo Mzungu, Rachael Mwarandu, Priscilla Randu, Anna Mweni. Sasa vile tutafanya wakati wa lunch, tutapatia akina mama nafasi yao, tutabaki nao watupatie maoni yao. Inaonekana wanaogopa akina baba. Sasa tutaendelea, Jonathan Baya, A. M. Luganje.

Bw. Luganje: asante sana Commissioner. Mimi kwa majina ni Albert Mulanda Luganje. Kwanza ninataka serikali ya majimbo. Ninataka kueleza na sababu zake, ni majimbo peke yake ambayo itatufaidi sisi wa Kenya sote kwa sababu kila jimbo lina rasilimali zake za uchumi na kila mmoja anamila zake. Basi tukiseme serikali iwe ya majimbo, jimbo la pwani linapato yake, jimbo la nyanza lina mapato yake, na utamaduni wake, jimbo la kati vile vile. Lakini hii serikali moja ni nzuri, lakini hata kizuri kikitwea chumvi nyingi, sikinaharibika?

Audience: Ndio.

Bw. Luganje: Kwa hivyo, tunasema majimbo kwamba ndio suluhisho. Tuchukue mfano tu, nataka twende haraka, Mombasa, pale kilindini, kama siokukosea, labda meli moja ikufunga safari pale, kama si kwa saa ni siku, elfu mia tano, rasilimali za Pwani. Je, ni wangapi tunayo ifaidi hiyo? Kama sio siku moja elfu mia tano, ni saa moja elfu mia tano. Ni meli ngapi zinafunga safari pale, kama nikusoma tunaambiwa hatukusoma, ndio ni sawa, hakusoma, lakini katika Kenya nzima, utalii mwingi ni Pwani, iko wapi college ya utalii, iko bara. Mimi Luganje nikipata nafasi ya kwenda college, nitapotea hapa Mombasa ama katikati ya njia. Ikiwa wale wa Nairobi wazaliwa wa kule, kila siku tunasikia yule amepotea, yule amepigwa risasi, je mimi masikini Luganje nikiingia Nairobi sijui, si wale wenyeji watajua huyu ni mgeni tu, si ndie wakuanzwa kunyan' ganywa? *(laughter)* Nitafika huko Utalii college? Sitafika huko, mutasema hawakusoma, sikupatiwa ile nafasi. Lakini je, kama utalii college ingekuwa Malindi, haki ya Mungu siningefika? Sasa tunakuta utalii uko hapa lakini tunatawalwa na wale ambao wamepata nafasi, umepewa nafasi, njoo utalii college kesho ama kesho kutwa, tumepotelea Mariakani, nafasi si lazima itaenda? Kweli itaendewa na Katana hii, haitaendewa na Katana. Ndiposa tunasema majimbo ili kila jimbo lijitegemee lenyewe. Na mapato yote ya jimbo lile, 20% iende kwa serikali kuu, lakini pesa zote za hapa na uchumi wetu, zibaki hapa. Hatusemi majimbo ile mtu wa bara afukuzwe, la, lakini uchumi ule wanaochuma hapa, ule ushuru ukipatikana ufaidi jimbo hilo. *(clapping)* Huku si kubaguana lakini tunataka rasilimali. Kama mapato ya kilindini yote yatoka milioni ngapi, 80% ihudumie hili jimbo la Pwani. Kule pia vile vile hakukosi kugawanyana, kutendana haki, hapo nimeondoka.

Elimu, iwe ya bure kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la nane. Halafu ile system ya maziwa, ililetwa nisuluhi, lakini badala ya hiyo ingerudishwa ile system ya kutoa vitabu na kalamu kwa shule kwa sababu unakuta mtoto kila siku, mimi nina watoto wasiopungua watatu, wako dalasa la kwanza, sita na la nane, lakini kila siku nisipokua na mia moja, basi itabidi nirauke sana maanake mtoto atataka kalamu, yule anataka kitabu, yule wa darasa la nane anataka vitabu kumi, ili wakiamka, baba yuko

wapi? Ametoka (laughter). Sasa atasoma kweli huyu? Huyu hatasoma, kwa sababu vifaa hakuna. Hapo ni upande wa elimu, haki za akina mama zitambuliwe kulingana na utamaduni wa sehemu anayotoka kwa sababu kama ni uridhi, kama si kutogithi, lakini kila kabila lina mila zake, iangaliwe kulingana na mila ambazo ni za kabila lile na ziheshimiwe. Tukifika upande wa sheria, sheria ziko mara mbili kuna sheria ya kuandikwa, kuna sheria za kitamaduni, lakini tunan'gan'gana mahali tukifika kotini, sheria ile ambayo iko kitabuni ndio ambayo inathaminiwa. Tunaomba Katiba itambue zile sheria za kitamaduni tukifika kotini ziwe na uzani sawa na zile zingine, ili isionekanae, kwa sababu nimeletewa karatasi halafu wewe angalia hii, unaushaidi wa makaratasi, lakini karatasi, na kuna watu ambao wanaoweza kutoa ushahidi kabisa kuhusu jambo lile, lakini wale sio chochote kuliko hiyo karatasi. Kweli hizi karatasi ukitia kwenye moto, zitapiga nduru, lakini mtu ukimtia kwenye moto atapiga nduru. Sheria za kitamaduni zipate uzito sawa na zile sheria za kawaida.

Bunge liwe na kipindi cha miaka tano, Rais awe na kipindi cha miaka mitano. Uwezo wa Rais, rais abaki amri jeshi mkuu, lakini awe na uwezo wa kuteua bunge maalum kulingana na idadi ya wabunge katika vyama, lakini mbunge maalum asipatiwe waadhifa wowote wa uwaziri au waziri mdogo. Kwa sababu ni hivi, mimi nimekataliwa na wananchi, umeniteua kama mbunge maalum, halafu unanipatia wizara, yule mpinzani wangu sitamhudumia katika wizara ile. (clapping) Kwa hivyo mbunge maalum awekwe, lakini asipatiwe wadhifa wowote, asiwe waziri, asiwe waziri masaidizi kwa sababu anaweza kutumia kofia ile ile akamthulumu yule mchaguliwa kule ambaye atakuwa anaumiza wananchi kwa njia nyingine. Kwa hivyo waziri akiwa ni waziri awe ni wa kuchaguliwa na kura. Rais awe na uwezo wa kuteua mawaziri, wabunge maalum lakini Katiba ionyeshe wazi kwamba mbunge maalum hana nafasi ya kupatiwa cheo cha uaziri au waziri msaidizi. Basi, ikiwa vile, itakuwa inatulinda zaidi. Jambo lingine, Rais awe anaweza kuvunja bunge kupitia kushauriana na wabunge, ikiwa kuna hali ya lazima. Jambo lingine, Katiba hii ambayo tunaiunda sasa, tukisikia kwa magazeti, sisi hatukusoma, tunaambiwa vile, mara Commissioners wenyewe wanagongana pale, vuta ni kuvute hivi, hata kama muda utakuwa mchache. Ikiwa hii Katiba haitakamilika, vipengele fulani viondolewe ili uchaguzi ujao uwe wa majimbo halafu nyinyi muendele. (clapping) Lakini ikiwa itakwama vile, na Katiba yetu inasema miaka tano tuwe na uchaguzi, tutachagua serikali ambayo ina msingi wa Katiba hii hii ambayo hatuitaki sasa. (clapping) Kwa hivyo, ikiwa wakati ni mfupi sana, na munahitaji muda wa mambo mengine kutekelezwa, lakini kile kipengee ambacho kinasema serikali ya Kenya ni moja, kiondolewe kiwekwe cha majimbo, tuchague majimbo, mambo hayo kwisha, halafu nyinyi muendele, kuna ubaya hapo?

Response: Hakuna ubaya. (clapping)

Bw: Lunganje. Lingine, watumishi wa serikali. Kuwe na Tume maalum ya kuchunguza mishahara ya watumishi wa serikali, kuwe na Tume maalum ya kuchunguza mishahara ya wabunge, kwa sababu tuangalie mfano, na kwa sababu ninaamini hii Tume ni ya kujitegemea, sitaki nifuatwe nyuma kwa nini ulisema yale pale. (laughter) Mbunge kwa wastani anapata shilingi elfu mia tano, na huo mswaada ulipitishwa baada ya wiki moja tu, ukapita mara moja. Je, kama kuna tume lingine tofauti, kweli hata mimi niambiwe Luganje tukae hapa ninataka tuongezewe mishahara, mahali ninahusika, sinitasimama mara moja tu. Kwa hivyo, kuwe na Tume ya kuchunguza mishahara ya watumishi wa serikali na ya wabunge maanake mbunge mmoja, tuseme tu, mahitaji

ya shule kwa mwanafunzi kil siku ni shilingi mia mbili, ukiwa na ustani, fanya hesabu wewe unayejua hesabu, elfu mia tano kwa mwezi unalipia wanafunzi wa ngapi, maelfu ya kuhesabu, mwezi moja tu. Na ni kwa sababu wabunge wenyewe wamekaa pale wakapendekeza tule hiki tuache hiki. Lakini kama tuna Tume maalum ya kuchunguza mishahara ya wabunge, haingekuwa vile, kwa hivyo ninapendekeza Comminssioners, mshahara ya wabunge kuwe na kitengo maalum cha kuchunguza mishahara yao. Watumishi wa serikali vile vile, ikiwa aliyenifundisha akiwa mshahara wa juu ni elfu kumi na tano, si dhambi hiyo, kweli kutaenda watu peponi? (laughter) Hakuwezi kwenda watu peponi na waalimu wangu, ambaye mwalimu wako ni babako anakula makate mkavu, wewe hapa sausage, Blue Band na nini, kwa sababu mshahara ni kidogo, haifai ndungu zangu, haifai hata kidogo, hafai hata kwa mungu. Kwa hivyo, mishahara ya wabunge ichunguzwe.

Utumishi, utawala wa mikoa uweko, lakini uwe namna hii, kwa sababu kuna jambo ambalo lazima tuizungunze ikiwa utawala Pwani umebaki, lakini kama DO anakuwa transferred, kwani sub-chief akiwa transferred kuna shida gani? Hakuna shida kama ni ya sub-location wa Gongoni apelekwe maarafa, apelekwe Ganze, Tana River. Si ni utumishi tu? Mbona hawa wandungu zetu wako hapa ukiwauliza hawa wanatoka hapa Gongoni kweli hawa? Ni utumishi tu. Kwa hivyo, utawala wa mkoa ubaki lakini kuwe na transfer kutokea sub-chief mpaka provincial level. Nimesema utawala uwe wa majimbo na wale wanaopigania urais, awe ni moja kutoka jimbo fulani halafu pia sio ndiye governor wa jimbo lile, awe ni mzaliwa wa jimbo lile, lile.

Mahali pengine, nirudi pale kwa bunge kidogo. Nina summarise, bunge baada ya kipindi chake, bunge likivunjwa, lazima kiwe na mtu anayeshikilia ile serikali maanake Katiba yetu inasema. Rais lazima awe mbunge, bunge likivunjwa speaker wa bunge awe sio mbunge, ashikilie serikali kwa kipindi kile ambacho uchaguzi utaendelea halafu yule atakayechaguliwa kama Rais, aje apatiwe ufunguo na speaker wa bunge, kuna dhambi hapo? Hakuna dhambi, lakini je, bunge limevunjwa, nani anayeshikilia serikali, munashindwa mtakayemchagua, nani? Hakuna. Kwa hivyo, bunge likivunjwa wabunge wote warudi nyumbani na speaker ashikilie ufunguo baada ya uchaguzi kila moja atarudi pahali pake. Basi ninataka kumalizia hapo na nimesema asanteni sana Commissioners, lakini serikali iwe ya majimbo na ikiwa ni ya majimbo tuheshimiane na mali zetu kwa sababu hapa Pwani ndio mahali ambapo zawadi inatolewa, anayepatiwa ardhi, ukichunguzwa amekuwa mkubwa serikalini, enda Pwani uchukue ardhi huko haina mwenyewe. Kwa hayo machache au mengi Mungu awabariki, kazi yenu iwe nzuri na mfanikiwe. (clapping)

Com. Riunga: Asante mzee Luganje, andikisha hapo. Kama tulivyosema, sasa tutapatia akina mama nafasi na tutawaomba akina baba kwa heshima waende lunch kidogo tutabaki hapa na akina mama. (noise) Hakuna ubaya, tutaenda pahali kidogo kwa sababu sasa ni wakati wa break ya lunch, halafu tutasikiza akina mama. Tulifanya hivyo hata kule kwingine. Tafadhali mtusikize, vile ilivyo iko ni kwamba wakati tulienda huko Kakoneni, tuliombwa na akina mama kwa sababu tulikosa akina mama kuongea halafu wakatwambia tuwapatie nafasi yao. Hii sheria tunayofuata inasema ni lazima tupatie kila mtu nafasi ya kusema vile angetaka, akina mama wakasema tukipatiwa nafasi yetu tukiwa akina mama kwa sababu shida zetu wakati mwingine ni tofati, hatuwezi kuzitaja mbele ya watoto na mambo mengine, ni sawa. Kwa hivyo, saa hii ni lunch break anyway, lakini badala ya kwenda lunch, tungetaka kuzungmza na akina mama, hiyo ni haki yao kama wangetaka kutoa maoni. Kwa hivyo, tutarudi hapa saa nane tuendelee, maswali tutauliza saa nane, tutafuata ile list iko.

Speaker ??: (In vernacular)

Translator: Nilipokonywa shamba na Keah wa Tamba, akaiza kwa mtu mwingine, Keah wa Dumbuwa. Hilo shamba langu liliuzwa elfu saba na mia tano. Nikamwambia sitaki, akaendelea kukata mpaka ile shamba sasa ilikuwa atupe, akaenda kwa chief na chief naye akamruka, amesema hata hivi ni mwisho kuwa mimi ni masikini hata ninataka nikate nusu nimpe. Lakini karatasi sina, kitambulisho sina, sasa nifanyaje ma-chief? Nimekuja kulia kwenu, ikiwa mtanisaidia munipe kitambulisho na karatasi mniambie, maanake shamba langu litaenda na Keah wa Dumbua hata hivi ninataka afukuzwe. Amefukuzwa majivuni, akafukuzwe na huku Kambi ya Waya. Sasa hapo alima kwa nguvu, mimi ninataka aondoke kabisa, ninataka afukuzwe, nimesema hata nimechoka mimi, shamba langu niendalo anapanda tu. Nifanyaje ma-chief na ma-DO? Basi ninaona uchungu na shamba langu nilipewa na baba yangu sasa baba amekufa, sasa ninasumbuka, machief sasa nifanyeje na ma DO? Nimekuja kwenu kilio, sasa chief amerudi nyuma maana niko masikini.

Esther: Kwa jina ninaitwa Esther Mwakesi, mimi maoni yangu ninayopendekeza katika Katiba ni kuhusu mambo ya wanawake. Unakuta mwanamke anaoelewa kwa muda wa miaka mingi halafu akija awachane na mume wake, anamfukuza hampatii hata angalao sehemu kidogo ya kuenda kujiendeleza kimaisha. Na unakuta hata wengine wanasema, wewe mpaka unilipe mali yangu, ndio uolewe na bwana mwingine. Sasa yule mwanamke unamkuta wakati mwingi anapata shida katika hali ya maisha. Jambo lingine, ningependelea kuhusu hawa vijana. Vijana wa huku coast kusema ukweli, wengine kimchezo ni wazuri, lakini unakuta kwamba wa huko bara ndio wanapewa nafasi nyingi ya kujiwakilisha kimchezo, unakuta wengine wamepelekwa chini fulani huko, hawa wa coast hawapewi nafasi nzuri ya kujiendeleza kimchezo. Maoni yangu ni hayo.

Com. Riunga: Niko na swali kidogo kwa sababu nilisikia hili jambo hata kule tulikuwa. Kulingana na mila zenu, nikisema sasa ukifukuzwa na bwana yako ni lazima sasa urudishe ile mali ilikuwa imelipwa?

Esther: Ndio, kutegemea na huku wanaendeleza hiyo mila, mwanamke akifukuzwa na bwana, alipe ile mali, sasa ndio tunaomba Katiba iangalie jambo hilo, kidogo akina mama wapate kujiendeleza na wao.

Com. Riunga: Na watoto wanaenda wapi?

Esther: Watoto kusema ukweli wanaambiwa ni wababa, kwa sababu yeye amelipa pesa ya mahari. Sasa tunaomba Katiba isaidie sana akina mama waweze kujimudu kimaisha maanake kina mama saa zote wanawekwa nyuma.

Com. Riunga: Asante sana. Edan Mwadoe, halafu Anna Samuel ajirayarishe.

Edna: Kwa jina ninaitwa Edna Mwadoe, mimi nilikuwa ninasema Katiba igeuzwe kama vile upande wa coast, kama vile

makampuni headquarters zake ziwewe coast na za up-country ziwewe huko up-country ili watu wa coast wapate haki yao. Na makumpuni, first priority ya kikazi ipatiwe watu wa coast kwanza. Na mimi ninapendelea majimbo.

Elizabeth John: Ninaitwa Elizabeth John. Oni langu ni wanawake ambao wanaachwa na bwana zao, sasa anapata usaidizi kwa serikali kuwa baba watoto anapewa watoto wake, anarudi kwa babake. Serikali inasema chukua mtoto wako na wajukuu wako ukalee. Sasa yule bwana kule atachukua bibi mwingine na atakuachia watoto wako. Sasa utakaa pale baadaye baba yako atakufa, pale ambapo amekuambia kaa hapa, wale ndungu zako wa kiume waanze kukufukuza. Sasa tunasikia kwamba kuna urithi kwetu kwa kuzaliwa lakini bado hatujajua uridhi tutaupata kwa njia gani. Na ninasikia kuna msaada ambao watoto kama unataka kuwasomesha, msaidiwa wewe ambaye hujiwezi, huo msaada hatujapata njia wa kuuona, twafanya kusikia tu. Kwa hivyo oni langu mimi nilikuwa ninataka nijue, kama tutapata uridhi kwetu kwa kuzaliwa tujue tutaipata kwa njia gani, kama tutapata msaada sis tusiojiweza tujue tutaipata kwa njia gani.

Com. Riunga: Asante sana. Kanze Katana, Felister, Sidi Baya, Priscilla Mweni, Sidi Masha, Mapenzi Ngoa.

Mweni: Jina langu ni Priscilla Mweni. Taabu yangu ni watoto wangu, wa kwanza ako class cha nane na amefukuzwa kwa sababu ya pesa, wa pili ako class cha tano na amefukuzwa kwa sababu ya pesa, mwingine ni wa mwisho msichana amefukuzwa yuko class cha tatu. Na baba yao alivunjika mkono hana kazi, kwa hivyo wote wako ndani ya nyumba na mimi sina la kufanya. Mimi mwenyewe nimeshikwa na typhoid na pesa za kwenda hospitali, sina. Sasa tunateseka ndani ya nyumba. Yangu ni hayo, sina nyingine.

Mwaki Mfunguo: Ninatoka hapa Gongoni. Ningependa maoni yangu, Katiba ibadilike maanake sisi wanawake tunaonewa sana na mabwana zetu. Hatuna haki, tunachukuliwa kama watumwa na ni wanawake wa nyumba. Maanake ukiangalia hivi, bwana atakuja ndani ya nyumba, wewe huna mamlaka yoyote, atakuja pale aanze kukusumbua, kukupiga akupige, kama ni chakula, chakula umepika, watoto pengine wamekula wamemaliza, na yeye ameenda ulevini, akija pale, atakuletea fujo na vituko tele. Sasa ukitafta wewe mwenyewe biashara zako ufanye kwa sababu uendelee, hauwezi kuendelea, anakuregesha nyuma kila kukikucha anakuregesha nyuma. Kwa hivyo utakuta mimi sina haki yoyote pale ndani ya nyumba, mwenye haki ni mwanaume. Kwa hivyo, ningependa sisi wanawake itiliwe mkazo pia na sisi tusaidiwe na serikali. Utakuta kwenye hiki chama za wanawake pia utataka kuingia, lakini kuanzia huku kwetu sasa utaingia kwenye hizo vyama lakini utaendelea mwisho wa kuisha sasa utataka mtu pengine umefika karibu na mwisho na kuchukua pesa, utataka mtu akudhamini, sasa ule mtu atukuambia mimi sikujui, siwezi kukudhamini. Sasa ukiangalia inaendelea hivyo hivyo mpaka inaisha, hudhaminiwi na mtu, utaendelea vipi, na utakuta chama kile cha wanawake hapa hatuwezi kuendelea, kinaenda kinafia, haya, imeisha hivyo hivyo. Kwa hivyo hapa kwetu sisi tunashida, tuna taabu, kwa hivyo tusaidieni, tunaomba msaada, tusaidiwe upande wetu wanawake. Hayo ndio maoni yangu.

Com. Abida Ali: (Nyevu Masha, Kazo Mzungu, Rachel Mwalandu, Priscilla Randu, Anna Mweni, Mary Joseph, Fatuma

Faith Ngumbao: Ninashukuru wote kwa kupata wakati huu ili nitoe maoni yangu. Mengi yamezungumzwa lakini ninagusia tu kidogo. Nikianza kwa upande wa serikali, tunataka serikali ya majimbo ndio ambaye itatufaa, sitaingia ndani zaidi kwa sababu yale ambayo yamezungumzwa yanatoshea. Ya pili ni kuhusu uongozi wa serikali. Kwanza kabisa tunataka Rais ambaye atachaguliwa awe anatoka katika jimbo lile letu, awe ni mkazi wa pale kwa sababu ndio ambaye anajua maslahi ya wananchi wale wa pale. Na pia uongozi wake upatiwe wakati, uchukue miaka miaka tano, ikifika miaka tano, an'golewe achaguliwe mwingine, na ikiwa hiyo miaka mitano hajafikisha lakini anaonekana kuwa ana mambo ambayo anayafanya chini chini ambao haipendezi, awe anaweza kuondolowa kabla ya hiyo miaka tano. Na pia tukiingia upande wa Ministers, wawe wanatoka katika jimbo lile na pia hao wawe na muda na wawe wanaweza kutolewa hata kabla ya ule muda na wakifika kule iwe kazi yao ni ile moja peke yake. Sio wengine wachaguliwe wawe mawaziri au ule upatiwe cheo ni gani, tulimchagua awe akituwakilisha sisi kule, akienda apate wadhifa mwingine, atakuwa yuko mara mbili, huku anatakikana na kule anatakikana, kazi mbili, hataweza kuzifanya.

Na nikiingia kwa upande wa wanawake, haki, hasa kwa wanawake, wananyanyaswa sana. Tunataka wanawake waweze kuangaliwa hasa katika uridhi na hata hawa ambao wanatia mimba wasichana, awe ni mwalimu, awe ni mwanafunzi, awe ataangalia yule mama na hata mtoto pia awe na uwezo wa kumtunza hata kama hana kazi, lakini ni jukumu lako kwa sababu ndiye aliyezaa yule mtoto. Sasa ukimuacha yule mwanamke, yule mtoto atatunzwa na nani, ndio sasa tunapata machokora wamekuwa wengi kwa sababu ya hiyo. Na tukiingia upande wa mayatima, wao wawe wanaangaliwa kwa sababu ni upande wa wale ambao hawajiwezi. Hawana njia, hawana wa kuwategemea, sasa serikali iwaangalie wawe wanaweza kuwapatia haya mahitaji yao. Pia wale wasiojiweza hawadhaminiwi kabisa katika serikali hii. Wao wawe wanapelekwa shule zao, vilema vipofu, na viziwe na baada ya kusoma, huwa wanapatiwa kazi ambazo zitaweza kuwasaidia. Wazee wasiojiweza wawe pia wanapewa maslahi yao hasa tukiangalia misaada ya mahindi ambayo inaletwa, iwe inapatiwa wale wazee wasiojiweza na mayatima. Mashule nayo pia yagawanywe kisawa sawa, yawe sawa sawa kama sehemu hii yetu, kuwe na shule za msingi, kuwe na shule za sekondari, colleges na University ziwe zimegawanywa sawa sawa. Pia katika hii shule ulipaji wa karo kuanza nursery mpaka darasa la nane iwe ya bure na pia kuwe kuna huu msaada wa kutoa vitabu kama mwengine alivyo sema, vitabu, kalamu, watoto wawe wanapatiwa. Yangu ni hayo machache tu.

Edita: Kwa majina ninaitwa Edita Mwangi. Maoni yangu ni kwamba ile mikono tatu ya serikali. Kila mkono uwe na mamlaka yake kwa sababu wengine wananyanyaswa. Kila mkono upatiwe kazi yake wasingiliane. Ni hiyo tu.

Eunice: Kwa majina ninaitwa Eunice daktari. Kutoka Fundisha Location. Maoni yangu ni kuhusu walemavu. Kwanza, nitaanza na shule. Shule za walemavu ni chache hapa pwani hasa utakuta kama mkoa wote wa pwani shule ya walemavu ni moja na ni Port Rietz, inahudumia tu darasa la kwanza mpaka nane, hakuna kuendelea. Unakuta unajiunga na shule zile zingine za secondary ambazo hazina facilities ambazo walemavu wanaweza wawe wanatumia. Pili, ni maoni yangu sasa, kwamba kila

wilaya kuwe na hizi shule kwa sababu ni walemavu wengi wamekaa nyumbani mwao. Hawajui ni mahali gani pa kwenda, lakini kama hizi shule zitakuwa katika wilaya, wazazi wangejua ni wapi pakuwapeleka hawa watoto, wangehudumiwa vipi na wangepata vipi hii elimu ambayo ni muhimu kwa kila mmoja kwa sababu kila mkenya atakuwa amelimishwa.

Tatu, kazi. Hivi leo unaingia hata kwa maofisi ya serikali huoni mlemavu ameajiriwa kazi. Ni maoni yangu hata serikali pia nayo iwe itafikiria hawa walemavu, kuna wengine wamesoma na wengine hawajasoma, wale ambao wana ule uwezo wa kufanya kazi, pia wao nao wataajiriwa badala ya watu waone wameketi wakiomba omba na uuwahurumie tu wakiwa hawafanyii lolote ama wakiwa hawana lolote la kuweza kujisaidia wao wenyewe. Nne, vifaa vya serikali. Zile ofisi za serikali ni manyumba za ghorofa, mlemavu hata kupanda kwenyewe anashindwa. Akitaka kuona msaidizi yoyote hawezi akafika hapo mahali, atashindwa kabisa, atabaki huku chini atumane mtu. Je majibu yule mtu ambayo atakuwa amejibiwa kule, atasema vile ambayo ameambiwa ama ataongeza yake ama atapunguza? Kwa hivyo, imekuwa shida mtu ajitafutie mwenyewe kwa sababu ya hivi vifaa vya serikali. Ukiangalia vifaa vile vya siku hizi vinaona tu wale ambao wanajiweza, wale ambao hajiwezi hawawezi kuhudumiwa na vifaa hivyo. Kwa hivyo ni maoni yangu serikali ifikirie wakati inapofanya mijengo, wakati inapoweka hivi vifaa vya kisasa pia ifikirie na watu wengine pia nao hawajiwezi wanahitaji kutumia hivi vifaa kama wananchi wengine wote.

Misaada. Hii misaada inayotolewa na watu binafsi kama vile kuna wakati mwingine, nilikuwa nikienda shule, nikaambiwa Bombululu kuna zile baiskeli zinatolewa. Hii msaada haiwafiki watu wengi kabisa na ni shda imekuwa shida sana mtu apate hiyo baiskeli, hata mimi niliipata kwa bahati kwa maana kulikuwa kuna mtu ananijua pale ndio nikapata. Lakini mwengine atakaa huku msituni hajui ni wapi ataweza kujisaidia, hajui ni wapi atapata angalau baiskeli, hajui ni wapi angalao atapata chochote cha kuwa anaweza jisaidia maishani mwake. Ni maoni yangu kwamba hata serikali ingeweza kuwasaidia hawa watu, hata kama ni loan iwape kitu kidogo ili nao waweze kujisaidia wenyewe badala ya wakae wakijihurumia ama wakihurumiwa na watu wengine. Pia wapewe nafasi katika hali ya kisiasa. Watu wengine wanaambiwa basi wewe kama mlemavu utatufanyia nini? Mdomo ninao kwani kule bunge, wabunge wanasema na miguu au mikono, mimi ninaona kama ni midomo wananzungumzia kule bunge. Kwa hivyo, hata mlemavu pia ana haki ya kuingia huko bunge aseme kitu na watu pia wamsikilize badala ya kusema, aah wewe utasema nini huko. Pia tufikiwe kwa upande wa mashamba, tunaambiwa eti hatuwezi tukaridhi kwa sababu tumelemaa, hiyo ni haki na serikali itufikirie kama wakenya.

Agnes: Kwa jina ninaitwa Agnes Dama Baya, mkaaji wa Kaimbeni. Kuhusu mambo ya Katiba, sisi kama wanawake ninaona tunanyanyaswa sana, hasa kuhusu mambo ya uridhi. Ukiwa pengine umeolewa na bwana yako ama umeachwa na bwana yako, ningependelea kamam mimi mwanamke yule bwana yangu vile ameniacha, vile vitu atakavyo niachia mimi na watoto wangu, viwe ni vyangu mwenyewe, sitaki ati kutoke bwana mwengine atakaye nihudumia kwa wakati huu hanioni chochote lakini kwa wakati ule atakuwa ameondoka, ama nimekosana naye, vitu vyangu vipokonywe. Kitu kingine, sisi wanawake tunaonekana tuko nyuma sana kuhusu mambo ya haswa kinyumbani, tukiwa pengine kumetokea kazi, wanawake hawawezi kuonekana, unaenda, unaambiwa kuwa utoe mapeni ndio unaweza kuhudumiwa, bila hivyo huwezi kuonekana kama unaweza kupata kazi inayoweza kukusaidia, wanawake wanawekwa nyuma, wanaume ndio wako mbele. Sisi wanawake tunafaa haswa

wakati kama ni wa campaign kama hivi, watu wanasema vikundi vya wanawake, maanake tuko wengi, ndio tunaonekana tunaweza kusaidia watu lakini baada ya hapo hatuonekani kitu kabisa, hiyo tunataka na sisi tuangaliwe.

Kitu kingine ni kusomesha watoto wetu. Watoto wetu kama hivi mwanamke akiwa anataka kusomesha, pengine bwana yake ni mzee, yeye amesoma, amefanya kulazimishwa kuolewa na yule bwana hana elimu sana. Mtoto yule anataka amsomeshe aendelee mbele, pengine akiitisha mchango huko, anaenda kule kwa sub-chief ama kwa chief anataka mchango achangiwe, utaona ataandikiwa tu waseme, aah, tutakusaidia, mama tutafanya hiyo mpango, lakini hakuna kitu chochote kinachokuwa juu ya ule mchango, ama achangiwe mtoto aende mbele. Ingekuwa hiyo kitu ni bora kuliko mtu abaki hapo na mtoto wake, kuwe na kamati ya kuwasaidia hawa watoto kwani wote ni wetu.

Kitu kingine ni juu ya mimea yetu. Mimea yetu kama ni korosho, minazi, inaweza kutufaidisha sana haswa huku kwetu, utaona kuna maharagwe wanatoa wenyewe bei tunanunua, sisi huku kama ni ni korosho, korosho tunaokota zinataabu, unalimia, unakata, unauza halafu bei inakuja kutoka huko, mtu ananunua korosho hapa kwa bei ya chini, ikifika kule anauza pengine kila moja, anapata elfu moja. Sisi hapa ikiwa umeuza kilo tano kwa shilingi kumi na tano, utapata nini? Lakini ikiwa pengine hiyo kilo moja imekuwa shilingi mia moja ama mia mbili, unaokota korosho nyingi. Lakini mali yote inaenda huko, hatuna chochote huku kinaweza kutusaidia ni mnazi tu unakatazwa. Ni kama vile bwanako anaweza kukuruhusia ufanye kazi halafu kuna wengine mabwana zetu wengine, mtu hataki bibi yake atoke afanye biashara yeyote na ukienda jioni hatusaidiwi na chochote. Kama mimi nina tatizo la mtoto wangu, hata hivi ninaomba msaada, nikaja kwa DO wetu, nikaenda kwa sub-chief, na hivi sasa sijapata mpango wowote, mtoto hivi yuko hapo, nimempeleka mwaka jana, ninataka msaada hata hivi sasa sijapata tarehe ya kuchangiwa na ninataka nimpeleke tena second term. Sasa kitu kama kile ningependa kamati iundwe ya kutuhudumia.

Selina Kenga: Kwanza mimi nitaanza kwa upande wa haki za akina mama. Kwa kusema ukweli akina mama wanadhulumika kwa upande wa tuseme, mama amefiwa na bwanake, sasa inabidi pale awe ataridhiwa, halafu yule bwana ambaye atamridhi, atachukua ile mali yote ambayo yule ndungu yake aliacha, halafu yule mama anamfukuza, sasa inabaki ni yeye na masumbuko, lakini mali yote hana nafasi nayo hata nusu yake. Na wengine basi, utakuta hata wakina mama wengine wanakataliwa hata na watoto wao, kama tuseme umefukuzwa uwe umeenda, si mwenye atakutetea pengine ni mtoto wako, huyu mtoto wako naye anashikana na huyu baba ambaye ameridhi pale mjini, na yule mama anakuwa hana chake kabisa. Huo ni upande wa uridhi. Upande mwingine, tuseme huyu mama ameolewa halafu bwanake anapenda tena kuoja bibi mwingine, sasa vile akiwa wako na mukona vitu ambazo wamezitifuta pamoja, halafu itakuwa huyu bibi mkubwa kama mwenyewe atakavyo kuwa anajisemea, hana nafasi ya chochote pale nyumbani isipokuwa ni huyu bibi mdogo ndiye mwenye kila kitu. Hata wakati mwingine utakuta anaambiwa ondoka na vijibwa vyako uende ukae mahali pengine lakini hapa sikutaki. Sasa ndio akina mama wanauliza, je, pale na mimi ni kama tumevitafuta sisi sote vile vitu, leo hii amenifukuza mimi, na hawa watoto ambao pamoja, leo hii waitwa vijibwa, tuende pale kando, pale kando nitaenda kula nini? Basi akina mama wanasema kama ingelikuwa inawezekana, amujenge vizuri pale kando, halafu vile vitu na yeye atamhesabia nusu yake yaani wagawanye, basi aende hiyo kando na hao vijibwa vyake. Lakini huyu ambaye wamegawanywa abaki na ile nusu, na yeye bibi yake mdogo hapa anayampenda, yeye pia

achukue vijibwa vyako aende pale kando.

Pia kuna watoto ambao sisi wakina mama, kabla sijaolewa ninaweza nikapata mtoto kabla ya kuolewa, halafu hawa watoto wataendelea hivyo wadogo wadogo, lakini mwishowe tunawaita na majina ya wajomba zao. Sasa utakuta wale watoto baadaye kama wamekuwa wakubwa, unaweza ukafukuzwa na hao watoto kwa kuwa unaonekana umeongeza budge pale nyumbani. Sasa badala ya kuongeza budget pale, na pia watakuwa wanawatumia kwa sababu wamekuwa wakubwa sasa wanaweza wakafanya kazi na kila wanafanya chochote, kile wanachopenda kwa sababu ni watoto wa mjini, hata wanaweza wakawa wanatumiwa zaidi kushinda wale pale nyumbani. Lakini kukitokea kitu hivi, munaambiwa, oh nyinyi hata hamna haki hapa, nyumbani kwanza hamuwezi kusema, hamna baba yenu hapa, hamna hii hamna hii. Sasa utakuta hata haki yake pale nyumbani atakuwa hana. Kwa hivyo hapo akina mama wakasema, je hiyo nayo situangaliwe?

Upande wa elimu, tunafundisha watoto wetu kuanzia darasa la kwanza hadi la nane, tukisema kutakuwa hakuna fees kabisa, tutakuwa tunajidanganya maanake tunajua chalk nizakununuliwa, vitabu, kila kitu pale shuleni, lakini zile gharama zisiwe kubwa kufikia kiasi cha kwamba mzazi hataweza, malipo yaweko lakini yawe ya kiasi ili wazazai nao waweze kujiwekea kufikia form one awe anaweza kupeleka mtoto wake shuleni bila wasi wasi. Lakini haya maneno mengi ya hapa primary yapunguzwe kidogo, tutalipa ndio ni lazima maanake chokaa lazima mnunue. Na pia kufikia upande wa waalimu tunakuta ya kwamba waalimu tunaweza kusema tunawanunua, kusema hivyo ni kwamba, kuna yaani mfanyi kazi yeyote mpaka atapitia shule. Ukifika shule, ni mwalimu ndio yuko kule, lakini utakuta ya kwamba upande wa malipo, mwalimu yuko chini zaidi ya yule mwanafunzi wake ambaye amemfundisha. Sasa utakuta mwalimu anadharauliwa lakini basi, yeye ndiye chanzo cha mimi nipate ile kazi ambayo inanipatia pesa nyingi, kama si mwalimu, singelifika kule ambapo ninapata pesa nyingi. Sasa nitaenda upande wa ardhi. Upande wa ardhi, tunasema ya kwamba kutoka baharini mpaka maili kumi huko, kuna sehemu ya watu fulani ambao hao ndio hao, lakini basi, zile ambazo zinahitajika hasa, ni kwamba sehemu yote irudi mikononi mwa serikali na halafu basi tujue ya kwamba, kila mmoja agawanyiwe pale pale mahali alipo. Agawanyiwe hapo vizuri apatiwe hata title deed, lakini sio ati mpaka fulani, huko basi utakuja kuambiwa kesho, wewe hapa ni kwetu, hapa ni kwa babu yangu, sasa hapo unakuta kwamba huna nafasi.

Twende kwa wasiojiweza. Kuna hawa wasiojiweza masikini, wengine wanabaki tu majumbani bila msaada wowote. Tafadhali, tuwafikirie ili basi wawe na wao tunaweza kuwasaidia, kielimu na hata kimakazi pia. Tunakuta ya kwamba ofisi zetu ni zile kazi za mpaka sijui unapanda ngazi, sasa akiwa hajijwezi, kupanda pale, aje kwako ofisini, aje aombe kazi itakuwa vigumu, atakuwa hataweza. Je, kama zingelikuwa flat tu hivi, na yeye akiingia pale awe atafikiriwa, hata kama atakuwa ni mtu wa kufagia fagia pale, zile za rahisi, ili na yeye awe anajisikia kwamba na mimi ninafikiriwa au ninajaliwa. Kufikia hapo, tunarudi upande wa biashara. Unakuta ya kwamba tunafinywa sana na hizi licence, na hiki kitu cha licence, tuseme ya kwamba ninalipa licence, sikatai lakini tuangalie ile biashara ambayo nitailipia licence inaniruhusu? Je kama ni mahali tu nimeweka hii kiosk ya vitu vidogo vidogo mwenyewe nipate mkate wangu na wanangu. Leo hii mtu anakuja anaitisha licence, niwe nitalipa hizo pesa, halafu pengine kesho, kesho kutwa nishindwe pale, tuseme baada ya siku mbili, tatu, jana nililipa licence ile, leo hii nimeshindwa,

ninaondoka mimi sasa biashara yangu imefail, hiyo nayo iwe itafikiriwe. Yangu ni hayo, asanteni.

Florena Mseri: Asante sana mwenyekiti na wanatume, nitazungumza machache kwanza juu ya walemavu. Ninapendekeza katika Katiba ijayo kuweko sheria kwamba mtoto atakapo zaliwa mlemavu aandikishwe kwa chief, halafu baadaye wapangiwe siku za kwenda clinic, ambapo madaktari watawahudumia na waendeleo kufanya hivyo mpaka mtoto atakapo endelea kufika shule na mpaka atakapokua mtu mzima aweze kujitegemea mwenyewe akipata msaada wa serikali. Pili, ninazungumzia juu ya watoto ambao wazazi wao wametengana, wamepeana talaka. Tunaona kuwa kina mama ndio hasa kwa mwaumbile walezi wa watoto. Tunaona ni sawa kikatiba, hawa watoto wabaki kwa mama, lakini mara nyingi zile mila zetu na tamaduni zetu ambazo zinakandamiza akina mama, zinatumiwa kudhulumu kina mama na watoto wanabaki kwa baba. Tunataka kwamba wakati huu katiba iamwe kwamba watoto wabaki kwa mama, hasa wale ambao wako chini ya miaka kumi na minane.

Tena watu wanapotalakiana, tunaona ya kwamba katika makabila mengine, hao akina mama wanalazimishwa kuregesha mahari. Lakini tuelewe kwamba, wakati ule mama amekaa pale, amefanya kazi, na hata ukimhesabia shilingi kumi kila siku, yeye atakuwa ile mahari asharegesha, kwa hivyo wasiregeshe mahari lakini iwe kwamba wale watoto ni wao wote, watawalea na kuwahudumia kulingana na uwezo wao. Halafu, ninazungumza juu ya ndoa za kienyeji. Tunapenda katika hii Katiba ijayo hawa watu wanaoona kitamaduni waweze kupewa vyetu vya ndoa kwa chief, kwa sababu imekuwa kwamba mara nyingine wanaposhtakiana ikiwa wameolewa wake wawili au watatu, yule mwenye cheti cha ndoa cha kutoka kwa kanisa au kwa kadhi ama kwa serikali, anapendelewa zaidi kuliko yule ambaye ametolewa mahari.

Mambo ya uridhi yashatajwa tayari na ninaunga mkono kwamba ardhi tuliitetea wakati wa uhuru ni ardhi yetu, ni ya waafrika walio katika nchi ya Kenya, sio ya watu waliotoka nje waridhi na waichukue halafu wauzie wale wenyeji, wawe kwamba wenyeji ndio wanakuwa squatters katika mashamba ya wageni. Halafu ninazungumzia juu ya bunge. Mimi ningependelea bunge ziwe mbili, hawa wabunge tunawachagua wanaotuwakilisha wawe katika chumba chao na serikali iwe katika chumba chao. Kwa sababu hivi sasa wako pamoja, na haiwezekani kwamba mtu anaweza kujikosoa mwenyewe, hasa wakati wanajadili mambo ya matumizi ya pesa zimetumika vibaya haiwezekani mtu kujikisoka mwenyewe, atakuwa ni mbunge tena kwa sababu upande mwingine ni waziri. Tungependa pia bunge hili lijipangie ratiba yake yenyewe isiwe kwamba inaambiwa na rais yeye huu ndio wakati wa kuanza na kufanga bunge. Tena tungependa bunge lipewe uwezo zaidi maana hivi sasa rais amepokonya bunge mamlaka na limekuwa haliwezi kusema vile linataka, linasema vile rais anavyopenda yeye mwenyewe. Kwa hivyo, lidhibitishe ama likubali wale wafanyi kazi walioajiriwa na Tume ya umma, wawe wafanyi kazi na kama watafutwa basi bunge likubali kuwa wamefanya makosa fulani. Pia tunataka hawa wabunge, waweze kuregeshwa nyumbani ikiwa wamefanya makosa, hii iwe kwamba wanaweza kukusanya robo ya wale wapigaji kura, waandikishe majina yao, watie sign, na pia watoe namba za vitambulisho vyao vya kupigia kura na vile vya taifa. Ikiwa robo ya hawa watu wanasema yeye hafai, basi yeye kurejeshwa nyumbani aachishwe kazi, na uchaguzi mdogo ufanywe, tumpatie mtu mwingine. Pia hawa wabunge wawe na elimu ya kufika kama form four, na wawe wamepita kingereza na Kiswahili na wamepata C ama zaidi.

Mwisho ninazungumza juu ya Tume ya uchaguzi. Hii Tume ya uchaguzi, mwenyekiti wake achaguliwe na bunge na yale mamlaka walio nayo tena waongezewe yale mengine, kwa mfano, wao ndio wataamua ile mipaka ya wakilishaji bungeni, igawanywe kulingana na wingi wa watu. Kuna waakilishaji bungeni wengine ambao wana watu wachache na wengine wana watu wengi kwa hivyo ifanywe sawa sawa. Sasa lingene ni kwamba wao watoe security wakati wa uchaguzi, sio serikali, itolewe na Tume ya uchaguzi, pia isimamie matangazo ya kisiasa wakati wa campaign. Tena itoe vyeti vya mikutano ya kisiasa, vyeti vya kitaifa namna hio na ipewe pesa, itengewe pesa ambazo zitaiwezesha hiyo Tume kufanya kazi kwa uhuru bila kutegemea serikali.

Juu ya uridhi, hasa upande wa wanawake. Mila zetu zinabagua sana wanawake, kwa hivyo, tunaomba katika Tume hii wanawake pia waruhusiwe kuridhi, akiwa ni msichana ardhi mali ya babake. Ikiwa ni mwanamke aliyoolewa basi mume wake anapokufa ile mali anairidhi yeye pamoja na watoto wake. Na isiwe kwamba mtoto wa kike ataridhi sawa sawa na mvulana, hiyo sehemu itakuwa ndogo, kwa sababu yeye akiolewa atapata sehemu ile nyingine ya bwana, mtoto mvulana atabaki pale pale na hatapata uridhi mwingine kutoka kwa mtu mwingine. Mwisho ningependa kusema juu ya waastafu. Hawa watu wanaostaafu kutoka kazi, watu wengine, wafanyi kazi katika maofisi ya serikali wanayazuia malipo yao. Ni vizuri hawa watu watakapopatikana wapate adhabu ya kuchelewesha, kutumia au kuzuia kufikisha haraka. Asanteni.

Com. Abida Ali: Haya tumpate pendo, hayuko, tumpate Christine Nseka.

Christine Nseka: Jina langu ni Christine Nseka. Oni langu ni kwamba walimu wa Nursery washuhulikiwe kama wale waalimu wengine katika mishahara yao. Utakuta muna shuhuli ngumu kuangalia watoto lakini utakuta munalipwa na wazazi na lakini wazazi wengine hawalipi. Sasa unakuta unakaa pale kwa muda mrefu pesa ni kidogo, huku unaenda shamba ama kufanya shughuli ingine, kila siku uko pale mpaka saa sita, lakini unakuta hatuna manufaa yeyote. Lingine, unaweza kuwa katika ule urithi, nyumbani kwenu uko na mandungu, na iwe wewe umenunua kitu pale nyumbani lakini unapoolewa utakuta kile kitu kitamilikiwa na wale ndungu zako. Wewe hutaesabiwa chochote na kile kitu ulinunua na pesa zako mwenyewe.

Lingine utaona wanaume huwa wanapenda sana kuwapa zile mali, hasa wagiriama, kwa mabibi zao, sasa ndio nilikuwa ninauliza kwa nini wao wanaenda nje sana na mabibi za watu, na wale mabibi zao hawawezi kuwapa zile pesa wakapewa wao watumie. Utakuta wale ndio wanapewa zile pesa zote wazitumie. Ni hayo tu.

Dama Ngombo: Nina shida. Bwanangu hayuko, lakini mimi ndio nimekuja, shamba langu limechukuliwa, la limwa na mtu na iko marafa hiyo shamba. Kwa hivyo nilikuwa ninataka maoni kwa sababu mimi sina shamba la kulima.

Com. Abida Ali: Enda kwa DO pengine utapata msaada.

Com. Riunga: Sidi Kesi, Gladys Yaa

Gladys Yaa: Mimi ningependa, kwa mfano, chief ambaye yeyote ataka kuchaguliwa tumchague kwa mlolongo, maanake utakuta machief wengine wanachaguliwa halafu ukienda una kesi yako unaambiwa mpaka utoe kitu. Kwa mfano, mimi sina kitu, inaonekana wazi ya kwamba kesi yangu haitaweza kusikizwa. Kwa hivyo, tunasema chief yeyote tukimchagua, tumchague kwa mlolongo. Ingingine ni ya kwamba utakuta sisi wanawake, mara nyingine tunadhulumiwa sana. Kwa mfano vile umeolewa na bwana yako, halafu unakuta anakufukuza, ikiwa wewe umekaa kwake kwa muda mrefu, anakufukuza pamoja na watoto. Sasa pale ninapendekeza ya kwamba ikiwa pengine amenifukuza na watoto wangu ikifika kule, awalee watoto wangu mpaka pale watakapofika umri wakuwa wao wenyewe wanaweza kujitafutia.

Lingine ni kwamba ningependa sisi wanawake katika upande huu wa kazi, utakuta mahali panapofanyiwa kazi ni wanaume pekee ndio wanachaguliwa kwa namba kubwa, lakini utakuta sisi wanawake mara nyingine hata kama hiyo kazi unajua, huwezi kuchaguliwa kwa sababu wewe huna haki. Kwa hivyo ningependa wanawake wawe na haki ya kuwa wanaweza wakaajiriwa sawa na waume. Kuwe na ile nafasi ya kuwa mtu anaweza kujiandikisha. Ni hayo tu.

Abida Ali: Megi Jungo: Anza na jina na uongee kwa sauti

Megi Jungo: Mimi nina mambo kidogo ambayo ningependa katika marekebisho ya Katiba yatekelezwe. Kitu cha kwanza ningependa wanawake wapewe nafasi katika uongozi, nafasi nyingi zaidi katika uongozi. Zile ambazo wanapewa kwa sasa tuneona kwamba hazitoshi, sehemu kama pengine ma DC, PC, makatibu na kadhalika, viongezwe kwa akina mama. Pia ningependa kutolewa pengine sheria fulani ambayo katika bunge kina mama pia wapewe nafasi za kutosha kwa sababu kulingana na mashindano ambayo yako, tunaona ya kwamba kina mama huwa hawapati nafasi nyingi hata pengine wakisisimama katika uchaguzi, tena utakuta kwamba wanashindwa na wanaume. Kwa hivyo kuwe kuna kiwango fulani hivi cha seats ambazo zitakuwa zimekuwa preserved kwa akina mama bungeni na hata pia kwa local authorities tuwe na seats tano ambazo councilors watakuwa wamepatia akina mama.

Kwa upande wa local resources, ningependelea ya kwamba kuwe na kama asilimia hamsini hivi ya zile pesa ambazo zinapatikana katika kitu kama tourism, airport, sea port, na kadhalika, iwe pesa hizo zitatengewa maendeleo katika sehemu zile ambazo resources hizo ziko. Tuseme kama pwani hivi, tupate pesa ambazo zitatoka katika utalii ama katika port, asilimia hamsini iwe itaregeshwa katika area ya coast ili ifanye development katika sehemu hiyo.

Upande wa serikali, mimi ninaunga mkono ile central government iendelee, iwe maintained lakini provincial officers kama PCs waondolewe, tuwe tutawapata governors katika hizo sehemu, na hawa governors wawe watakuwa elected na watu wenyewe wanainchi. Jambo lingine ni kwamba, naomba mkono ile term ya five years kwa president na pia katika kwa wabunge, lakini ningekuwa na mapendekezo haya. Kwa sasa kama president inasemekana kwamba ni atawale kwa kipindi cha miaka kumi mfululizo, mitano halafu baadaye mitano, mapendekezo yangu ni kwamba hata MPs vile vile iwe namna hiyo. MP asibaki kwa

kipindi kirefu zaidi, kuna MPs ambao wame-serve kwa miaka hata ishirini ama zaidi na si kwamba ni wazuri sana lakini ni kwa sababu wana nafasi yakufanya mambo fulani fulani kama rigging na mengine kwa sababu wana pesa na wamekaa kule kwa muda mrefu wana njia za ku-manipulate hizo elections na warudi. Kwa hivyo ningependa kwamba kama president amewekewa two terms, MPs nao hivyo hivyo, wawe na two consecutive terms hata akiwa ni mzuri namna gani, atoke mwengine angie.

Jambo jingine ambalo nilikuwa ninapendekeza ni level of education ya councilors. Councilors tunapenda at least wawe na form four level of education, kwa sababu kuna mambo mengi ambayo huwa yanataka yatekelezwe na mambo ambayo ni wasome waelewe ndio watekeleze. Wengi wao tukiangalia sana ni class seven, standard eight drop out, kwa hivyo hawatuhudumii kisawa, tunataka at least level ya chini kabisa iwe ni form four ndio ninafikiri watahudumia wananchi vizuri.

Kuna mambo kama ID, mabadiliko ya particulars katika ID. Jambo hili limesumbua sana haswa upande wa mashambani, kwa sababu utakuta kwamba kama mama ameolewa na anataka kugeuza majina katika ID. Kuna mambo mengi sana ambayo huwa yanatakikana ambayo wakati mwingi sana yanamtatiza mpaka mama yule anabaki vile vile akiwa na jina lake lile la maiden na jambo hili baadaye linakuja linasumbua kwa sababu wakati wa urithi, pengine mume wake amefariki, sasa utakuta kwamba akiambiwa apeleke zile particulars pengine ndungu za bwana watapeleka kuonyesha kwamba ni ndungu yao. Yeye akipeleka kitambulisho na nini bado kinasema kwamba hakuna jina la mumewe pale, kwa hivyo inaonekana hakuna ushaidi wa kutosha kwamba yule alikuwa ni bibi ya mtu. Sasa tukichukulia kwamba kuwa ameolewa na sheria za kimila, customary law, kwa hivyo inakuwa vigumu sana kwa yule mama kupata haki yake kwa sababu kuna mambo kama hayo hayakutekelezeka.

Jambo jingine ni kuhusu uridhi kwa watoto na mali wakati mama na baba wamekosana. Utakuta kwamba katika divorce wakina mama hawapewi haki kwa sababu katika mila ya watu wa pwani hasa utakuta kwamba baada ya mama na baba kukosana, wale watoto kimila ni wawe na baba. Sasa tunataka at least kuwe na sheria ambayo itaondoa jambo hilo, utakuta hata watoto wadogo kabisa ambao hata wako under age, kama pengine miaka mitano, wanakuja wanabebwa kwa lazima wanaenda kwa baba kwa sababu anaambiwa kwamba mila inasema mtoto akae na baba yake. Kwa hivyo, tungependelea angalau kuwe na sheria fulani ambayo itafanya watoto wawe na mama, ama wachague wenyewe kama wamefika umri wa kuchagua, ili mpaka wakifika akiwa adult anaweza kuchagua yeye mwenyewe pahali atakaa kuliko kulazimisha hii hali ya kwamba watoto wote wawe na mzazi wa kiume bila mama yao, ninafikiri inatesa sana watoto hiyo. Pia vile vile katika hiyo mila kuna huu ulipaji wa mahari, kuna mila ambayo inasema kwamba mama akiolewa, ile mahari kama amekosana na mume wake basi ile mahari niaregeshe na watoto hapati, angalau kwamba kungekuwa na sheria ya kwamba mahari imetolewa ile huwa ni kama zawadi tu kwa wazazi wa msichana. Lakini sasa ikiwa imekuwa kama ambaye ni uchumi wa kwamba baadaye iregeshwe, ninafikiri inakuwa si vizuri. Kwa hivyo kama watu wamekosana na wameachana, ibaki hivyo hivyo tu, ibaki kama zawadi lakini isiwe kama ni malipo ambayo kwamba ni alipe.

Kuhusu majimbo, wanasema kwamba majimbo yaweko, lakini hata hivyo wale wafanyi kazi ambao watakuwa wameajiriwa

kwa sababu kuna wengi sana huwa wana complain wanasema kwamba, kukiwa na majimbo hata wafanyi kazi pia tunataka watoke katika sehemu hiyo hiyo. Kwa hivyo maoni ni kwamba, hatusemi kwamba majimbo yakiwako watu wafukuzwe waende kabisa wafanyi kazi pia waende ati tubaki na watu wa pwani peke yao ama watu wa sehemu hiyo wafanye hizo kazi. Kama kuna kazi fulani ambazo zinahitaji professions fulani wawe watafanya, basi wabaki wataajiriwa waendeleo kufanya kazi katika hayo majimbo. Lakini sana rasilimali ya hilo jimbo ndio itumike katika ku-develop zile sehemu hizo. Mambo ya mashamba, tunaona kwamba hili tatizo lingeishia katika district level, kama kuna matatizo yote ya mashamba yawe solved mwisho katika district level siyo kwamba mpaka Nairobi huko ambako ni mbali, wengi hawawezi kuenda huko na kupeleka malalamishi yao ama kesi zao. Kwa hivyo, iishie katika district. Hayo ndio yalikuwa maoni yangu kuhusu marekebisho.

Naomi: Majina yangu ni Naomi Kariuki, ninafanya kazi na watoto. Tulipokutana kama maidara ya watoto, wale watu wanaofanya na watoto tuliomba the revised Constitution iwe inaweza kutambua mtoto, kwa hivyo tukasema at least the principle ya kwanza iwe ni distinct recognition of children in a special section. We came up with twelve principles and I'm just going to talk of a few and then I can give up the memorandum.

Principle number one should be distinct recognition of children in a special section under the bill of rights. There should a definition of a child whereby, for the purpose of legal interpretation and connected with tender, a child should be any person below the age of 18 and this definition should be considered to mean every boy or a girl and children with disabilities. All children have a right to nationality and citizen right and every Kenyan child has automatic citizenship. Right to education, every child should be entitled to free and compulsory basic education and affordable subsequent education, both which should be the state responsibility to guarantee. Children should be protected from abuses and exploitive measures. Na hapo tukaangalia abuse and neglect, discrimination through certain cultural practices have also had a negative influence on the life and welfare of children. Kwa hivyo constitution iangalie namna hiyo. And the best interest principle is, everything that has to be done about a child must always be guided by the child's needs. Tukaangalia access to justice by children. The reviewed constitution should provide that no civil criminal proceedings in a court of law concerning a child should proceed in the absence of a legal practitioner for the child.

And finally I'll talk about the governance. Revolution of power in governance and budgeting should be addressed in the reviewed constitution to facilitate protection of children upto the grassroot level. Yangu ni hayo, yale mengine yako kwa memorandum.

Abida Ali: Rehema Ali Mzee, Nuru Bakari.

Nuru: Jina langu mimi naitwa Nuru Bakari. Mazungumzo yangu mimi ninaongea kuhusu mimi ni Kanu, lakini kulingana na yale mambo ambayo yaani huwa yananihuzunisha ni kama vile mtu ametoka sehemu za mbali pengine kule ametoka na matatizo, amekuja mahali kama hapa naishi baadaye nao wanapata wageni wanakuja hapo. Sasa katika muda ule wa kuishi, baadaye

kutokee matatizo kitu kama vile Tana River. Sasa wakati yale matatizo yakitokea halafu serikali inasema huyo mtu kwa vile ameishi miaka mitano au kumi yeye ni mwenyeji wa hapa hana ruhusa ya kuondoka sasa ni watu wake tu waumizane na kuuwana ambako hakuna idadi na ukiangalia hata saa hii kuna watu wengine ambao wametoka huko wanauliwa. Kati ya watu kama hao ikiwa wanaendelea kufa wale ambao sasa ni viongozi, yale maneno wanaenda kusambaza wakapeleka mbele, hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kuzungumzwa ndani ya redio hata wakati ukija hayo maneno yakijulikana ni baada ya wiki mbili tatu na watu wanaendelea kuumizana. Sasa mimi napendekeza, mtu yule kama vile mimi nimetoka huko nyumbani nimekuja hapa ninaishi kwa muda, kama vile nimeishi na sasa nimeonekana tabia zangu ni mbaya afadhali ni bora nirudishwe kule kule ambapo nimetoka. Maanake sasa wananchi wa hapa wenyewe mimi wamenikaribisha nimeishi kwa muda na leo vitendo vyangu vimekuwa si vizuri, nina haki mimi kuambiwa nirudi pale kwetu ambako nimetoka. Haina maana ya kukaa hapa na kuwatatiza wananchi ambapo mimi ni mgeni.

Kitu kingine ni kama vile hawa ndungu zetu ambao tunaishi nao hapa, hawa wagiriama, mtu anaweza kuoia mwanamke akaishi naye kwa muda mrefu sana na akazaa naye watoto. Badala kuwa amezaa naye sasa ameshachoka na yeye anamfukuza, anamwambia nenda kwenyu na madhala kuwa ameenda kwao yeye wale watoto anawaacha hapo tena anadai mahari yake apewe. Kwa hivyo, ninaona hilo jambo pia mungeliangalia ili kuhusulia hilo jambo la wagiriama. Na lingine ni hilo la huko ambalo mtu amekuja na ni mgeni na anasumbua na hawezi kuchukuliwa hatua yoyote kwa kuwa huyo mtu amekaa hapo kama miaka mitano kama ni miaka kumi, sasa wanaumiza mtu na serikali haichukui hatua yeyote pengine mtu anajua hakika mahali kama hapa na mamburui, kuna vita. Mtu haendi kwa vile yule anayekuja pale si kabila yake na hamhusu sasa yeye ananyamazia tu hapo, juu wale watu wa ngazi ya juu hawawezi wakajua kama kunaendelea nini unaona wananyamazia nayo hapa hata akija akitoka nje huwa watu wamekufa wengi sana. Kwa hivyo ninapendelea majimbo maanake si majimbo yaani ya kufukuza watu, la, si majimbo ya ati mtu ni mgeni aondolewe, hiyo siyo.

Mimi ninataka majimbo ile ambayo watu wanaweza kuitengemea maanake ninajua kwa hakika huyu ni mtoto wangu, huyu ni ndugu yangu na hapendelei yule kuumizwa ni lazima yeye atakuwa anaona uchungu ikiwa jamii yake wanakufa. Lakini ikiwa mtu umetoka pengine Kisumu, amekuja hapa anaishi baadaye hata ukiona mtu pale amekufa na yeye pengine ni polisi, kama ni askari, hawezi kuwa na uchungu maanake anajua yule amekufa si jamii yake. Lakini ikiwa ni jamii yake, hawezi kupendelea ule mtu wake afe, lazima kile ambacho kinahusika atazungumza ule ukweli maana vile ambavyo vinaendelea sivyo vinavyozungumzwa. Inaweza kuwa vita vimondoka kivingine halafu utasikia ndani ya maredio yanazungumza nyingine, unaona kwa vile pengine kiongozi ni kabila nyingine ameshakwenda kupewa hongo sasa anabadilisha yale maneno ili nyinyi mzidi kuumia. Kwa hivyo, ninaona hayo ndiyo yangu ambayo yalikuwa yamenigusa. Asante sana.

Com. Abida Ali: Margaret Peter, Nancy Joseph, Kauchi Mary, Taabu Mueni, Agnes Kadzo, Sophia Omar, Esther Harufa.

Esther Harufa. Maoni yangu ni juu ya shamba. Shamba yangu nimepokonywa na nimetoa pesa ili shamba yangu irudi na sipati shamba yangu mwaka huu ni wa tano sasa. Mimi sina mtu wa kunichumia ile shamba ndio baba, ndio mama, ndio bwana

yangu. Sasa ndiyo shida yangu iliyonileta hapa nije nilie kwa serikali waniangalilie.

Com. Riunga: Nani amechukua shamba?

Harufa: Ni chifu Taraka.

Com. Riunga: Ulikwenda kwa DO?

Harufa: Sijui DO mimi.

Com. Riunga: Kingi, where is the DO's office?

Kingi: The DO's office is down there.

Com. Riunga: Muone yule, halafu umuambie. Utaenda umuone yule bwana ofisini mwake. Sheila Kahindi. Wale akina mama kama kuna wangetaka kuzungumza waziwazi hata wanakaribishwa. Ninafikiri bwana Luganje ndio alikuwa wa mwisho, sasa tuko na Joseph Kazungu. Karibu bwana. Sasa munaweza kukaribia ili mukiitwa munaweza kuja haraka.

Joseph Kazungu: Asante sana kwa kunipa nafasi hii na jina langu naitwa Joseph Kazungu Kaingu na nina maoni mawili ambayo yanahusiana na haki za binadamu. Tunaona haki za binadamu wakati mwingi zinatajwa. Lakini kwa upande mwingine tunaona kwamba hazitekelezwi na nikisema haraka haraka ni kwamba, kuhusu hapo chini vile hali inavyoendelea pale tunajua kabisa kwamba watu wanachukuliwa kama wengine si watu na wengine ni watu. Kwa mfano, mkenya akipatwa na hasara pale chini basi ile transport, nikisema hivi ninajua wengine wataniunga mkono, kwa sababu anachukuliwa anaingizwa kwa tractor ambayo haina trailer na anapelekwa kwa usaidizi huko. Lakini mwengine kama ni muhindi kama ni wale wenyewe pale anachukuliwa kwa hali nzuri, na hii hali za kusema kuna haki ya binadamu haiangaliwi sana, zinatajwa tu lakini hazitekelezwi. Na hata wale wanapatwa na hasara hizo, akienda mahali popote, akienda kutaja jambo kama hivi, hatiliwi maanani, anaonekana kwamba ni mtu ambaye anaharibu au ni kama mtu ambaye anachokesha akili. Kwa hivyo, mimi kwa mawazo yangu ninataka sana hayo yatiliwe maanani, kama ni haki iwe kwa kila mmoja sio wengine wachukuliwe ati wana haki na wengine hawana.

Maoni mengine ya pili ni kuhusu ya wale ambao hawajiwezi. Tunaona mtu asiyejiweza, sio kwamba amezaliwa vile akipenda awe hivyo. Lakini utakuta kwamba hawatiliwi maanani sana, maana utaona kama n'gombe wako maofisa wanaohusiana na mambo ya n'gombe, kama ni ugonjwa wa n'gombe, anaenda kutibiwa na kufanyiwa mambo yoyote ambayo yanaweza kumsaidia. Lakini yule asiyejiweza, hata hawezi kuwekwa maanani sana, na hawa wasiojiweza ni mizigo sana kwa wale ambao wanawachukulia. Mtu kama akiwa ni kipofu, huyu akiwa ni kipofu ni kama wewe nawe ni kipofu, na zile shughuli zote za yule

kipofu au yule asiyejiweza ni wewe ndiye unatakikana uzishughulie au umsaidie nazo. Lakini kwa upande mwingine, Katiba haiwezi kumchukulia huyu kama ni mwanadamu, ni kutaja tu kama kuna misaada fulani inakuja na hata ikija itawafikiria pengine wale waliokaribu lakini wale wengine ambao wako mbali na hawa wanaohusika hawawezi kutiliwa maanani. Kwa hivyo, utakuta kwamba mzigo wa wale wasiojiweza unakuwa mzigo kwa mtu binafsi, sio kwa serikali au kwa mtu ambaye anahusika. Kwa hivyo mimi ninaonelea kwamba wale nao wahesabiwe kama watu, kama ni kuwekewa viwango fulani kwa wale ambao hawajiwezi, waweze kupatiwa nao, maana utakuta kama ofisa aliye-retire kuna kiwango fulani ambacho anapewa kila mwezi na huyo kipofu au yule ambaye hajiwezi hana chochote ambacho anaweza kujisaidia nacho na serikali iko, inaangalia tu inajua, lakini wale hawatiliwi maanani. Kwa hivyo, mimi kwa mawazo yangu ni kwamba wale watu nao ni watu, maana wao ni watu ambao wamezaliwa na wanamahitaji, ikiwa ni kuvaa, kama ni kula, kama ni jambo lolote lile ambalo yule anayejiweza anataka apate na yeye naye anahitaji pia apate. Kwa hivyo, naomba kwamba katika kipengele hiki cha Katiba wale nao wahesabiwe kama ni watu, wapatiwe misaada kama wengine. Yangu ni hayo tu.

Com. Riunga: Asante sana bwana Kazungu, sasa ni bwana Kasim.

Kasim: Commissioners wetu, bwana DO, nashukuru kwa nafasi hii na maoni yangu ni kama inavyofuata. Jambo la kwanza nitazungumza juu ya land and property rights, haki za umilikaji wa ardhi nchini Kenya. Kwa hivyo, kulingana na Katiba iliyoko ni Katiba ambayo imetugandamiza sana sisi wananchi kwa upande wa ardhi. Kwa mfano, kifungu cha kwamba uwezo aliopewa Commissioner wa kutoa ardhi mahali popote au ardhi ambayo mwanainchi ameiliki kisawasawa na mwananchi ameimarisha. Kwa hivyo, ardhi hiyo inachukuliwa na yule ambaye ameimarisha na anapewa mtu ambaye yeye hakuimarisha. Kwa hivyo, uwezo huu ambao amepewa Commissioner Kulingana na maswala ya ardhi, ninaomba katika urekebishaji wa Katiba, kifungu hiki kiangaliwe sana. Kwa mfano, hapa kwetu katika eneo la Magharini, sehemu ya Ngomeni, kuanzia Mjana Heri mpaka kufika Rassim Mawinde, utaona acre elfu saba ambazo ndani yake kuna wananchi karibu elfu kumi na tano, kuna mashule, misikiti, makanisa na miradi mbali mbali. Lakini kwa sababu kifungu cha sheria kinasema yeyote aliyepewa title deed au aliyepewa karatasi yaani allotment letter, ndiye mwenye haki ya ardhi hiyo. Kwa hivyo utaona hivi sasa hawa wananchi elfu kumi na tano wanahangaishwa kwa sababu wao hawakupewa haki za kumiliki ardhi, wamepewa watu ambao hata sasa hawajulikani. Kwa hivyo jambo la kwanza ni kifungu hicho kiwe kitarekebishwa.

Commissioner asiwe na mamlaka zaidi ya kutoa uwezo juu ya ardhi. Na urekebishaji huku kulingana na maoni yangu, ninaona local communities, committee ambazo zinachaguliwa na wananchi ndizo ambazo zipewe mamlaka na ziidhinishwe juu ya utoaji wa ardhi. Kwa hivyo, vile vile, kila district kuwe kuna headquarter ambayo wananchi wanaweza kupewa title deed, sio kwamba mtu akitaka title deed, mtu asafiri kutoka hapa mpaka Nairobi. Kuna wengine Nairobi hatujui, pengine mtu anaenda na fare na baada ya kwenda na fare, huna pesa za chakula. Kwa hivyo jambo hilo liwe litaondoshwa kabisa katika Katiba, iwe mwananchi wa hapa akitaka title deed akienda Malindi wa siku mbili, tatu, tayari ameshaipata hiyo title deed.

Jambo lingine ambalo ningelipenda nizungumze ni kuhusu absent landlords. Kuna ardhi ambazo zimemilikiwa na watu fulani.

Ardhi hizo wenyewe hawaonekani wala hawapo. Wanainchi wameishi katika ardhi hizo tangu jadi, lakini kila wakienda kutafuta title deed, wanaambiwa kwamba ardhi hizo zinawenyewe na hao wenyewe hawaonekani. Kwa hivyo, hizo ziwe title deed hizo ziwe zitafutuliwa mbali na wale wananchi ambao wako katika maeneo hayo ndio waidhinishwe na wapewe title deed.

Jambo lingine nitaongea ni kuhusu value – malipo juu ya ardhi. Malipo ambayo tunapewa ni malipo ambayo ni ya juu sana. Kwa hivyo mwananchi ambaye maisha yake ni maisha ya chini yeye hajiwezi, kwa hivyo mwananchi huyu anataka title deed, akienda anaambiwa, kwa mfano, nusu acre anaambiwa tupatie laki mbili ndio tukupatie hii nusu acre. Kwa hivyo, hiyo huwa ni kizuizi ambacho kimemfanya huyu mwananchi asiwe na uwezo wa kupata title deed. Kwa hivyo, malipo ambayo yako yaondoshwe au yarekebishwe kwa kiwango ambacho ni cha chini na kinaweza kunufaisha mwananchi ambaye hali yake ni ya chini. Haya ni kwa upande wa ardhi.

Ninaingia upande wa Judiciary, mambo ya mahakama. Katika mahakama kuna koti ambazo zimegawanywa section mbali mbali, kwa hivyo mimi nitazungumza kuhusu haki ya koti ya Kadhi kwa sababu sheria ya koti ya Kadhi ni sheria ambayo imepangwa na Mwenyezi Mungu kuna sheria ambazo tunazipanga sisi za kikatiba ambazo ni sheria zetu wanainchi. Kwa hivyo Kadhi's court ni sheria iliyopangwa na Mwenyezi Mungu na ina haki iheshimiwe zaidi. Ikiwa Chief Justice katika nchi ya Kenya ana mshahara kiasi fulani na Kadhi au chief Kadhi apewe kiwango sawa sawa cha mshahara kama kile ambacho anapata Chief Justice. Hii ni haki ya kwanza ambayo tunaipigania katika koti yetu ya Kadhi. Haki nyingine ni haki ya usafiri. Utaona kwa mfano, ukienda kwenye koti nyingine utaona magistrate yuko na gari hapo, lakini Kadhi katika kiislamu au ambaye yuko katika mahakama, hapewi huduma kama zile wanapewa majaji wengine.

Jambo lingine ni kuhusu clerks na servants ambao wanaandikwa kuhudumikia Kadhi's court. Kwa mfano, utaona katika koti ya Malindi, ukienda Kadhi ni muislamu, kwa hivyo kuna matatizo ambayo kabla hajaingia kwa Kadhi yanatakikina yasuluhishwe na wale ma-clerks. Kwa hivyo, utaona hakuna clerk hata mmoja ambaye ni muislamu. Pale tunaomba sisi katika marekebisho ya Katiba, kila Kadhi ambaye yuko aekewe ma-clerks ambao ni waislamu kwa hivyo kabla mtu haja-file case, wawe wale clerks wataweza kumsikiza yale malalamishi yake wakiweza kuyasuluhisha wayasuluhishe na ikiwa hawayawezi ndio yafailiwe katika koti ya Kadhi. Jambo lingine utaona mtu amehukumiwa, mfano, katika sheria za Kadhi, katika mambo ya kuridhisha waislamu. Mwanamke ana fungu lake la kuridhi na mwanaume vile vile anafungu lake. Kwa hivyo, utaona saa ingine watu wanahukumiwa katika Kadhi's court mara utaona faili imeitishwa, imeingia katika Court of Appeal, inahukumiwa na mtu ambaye yeye hata hajui ile sheria ya kiislamu imezungumza kinamna gani. Kwa hivyo, tunaomba kufanywe marekebisho iwe kutapatikana ikiwa mtu amehukumiwa na Kadhi hakutosheka, akienda kwa Chief Kadhi iwe ni mwisho, hakuna Court of Appeal na ikiwa iko Court of Appeal irudi hapo hapo mikononi mwa waislamu.

Jambo lingine tunaomba kwamba, katika marekebisho ya Katiba kupatikane Kadhi katika kila district, sio leo Malindi kuna Kadhi, Tana River hakuna Kadhi, Kilifi hakuna Kadhi. Hii inasababisha kupatikana kwa msongamano mwingi katika makoti ya

kiislamu. Jambo lingine katika Judiciary, nitazungumza kuhusu vifungu fulani vya Katiba. Kuna mambo ambayo kwa mfano, kina mama wamelalamika mara nyingi, mambo ya kunajisi au sodomising. Utaona kuna visa vya kunajisi ambavyo vimezidi au sodomising – kulawiti watoto wa kivulana. Visa kama hivi vimezidi lakini wale ambao wametendewa haki kama hizi au makosa kama haya ni watu ambao ni masikini hawajiwezi. Kwa ajili hawajiwezi mara nyingi wanagandamizwa na makoti. Kwa hivyo, tunaomba kupatikane marekebisho ambayo wale wanyonge vile vile wataweza kutiliwa maanani maswala yao.

Jambo lingine ambalo ni la tatu. Kifungu nitakachozungumzia ni kuhusu utawala wa serikali. Kwa hivyo, kama tulivyosikia maoni ya wenzetu wengi, na mimi maoni yangu ni hapo hapo ninayaunga, yaani ni utawala wa federation regionalism, yaani kupatikane utawala wa majimbo. Kwa hivyo, majimbo ndio sababu ya kuondosha corruption, ndio sababu ya kuondosha ufisadi. Utaona kuna kelele nyingi zinapigwa, Tume mbali mbali zinachaguliwa kurekebisha mambo ya ufisadi lakini hizo Tume ambazo zikichaguliwa nazo pia huenda mahali fulani zikateleza, zikabidi ziingie katika mambo kama hayo. Kwa hivyo, suluhisho kubwa la kuondosha ufisadi nchini Kenya ni kupatikane utawala wa majimbo na utawala wa majimbo iwe raisi wa serikali kuu akikaa baada ya miaka mitano achaguliwe mwengine na yule ambaye atachaguliwa, achaguliwe kutokana na haya majimbo mengine. Kwa hivyo, kila jimbo liwe litakuwa lina uwezo wa kupeleka mwakilishi wao kila baada ya miaka mitano, kwa mfano, raisi ametoka coast province baada ya miaka mitano ijayo atoke tena coast province, mitano tena atoke coast province, jambo kama hilo liwe litaondoka.

Kila jimbo liwe lina haki litapata angalau sehemu fulani, kila baada ya miaka fulani, kila jimbo liwe litaonja kiti cha urais wa serikali kuu. Vile vile usawa wa kielimu. Haki za kielimu kwa mfano, wenzetu wengi wamelalamika, coast province hakuna university. Kwa hivyo kuwe katika majimbo kutawekwa vifungu vya kuweka usawa katika elimu. Kila jimbo liwe litakuwa na University, na watoto ambao wanatakikana wachukuliwe, kwanza wachukuliwe asilimia sabini na tano watoke katika jimbo lile, wale ambao watabaki watoke kutoka sehemu za nje.

Kifungu cha mwisho ambacho nitamalizia ni kuhusu haki ya uajiri wa wafanyi kazi wa serikali. Maoni yangu ya kwanza, ninaomba kwamba head of state, wale wakuu wa wilaya, wanatakikana wanainchi ambao wanatoka katika District zile zile. Kwa mfano, ikiwa cheo cha DC kitabaki, D.C awe ametoka, kwa mfano sisi tumetoka Malindi, atoke hapa hapa Malindi, na wengine watoke hapa hapa. Lakini sio leo kutoa mtu Lamu uje umueke Malindi, hajui mila na desturi za watu wa Malindi, hii inasababisha corruption iwe itaendelea. Jambo lingine ni kwamba wafanyi kazi asilimia sabini na tano wawe watachaguliwa kutoka hapa. Sio vijana wengi wanarandaranda, watu kwenya mabangi pengine mtu amesoma mpaka form four, university lakini kwa sababu nafasi za kazi wananyimwa. Kwa hivyo hii inasababisha yaani kuleta uhalifu na vile vile kuleta uzoroteshaji wa maisha wa wale wenyeji ambao wako katika sehemu hizi. Kwa hivyo liwe kila jimbo litaidhinishwa kulingana na Katiba kwamba wale wanaandikishwa iwe 75% wametoka katika ile sehemu ile pale. Kwa hivyo, kwa haya ninawashukuru sana na tunaomba Mungu atubariki kwa yale ambayo tumeweza kuyasikiliza.

Com. Riunga: Asante sana bwana. Simeon R. Nzai.

Simeon R. Nzai: Basi ninatoa shukrani zangu kwa ma Commissioners ambao wako hapa, maafisa mbali mbali, wananchi kwa kutupatia nafasi hii ya kutoa maoni yetu kwa Katiba. Mambo mengi yameshazungumzwa lakini nitagusia mambo kidogo kwa maoni yangu ambayo naona hayo yakiwa yatatiwa maanani na kurekebishwa, yawe katika hiyo Katiba itakayofuata, basi Kenya yetu itakuwa nzuri. Kwanza ninazungumzia kuhusu uchaguzi kadri vile ambavyo ungekuwa ni uendeleo. Tunakuta wakati wa uchaguzi baada ya miaka mitano, kuna hali ambayo wapigaji kura huwa hawapewi nafasi nzuri ya kuchagua wale ambao wanaowataka hasa. Kwa mfano, katika constituency fulani, utakuta wale wenyeji ambao wanakaa pale mahali sio ambao watapiga kura pekee yao, utakuta mtu anasimama ambaye si wa pale mahali, lakini anaenda analeta watu kutoka nje na wanapiga kura pale yeye anapitishwa pahali ambapo hatajikani. Na kwa sababu amepitishwa na watu ambao huwa wanatoka katika sehemu nyingine, kuendeleza katika ile sehemu ambayo anafanyia hiyo kazi ambayo amechaguliwa afanye, hafanyi. Kwa hivyo, ingekuwa vizuri katika Katiba tuanayotaka iundwe, basi vitambulisho viweze kuangaliwa vizuri ni wa akina nani wanatoka katika eneo lile hasa ili wamchague mtu atakayewakilisha matatizao yao vilivyo.

Tatizo lingine ambalo ninaliona ni kuhusu rais. Rais kama vile ambavyo imezungumziwa tayari na wenzangu, nasisitiza kuwa rais kwa ule mfumo unaendelea ana mamlaka mkubwa, kiasi ambacho watu wakiwa wanataka kutoa maoni yao Kenya hii haiwezekani. Kwa hivyo wanaogopa kuogopa, imekuwa hata kama chama cha upinzani kinatoa maoni yake unakuta hakina nafasi kwa sababu mamlaka yote yana rais. Tena kumesemekana ikapitishwe kuwa ni sheria 'one man one job', lakini tunakuta mawaziri, rais, wana kazi nyingi kiasi yakuwa zingine zinalala kwa sababu ni mtu mmoja na ana kazi nyingi. Kwa hivyo tuangalie nafasi hizi ambazo kuna watu Kenya, wananchi wa Kenya ambao wangeweza kuzifanya, lakini zinapewa watu ambao sasa wao wana kazi tayari, halafu hizo wanapewa wao vijana wengine wamesoma mpaka vyo mbali mbali wanapiga lami hawana kazina kazi zinarundikiwa mtu mmoja. Kwa hivyo, ingekuwa kila mmoja kazi, basi tungepinguza huu uhaba wa kazi. Kitu kingine ni kuwa wale ambao wamestaafu katika serikali, wao ndio wanarudishwa kama ni ma Commissioners, hao ndio wanapewa kazi nyingi hivyo ambazo sasa pesa zote ambazo zingenufaisha wale vijana na wale wengine ambao pia wamesoma na wanaweza kufanya kazi hizo hawaangaliwi masilahi yao, wanakuwa pale pale.

Tatizo jingine ambalo tungependa liangaliwe ni bunge. Wabunge wetu wa Kenya imesemwa tayari hapa, wanajipendekeza zaidi, wanajipenda nafsi, na hiyo ndio sababu ikasemekana ingekuwa heri wakati Katiba hii inapitishwa, wasiwe na mamlaka ya kuangalia mishahara yao, kuwe na timu maalum. Isitoshe, hawa mawaziri na wabunge tukiangalia wanajipendekeza hata hali ya kuleta vitu kutoka nje, mwananchi wa kawaida ambaye ana aanza uchumi anataka kuagiza gari kutoka nje, ushuru huo, lakini kama ni mbunge ama waziri ambao hao wana pesa nyingi, inakuwa ni duty free. Mnaonaje mambo haya? Wa kusaidiwa na duty free ni ule mwananchi wa kawaida ambaye hana pesa nyingi ama ni huyu millionaire? Kuna haki hapo?

Kitu kingine ambacho kingeangaliwa zaidi katika Katiba hii yetu ya Kenya na hili jambo limezungumzwa na watu wengi ni umiliki wa ardhi. Tunakuta ardhi kabla ya uhuru wale walionyakuwa hii ardhi, hawakuipata kwa hali ya halali, pengine kama alikuwa ni sultan amechukua nafasi hii na kuwapatia watu akisema huku hakuna watu ni mbwa na mayonda sehemu hizi. Basi

hata waarabu walipofika hapa kulikuwa na wenyeji hapa, kuna wabajuni, kuna wagiriama, kuna makabila nyingi zilikuwa zianishi hapa, hakukuwa kuna mayonda hapa. Kwa hivyo, mtu kutoka huko aje apewe ardhi hiyo yote kwa sababu kiongozi alitoka uarabuni, sasa yeye ndiye anamamlaka huku anapeana, hiyo iangaliwe na ifutiliwe mbali na kama imeshafutiliwa watu wasisumbuliwe.

Na hii imepeana nafasi kwa wale ambao sasa, hapa nazungumzia Commissioner wa ardhi na waziri ambaye anahusika na mipango ya ardhi. Nao wamepewa mamlaka ambayo kile kilichokuwa kikifanywa na yule mwarabu wa zamani ambaye hakuwa mkenya. Wanatoa ardhi kule juu mahali ambapo kuna watu kama hawa, mtu anaenda kule anasema hakuna watu kwa sababu katika rahamani, inaonekana hapo hakuna watu. Lakini hawaji wakaangalia hapo mahali hakuna watu kweli, mtu anachora huko anapewa, ukifika hapo mahali, kama ndugu aliyenitangulia hapo mwanzo anasema kuna watu elfu kumi na tano kule sehemu ya Ngomeni nao wanaambiwa hakuna watu ni mayonda, ni mayonda hao watu elfu kumi na watano? Na mtu alipewa hiyo ardhi kule. Kwa hivyo mambo kama hayo yale ya waarabu wa zamani yafutwe na haya ambayo ni ya hawa hawa jamaa zetu wakoloni wa leo pia nayo yafutwe, ili ardhi ipewe wenyewe.

Elimu: Hii elimu ni haki ya kila mwananchi na kipengele ambacho ningependa kiendelezwe ni kuwa, hali ya elimu huku kwetu imezorota sana kwa sababu hatupewi zile nafasi nzuri. Kwanza elimu ambayo inaendelea haipatii nafasi watoto ambao wanasomeshwa kuwa na hali nzuri ya kukabili maisha ya baadaye. Unakuta elimu ambayo inafundishwa hasa sehemu hizi ambazo waalimu wakiwa wanafundisha, zamani kulikuwa kuna mashamba ambayo watoto wale wanafundishwa wanaenda pia kujifunza hata kulima, kupanda nyanya na mboga. Siku hizi hakuna vitu kama hivyo ni elimu mtoto anakaa darasani kutoka asubuhi mpaka jioni na hakuna elimu ya utendaji ambayo itamsaidia yule mtoto, hata akiwa hatapata kazi akajajiri mwenyewe. Kwa hivyo hiyo iangaliwe na sehemu hiyo ya elimu pia utakuta sehemu hii yote haina shule ya upili ambayo ni ya kitaifa, mkoa wote huu. Sasa mambo haya yote unataka elimu endelee vipi. Kwa hivyo hiyo hali iangaliwe. Asante, ninaona nimemaliza.

Kuhusu mahakama, ingekuwa Katiba iangalie vizuri sana irudishe ile hali ya zamani, kuwe na kamati ambazo zitaundwa mijini kama zile za zamani walikuwa na makundi ya vaya ambayo walikuwa wanaweka nidhamu miongoni mwa jamii na wakisema jambo watu wanatii. Sio mtu ambaye ametoka huko hajui masilahi ya watu, desturi za watu ziko namna gani, anakuja anaamua vitu ambavyo hata vinazidi kuchongea mambo ambayo hayastahili. Vaya hio ndio ilikuwa mahakama yetu. Kwa hivyo kukiwa na jambo kama hilo litasaidia sana na hata jamaa watakaokuwa wanakuja katika mji watakuwa ni wapitie katika kundi hilo, wajulikane wako namna gani, wametoka wapi, wanaishi vipi kule ili wakaribishwe.

Kitu kingine ambacho hapa naona Kenya hii kinazidi ni kuwa serikali yetu imeanzisha mipango ya District Development Focus ama maendeleo ya wilaya. Hasa utakuta wilaya itaendelea vipi kama miradi hii ya maji haitasambazwa katika sehemu hizo za mashambani na hiyo elimu haitasambazwa, hali ya afya haitatengenezwa vizuri katika sehemu hiyo. Maofisi yote, vitu vizuri vyote vinajengwa vinawekwa katika miji mikubwa, na hii hali imebaki tu kuambiwa maendeleo katika mashamba. Sasa utakuta miji imejaa watu tele, machokora wamejaa kule na watu wote wanaenda kule kwa sababu huko kuna mambo mazuri.

Katika Katiba ijayo kila kitu na kiweze kufanywa mashambani na hamtaona watu wakikimbia kuenda katika miji na kujaza miji huko, kwa sababu kama ni hospitali nzuri zitapatikana mashambani, kama ni shule ni nzuri zitapatikana mashambani na usalama utakuwa umedumishwa. Kwa hivyo, Kenya hii hasa katika huo usalama, nikimaliza ni kuwa wanaolindwa ni watu wakubwa, lakini raia wale wadogo kabisa hawalindwi, na hiyo ndio sababu hata biashara mashambani haziendelei. Leo unajaza stock katika duka lako asubuhi iwe hakuna kitu, usalama hakuna. Tafadhali, kwa sababu wakati hautoshi, ninasema hivi kuwa Katiba ijayo iangalie mwananchi wa kawaida, kama ni kumaliza umasikini katika hii nchi yetu ya Kenya. Asante.

Com. Riunga: Asante sana bwana Nzai. Tunamuita bwana Dunson Matole Haji, Emmanuel Kapombe, karibu. Tafadhali mujaribu kufupisha kwa sababu tuna ambao watu wengi hawajapata nafasi.

Emmanuel Kapombe: Asante bwana Commissioner, yangu ni machache sana, tena nitaenda mbio mbio nimalize haraka. Kwanza nitaongea kuhusu uajiri wa waalimu. Hii mimi naleta mbele hapa kwa Commission kwa sababu ninaona kwamba serikali wakati mwengine hujitafutia shida yake. Kwa mfano sasa kuna shida ambayo huenda waalimu wakagoma kwa sababu ya mshahara, wanadai mshahara, serikali imeahidi kitu halafu kile kitu waalimu hawapatii. Tume ya kuajiri waalimu kama ingewezekana Katiba itaje ya kwamba, wale waalimu ijapo ni wengi ndio wale serikali iwaajiri. Kwa hivyo kama ingewezekana napata swali hapa ya kwamba mtu ambaye anaajiri mfanyi kazi ndiye yule ambaye anamlipa mshahara wake. Leo hii hapa kuna waalimu wameajiriwa na Tume ya kuajiri waalimu na hapa kuna serikali, ambapo inagombana kwamba mshahara huu, walimu ni wengi na hii pesa inakuwa nyingi na mtu kuwa na moyo wa kufanya kazi ni awe amelipwa vizuri. Huwezi kulipa jaji milioni moja kwa mshahara wa mwezi mmoja na mwalimu aliyemfunza jaji pale analipwa shilingi elfu saba, elfu nane. Hiyo ni dhuluma kabisa. Kwa hivyo ninaomba kama itawezekana Katiba ya leo itilie maanani moja kwa moja, TSC iakiandika waalimu iwe na uwezo itoe budget kwa serikali itoke na pesa kule ndio lile pendekezo la mshahara wa waalimu itolewe na Teachers Service Commission walipwe waalimu waridhike, wafundishe watoto wetu. Watakao ingia hasara saa hii kama walimu wamegoma ni wazazi kwa sababu watoto watakosa elimu, kwa hivyo mimi nasema Katiba mpaya itilie maanani hali ya kuajiri walimu na kuwalipa. Ikiwa control ya mshahara iko juu ya mtu mwingine na anayeajiri ni mwingine, hapo kunaingia shida.

Pili, ninaongea habari ya labour. Sheria za labour mimi ningeomba Katiba iangalie. Saa hii sijui kama kuna sheria za labour au la, kwa sababu utaona yakwamba, kwa mfano, hapa makampuni ya chumvi ijapo hii ni ya Kenya mzima, ni kwamba watu wanaajiriwa wanapata mateso hapa na pale. Saa hii ukiingia hapa hata ruhusa ya kuingia kwa chama cha utetezi hawana, ukianzisha chama cha utetezi pale unafutwa kazi. Kwa hivyo, watu wa labour wakiingia hapo, serikali hii tulioko nayo sasa, ni waende pale waende washibe na watu waendelea kuteseka. Kwa hivyo hapo ingekuwa jambo la maana sana, labour iimarisha sheria zake ili wafanyi kazi wapate utetezi direct kwa serikali kwa sababu sasa inaonekana hakuna sheria inayolinda watu wanaofanya kazi.

Tatu, yangu nikusema ya kwamba ardhi, ardhi tunashangaa ya kwamba mkoloni aliondoka na ukoloni wake. Lakini ajabu mpaka leo kuna vyeti ambazo ni British Protectorate ambazo kufikia leo vyeti vya kutoka mkoloni mtu anamiliki shamba hapa.

Hiyo ni ajabu kubwa hata leo hii Commissioner, kuna kesi hapa yakwamba mtu ana cheti cha kutoka mkoloni na anfukuza watu kutoka kwa eneo ambalo ni la umma la kuekesha n'gombe. Hiyo ni ajabu. Watu wameandikiwa mashamba yao wapate vyeti vyao vipya, lakini inakuwa cheti kile cha mkoloni kinatambuliwa? Kwa hivyo ni maoni yakwamba Katiba yetu mpya ifutilie mbali uweko wa vyeti vya zamani vya kutoka British Protectorate, vile vya kutoka uarabuni sultani. Mwenzangu amesema hapa viondolewe kabisa na watu waweze kuishi kwa vyeti vipya vya serikali yetu.

Lingine ni kuhusu security. Tutateta hapa na pale lakini hali ya kuleta maendeleo ya nchi ni watu wawe wametulia vuzuri, wanafanya kazi zao za mashamba na kila kitu. Lakini utakuta kwamba sehemu zingine za Kenya ile hali ya security hakuna. Kenya hapa kuna wageni wengi ambao wanaingia kwa milango ya nyuma, wanaingia mipakani huko. Katiba iongee vizuri kuwe na hali ya ulinzi wa kutosha. Saa hii hata ukifika Nairobi kuna wasomali matajiri ambao wamekaa huko, ukiingia Mombasa hali kadhalika, watu matajiri wameingia na wapi? Kwa hivyo hali ya security inaleta taabu hapa, saa hii watu wanavunjiwa nyumba zao, hawawezi kulima mashamba yao kwa sababu wao usalama kwao hakuna. Kwa hivyo Katiba hii itilie maanani sana usalama wa wananchi wa Kenya, maanake tukiwa salama ndio maendeleo.

Lingine ninaunga mkono kwa dhati – majimbo. Ndio lengo la pekee la mwananchi, leo kutoka pembe hii hapa mpaka mwisho. Juzi nilisikia redio kile kipindi cha maoni ya wananchi kutoka pembe ya Turkana mpaka Tana River mpaka wapi, wote wanasema kuwa ni majimbo. Kwa hivyo hata mimi naunga mkono Katiba mpya itaje ama itoe uhuru serikali ijayo iwe ya majimbo.

Uridhi. Kama ni uridhi ujue kuna mume kufa mwanzo au mke afe mwanzo. Sasa shida ni kwamba, ikiwa mume ametangulia kufa yule mama Katiba inaweza taja kwamba yeye apate uridhi wa bwana yake. Lakini ujue pia kuna wanawake ambao nao pia ni waharibifu. Pengine ndungu yangu akichukua nafasi yangu aweza kuwa mbaya awache wale wanangu wakateseka. Lakini ujue pia kuna wanawake wengine ambao wakipata uridhi na yeye pia anaangalia kwao anasahau watu wangu na wanangu, wako pia ambao ni waharibifu. Sasa mimi ninatoa maoni ya kwamba lile jambo la busara, Katiba hii kama ingekuwa inafaa, huyo mama aweze kuwa chini ya mamlaka ya watoto lakini kuna uhuru wa mimi mridhi wangu awe ni mwanangu wa kiume na saa zingine achukue uridhi yeye pengine achukue uridhi wa mke wangu halafu pia sheria iangalie. Je, na yeye kwa kuwa ananipenda pengine afe baada ya mwaka moja, sasa mimi nimekufa na yeye pia amekufa. Sheria sasa iangalie hapo, mali yangu itakuwa salama namna gani? Akifa kama hakuna sheria nzuri kwa Katiba hii anaweza kuandikisha watu wa kwao. Na mimi sipendi aandike hivyo, kwa hivyo iwe salama mikononi mwa watoto wangu. Halafu kuna lingine ningetaka kuongea ambalo lishaongewa kutoka-----

Com. Riunga: Tafadhali mzee ako na haki ya kutoa maoni yake.

Emmanuel Kapombe: Kutoka sub-location, kuenda kwa chief ambayo ni location mpaka division, ingekuwa jambo la maana sana sisi raia Katiba hii iseme tupige kura kwa wale watu, sub-chief, chief na DO hapo ingefaa.

Oni langu lingine ni kuhusu agriculture – bwana commissioner, hapa tukiangalia saa hii, uulize hapa maafisa wengine utakuta wananchi hapa hawawajui. Wanafanya kazi yao ya ukulima, wakijielimisha wenyewe huko na utashangaa katika mkutano utakuta yule afisa wa kilimo. Katiba hii itiwae maanani kuelimisha watu kwa hali ya kilimo, Kenya yetu tunategemea kilimo, kwa hivyo kama hakutakuwa na elimu ya kutosha kwa ukulima sio jambo nzuri. Kwa hivyo, kuwe Katiba hii itoe namna ya wakulima kuelimishwa waweze kupata elimu na waweze kuwa na ukulima wa kisasa bwana Commissioner. Katiba iwe inaruhusu kama inawezekana huwezi kula bila pesa ukiniambia jembe ndogo la mkono wagiriama halina maana na lile la maana ni tinga tinga. Tinga tinga ni ya nini na senti sina, nitalima aje? Kwa hivyo, kuwe na uangalifu kwa kuangalia mikopo ya wananchi iwe serikali inaangalia, sheria iangalie mikopo kwa wananchi waweze kusifu hapa sisi ni wakulima sote. Ukulima wa ufugaji, wa mahindi na mambo mengine, lakini tuangaliwe katika kilimo tutapewa msaada na serikali kinamna gani? Katiba iongee hivyo.

Ninafikiri la mwisho kabla sijamaliza. Uwezo wa rais ni mkubwa mno, anaajiri Chief Justice, aajiri Kadhi, kuna vyeo maalum vina presidential appointments. Watu wanaajiriwa na Moi mwenyewe ama rais yule. Itakuaje mtu ambaye umemuajiri kazi asikusikize wewe. Kwa hivyo, jaji pale anaweza kupigiwa simu na rais kwamba kesi hiyo ni ya mtu wangu iwache na akawacha, ama hiyo haiwezekani?

Audience Inawezekana.

Emmanuel Kapombe: Ukweli ni kwamba yule mtu ambaye atakuwa anatoa vyeo kama vile asiwe mtu mmoja. Rais wa Kenya ana mamlaka makubwa mno, yapunguzwe asilimia hamsini.

Investments. Wenzangu wameongea hapa. Hapa kuna aibu kubwa sana, hapa kwetu, lakini ninaongea kwa Kenya nzima kwa jumla. Katiba iongee wazi kwamba kama hapa ni mfano tu, utakuta chumvi ya mamilioni ya pesa inatoka, lakini hakuna senti ambayo inakatwa. Kama ingewezekana, Katiba mpya ipeane uwezo kwa county council wachukue pesa za maendeleo ya kule ile mali inatoka. Ingekuwa jambo la maana sana hata kama ni asilimia ishirini ya mapato ya pale yaingie kwa county council yetu ya maendeleo wacha ile ambayo ni ya maendeleo ya county council, maendeleo ya area kule mali inatoka, kama ni chumvi au mambo mengine, itakuwa jambo la maana sana. Twenty percent ipitie kwa county council ama kwa njia nyingine ambayo Katiba itakuwa imeruhusu kwamba mwananchi wapate kwa sehemu ya maendeleo, si wahindi kutajirika hapa na wananchi wanaendelea kupoteza maisha.

La mwisho ningesema yakwamba constituencies zingine ni kubwa sana, zikatwe ziweze kuwa na wabunge wawili, na nikitoa mfano ni Magharini. DO wawili wa Magharini wana mbunge mmoja na ninajua si Magharini peke yake, kuna kwingineko huku Kenya, ambapo watu ni wengi na ma-DO pengine ni wawili na mbunge ni mmoja na pengine tayari huyo mbunge, eneo ni moja linamshinda, itakuwa eneo ya mara mbili. Mbunge awe ana DO wa Magharini, ana DO Marafa, ana DO Turkana, ana DO

upande mwingine. Hiyo itakuwa ni jambo ambalo si rahisi mtu kutofanya kazi. Itakuwa jambo la maana Katiba iangalie zile sehemu ambazo ni kubwa zikatwe ziweze kuwa na wabunge wawili. Tukibahatika Marafa itakuwa na mbunge na hapa pia kutakuwa kuna mbunge.

Uhuru wa kuabudu: Serikali yetu tukufu tunashukuru uhuru wa kuabudu uko lakini hautekelezwi vile ambavyo unapaswa kutekelezwa, kwa sababu utakuta mambo mengi. Kwa mfano, mkutano kama huu kama ungaliitwa siku ya Jumapili au Jumamosi ama pengine hata Ijumaa kwa saa fulani, ungewakosa hawa watu. Kwa hivyo, ule uhuru wa kuabudu kama ni siku ya kuabudu ziwachwe kando, zile siku za kazi mje tufanye kazi kwa pamoja. Katiba itaje wazi ya kwamba uhuru wa kuabudu kama ni mikutano yetu ya kimaendeleo ifanywe siku za kazi. Kama ni mikutano yetu ya mambo gani, siku za kazi. Siku za kumwabudu Mungu zibaki ni siku za kumuabudu Mungu moja kwa moja. Ninasema asante kwa kunipa nafasi.

Com. Riunga: Jiandikishe tafadhali. Mwingine ni William Sidi, Ahadi M. Kiti, Julius Nzaro, karibu.

Julius Nzaro: Jina langu ni Julius Nzaori. Mimi ninataka kusema hivi, babu na mababu zetu walin'gan'gana kwa jasho wakamwaga damu. Lengo, madhumuni na shabaha yao kubwa ilikuwa katika mambo mawili. Jambo la kwanza, walikuwa ni kupata uhuru wa kujitawala. Jambo la pili lilikuwa ni kuikomboa nchi yetu kutoka kwa mkoloni na mwarabu ambaye alikuwa ametutesa kwa miaka mingi. Swali langu ni hili sasa, je Katiba yetu ya kwanza ya serikali ilihusika vipi katika swala la kukomboa ardhi kutoka kwa mkoloni na mwarabu? Kama serikali haikuwalipa ridhaa hawa watu wakoloni na waarabu, kwa nini? Na kama iliwalipa mbona sasa sisi watu wa pwani, Magharini Constituency bado ni ma squatter katika enzi ya miaka thelathini na nane ya uhuru? Maoni yangu ninataka niseme hivi, hali hii imetuadhiri sana sisi watu wa pwani na Magharini Constituency kibiashara, kimaendeleo tofauti tofauti. Mapendekezo yangu nataka niseme hivi, nataka Katiba hii iwe na sheria na sheria hii ipewe uwezo na mamlaka makubwa ya kumlinda mwananchi au raia wa kawaida dhidi ya matajiri na mamlaka ya serikali. Tajiri asipewe uwezo wa kutumia utajiri wake kumgandamiza mwananchi kupata haki yake. Na mamlaka ya kiserikali yasitumiwe kumgandamiza mwananchi kupata haki yake. Ni katika njia hiyo sisi wananchi wa kawaida tunaweza kupenyeza juu kwa maana tutakuwa na support ya kushikwa kotini, tunaweza kufuatania mambo yetu tunayofanya, lakini bila hivyo hatutaweza.

Jambo lingine ni kwamba serikali sasa tunaelekea hali ya uchaguzi. Serikali itapoteza pesa nyingi sana katika campaign. Kwa nini pesa hizi zisitumiwe kiasi kukomboa hizi shamba, zetu zote, hizi tatizo zote za mkoloni kwa nini zisikombolewe sisi wananchi tukapata hizi title deed zetu? Pesa zile zikombole mashamba yetu tupate title deed zetu tupate kujiendeleza na sisi.

Jambo la mwisho naunga mkono serikali ya majimbo. Kuhusu urais nasema kwamba mamlaka kidogo yamezidi. Kuna jambo moja ambalo kidogo naona si nzuri hata kidogo. Katika nyanja ya kuelepeana uwaziri ama waziri mdogo, utakuta leo fulani na fulani ni waziri wa afya, fulani na fulani ni waziri wa ardhi, haimalizi miezi tatu wameshabadilishwa wameenda huku huku, there is a reason behind that. Hatutaki namna hiyo, tunataka kama mtu ni waziri wa afya, kama ni mtu wa fedha kama ni mtu wa ardhi

awe pale ndiposa tatizo likija tunajua ni nani wa kufuata. Lakini leo hapa, leo pale, inaonekana kuna reason behind that one ambayo inazidi kutuumiza sisi. Asanteni.

Com. Riunga: Adnan Salim

Adnan Salim: Jina langu ni Adnan Salale Salim. Asanteni sana Commissioner na wageni wako pamoja na wananchi wote ambao mko hapa. Maoni yangu mimi ni kama yafuatavyo. Mnajua mwanadamu wowote yule, kutoka yule wa mwanzo mpaka huyu ambaye tunazungumza sasa, mimi na wewe. Hakuna mwanadamu ambaye ako responsible, yaani akodhamana kudhamini wengine awe atawatendea sawa, hakuna. Na kitu kinachomchunga mwanadamu ni sheria, halaiki haingekuwa sheria basi mwanadamu angekuwa anaishi zaidi ya mnyama yule ambaye ako chini yake. Mwanadamu ako juu, mnyama ako chini lakini angemshinda kwa maovu wa yule mwanadamu, lakini kinacho m-control na kumfanya auadilifu ni sheria. Kwa hivyo, hayo yote ninayoyazungumza mpaka tupate kitu sheria iwe ni sumu kwa kila mtu, yaani iwe maana yake ni hivi, sumu ile ikiwa natumaini nyinyi wote mnamjua mnyama yule paa alioko msituni na ndovu, iwe ina maana kwamba ile sumu paa akila atakufa, na ndovu akila atakufa naye. Si kwamba leo paa amekula ile sumu tumemzika kesho ndovu amekula anajitembelea na jamaa zake, hiyo huku hakuna. Maana kusema hivyo ni kwamba, hakuna kutukana kiongozi yaani president, viongozi na hata yule mwananchi wa kawaida wawe chini ya kibanda yaani sheria, wote, hakuna ambaye atakuwa above the law. Hiyo above the law si democracy. Wote tuwe chini ya sheria, kumaanisha kwamba ikiwa mwanaichi wa kawaida akifanya makosa, akiwa atashtakiwa na hata yeye president ashtakiwe hata yeye DC ashtakiwe, hata yeye DO ashtakiwe. Hiyo ndiyo itavunja ufisadi. Lakini kusema kwamba tumchague chifu, ndio tutamchagua tu kwa kura okey, sawa, lakini si atafanya ufisadi? Lakini kama sheria iko ile itakayo mshika chifu na ile itakayomshika president iwe ni moja, hakuna ufisadi, hakuna lolote.

Pili, ni huu utawala ambao tuko nao sasa. Tunadai kwamba ati tumeangusha uchumi ni kwa sababu ya uongozi. Sababu kama kuna gari yako na inabeba tani ishirini, je ukibebesha tani hamsini siitanguka? Siitaanguka? Sasa vipi wewe leo unatuambia hapa kwamba uchumi umeanguka, unafanya retrenchment, yaani kuwafuta wale watu, unafuta yule mwenye elfu tatu unamuacha mwenye elfu mia nne anakula, kwa nini? Mwenye elfu mia nne tena yeye ni mzee badala ya kukaa nyumbani amuache yule kijana ambaye ameanza sasa wa elfu tatu ndio anafutwa anaenda kurandaranda, awe mwizi na yule wa elfu mia nne pengine ana ghorofa ashafanya kazi zaidi ya miaka ishirini anakaa kazi, ambao hicho ni kitu ambacho kimechangia uovu Kenya yetu. Kwa hivyo, kifungu maalum ambacho kinaharibu na hata Afrika yetu inaleta coalition ambayo kama wenzetu vile Congo, Rwanda, Zaire, Somalia ni kwa sababu kifungu hiki hakuna kwamba yule akifanya uhalifu unawachwa mdogo ndiye anahukumikiwa na mkubwa anaiba na anawachwa. Ikizidi sana, mtu kwa mfano yaani kama ni mtawala wa hapa Malindi akifanya uhalifu unapigwa transfer anapelekewa Nairobi na mambo yanaishia hapo kwa sababu yeye ni mkubwa. Lakini akifanya mtu mdogo tu kawaida, kesho unamkuta mahakamani, unaona ambayo ni kitu makosa hayo ninayesema. Kwa hivyo, ninawaambia kwamba ni afadhali tuwe na sheria moja sote katika kibanda kimoja ndioittoa huu wasi wasi. Ninamalizia hapo, asanteni.

Com. Riunga: Asante sana kwa hayo maoni yako, sasa tuko na bwana Julius Kisao, Josphat Wanyama, Keya Chengo

Mramba, karibu.

Keya Chengo Mramba: Asante sana bwana mwenyekiti, Commissioners. Ndungu zangu kwa hakika hii leo ni siku nzuri sana na ni siku muhimu kabisa kabisa. Nashukuru, nimeandika kitu kidogo hapa lakini kwanza nitazungumzia kwa ufupi kuhusu mfumo wa Katiba gani tunayoitaka. Katiba tunayoitaka tumezungumzia kwa kirefu sana na wenzetu ambao wametangulia. Na mimi pia nitazungumzia maana lengo letu ni lile lile moja tu, nafikri hakuna zaidi. Katiba tunayoitaka sisi hapa katika mkoa huu wa pwani ni Katiba ya ule muundo wa serikali ya majimbo, ambapo mamlaka ya nchi na bunge yawe yamegawanywa baina ya serikali kuu na majimbo maalum. Hii habari ya majimbo ilikuweco kutoka enzi ya kutafuta uhuru. Wakati ule si kupiga kura lakini bendera ilipopepea nilikuwa kidogo ninaona. Sisi katika mkoa huu tulipigania majimbo, lakini mambo siwezi kuzungumza kwa kirefu sana vile ilivyokuwa mpaka Katiba ya majimbo ikaondolewa lakini sasa baadaye tulijua kwamba kulikuwa na malengo fulani ndio sababu Katiba ya majimbo ikaondolewa na yale malengo ambayo yalikuwa yakitakikana nayo pia tumeyashuhudia. Lengo lake lilikuwa ni nini kuondoa Katiba ya majimbo, mpaka sasa sisi tuko pale pale, kwa mfano, mtu wa pwani hapa katika mkoa huu, sio sisi watu wa pwani peke yetu, kuna wenzetu huko mikoa fulani fulani mpaka sasa tunasema hakuna serikali ambayo itaweza kutuweka salama hapa katika nchi hii bila ya serikali ya majimbo. Serikali ya majimbo ili tupate uhuru wa amani na haki ni majimbo.

Pili, ilikusaidia wakaaji wa kila jimbo wajiletee maendeleo, hakuna serikali ambayo inaweza kuwa na mambo kama hayo isipokuwa ni majimbo. Tatu, kuleta umoja wa hiari kwa nchi nzima, hakuna serikali itakayo fanya hivyo isipokuwa ya majimbo. Nne, kuwapa wakaaji wa majimbo uraia kamili, serikali kwa kupitia provincial councils zao. Hakuna isipokuwa ni serikali ya majimbo peke yake ndio itakuja kutuweka sawa. Serikali ya majimbo itakuja kutufanya sisi katika Kenya hii tuishi kwa amani na usalama wa sisi tulioko hai sasa na vizazi vijavyo. Hakutakuwa na shida ya ile tribal clashes Kenya nzima ikiwa kila mkoa utakuwa unajitegemea, unajitawala yenyewe. Kusema hivyo, hatusemi kwamba tunalazima kwamba tuwe na serikali ya vipande vipande yaani hapa kuwe kuna president, kuwe kuna nani, yaani kuna jeshi letu hapana. Serikali iwe ni serikali ya umoja lakini kila mkoa uwe unajitegemea kiuchumi, mipangilio yote yawe yanapangiliwa kimkoa bila kuingiliwa na serikali kuu hata kidogo. Ikiwa hivyo, sisi wenyewe hapa tutaweza kunufaika, itakuwa ni kama sasa tunaanza uhuru ule ambao tulinyimwa miaka arobaini iliyopita, itakuwa na sisi tumeingia kwenye uhuru na sisi kwa kila kitu.

Councils zetu ziwe ndio ambazo zinaweza kuamua kila kitu. Wajumbe watakuwa wanazungumzia mambo ya Kenya nzima kwa jumla, kama tutakuwa na waziri mkuu, ama president ama nini, lakini kila jimbo liwe litakuwa na nafasi lenyewe kujiamulia kila jambo, maendeleo, elimu na kila kitu. Kama ni uwanja wa international airport, tunaamua wenyewe hapa hapa mkoani, tunajenga, wazungu wanakuja huku, wageni wanakuja direct. Hapo tutakuja na sisi watu wa pwani tuinuke tuwe kama watu wengine. Inasemekana kwamba hapa sisi hatusomi, tunasoma, lakini vifaa vya kusomea viwapi ikiwa wewe maskini, nyote kwa jumla ni maskini, mtaa mzima pengine muna skuli yenu hapa lakini ni maskini hamjiwezi, mtaijengaje skuli iwe inaweza kuleta manufaa, watoto wanaweza kufaulu vipi bila vifaa maalumu ikiwa wazazi wenyewe ni maskini, haiwezekani. Lakini wenzetu kwa vile walibahatika wakapata viongozi ambao walikuwa wako karibu nao, wamepata nafasi wakajenga maskuli, vifaa vyote

wakawa navyo. Kwa hivyo ikawa nao watoto wanapita vizuri, university wanaenda lakini sisi hapa tumefinywa, umasikini umetuzidi hata leo hebu niambie kama mtoto wako bahati nzuri amepita basi anaenda university Nairobi huko, huwezi kumpeleka mtoto wako university. Hapa utazunguka wewe mpaka mwisho utalala na ni basi huwezi kuinuka tena, kwa sababu ya nini, hiyo serikali ya umoja, tushaiona mambo yake, hakuna kitu kipya ambacho tunaweza tukaambiwa kuhusu serikali ya umoja. Kwa hivyo, sisi tunataka ile kufanya kwa uzuri, tuantaka ile ile Katiba ya majimbo iwe ni ile ile, ituponyeshe na sisi angalau watoto wetu sisi tushafika kati kati lakini watoto wetu angalau waje wapate hewa safi angalau nao, kiuchumi na kielimu.

Kwa hivyo, time ni kidogo, nitaondoka hapa lakini mwito wetu ni nini jamani? Majimbo, mpaka yaje, si la hivyo hakuna usalama.

Com. Riunga: Haya asante, tatamuita bwana Josphat Mutiki.

Josphat Mutiki: Asante sana Commissioners ambao memefika hapa, wanainchi kwa jumla. Yangu yatakuwa machache sana kwa sababu mengi yashazungumzwa na hayo yangu ndio yale wananchi wametangulia kuyazungumza. Katiba yetu, tunataka nini, tunataka Katiba ya namna gani sisi wananchi wa Magharini? Wananchi wa Magharini Katiba ambayo tunaitaka ni Katiba ambayo itaundwa kwa wakati huu, tungetaka kuona Katiba ambayo mamlaka yako kwa wananchi wenyewe, na Katibai si nyingine bali ni Katiba ambayo itaipatia majimbo mamlaka kamili. Serikali ya Majimbo muundo wake utakuwa namna gani, ambao utamwezesha mwananchi wa kawaida kuwa na mamlaka ni serikali ambayo itakuwa nguvu zake ziko kwa local authorities. Councils ziwe ndio mashina ya serikali yetu ya majimbo. Madiwani wanapoenda kwa councils iwe hapo ndio mambo yote yanayohusiana na jimbo hili yataamuliwa pale pale. Council iwe na wakilishi kutoka kila district. Kama tuko na district ya Malindi, tuwe na district moja, council moja hii itakuwa chini ya mwenyekiti na mwenyekiti na madiwani wake watakuwa wamechaguliwa kwa pamoja na wananchi moja kwa moja. Inaamanisha kwamba mwenyekiti wa council awe anachaguliwa moja kwa moja na wananchi na hii itawapatia nafasi wanainchi kuona kwamba mambo yao ambayo wanayataka yatekelezwe yanapitishwa vizuri kwa council na hii ndio itakuwa ni nguzo ya kwanza ya ile serikali ya majimbo. Na chairman wa council atakapokuwa anachaguliwa na wananchi awe na running mate au yule vice wake wawe wanachaguliwa wakati mmoja.

Baada ya councils, kuwe kuna assembly ya region. Assembly ya region hii iwe inahudhuriwa na chairman na Member of Parliament, hao watahudhuria assembly ile ya region ambayo itakuwa chini ya kiti ya governor. Hii itakuwa inaangalia mambo yote ya region ile. Sasa yale yote yatakayokuwa yamepitishwa katika council, nguzo au kilele chake itakuwa ni pale kwenye region assembly. Hapo ndio itakuwa imefikia kikomo ya yale yote ambayo councils zimekata shauri. Mheshimiwa mbunge yule yule ndiye atakayekuwa anahudhuria kule juu kuwakilisha yale ambaye yatakuwa yemetoka kwa Regional Assembly. Hivi, nina maanisha ya kwamba baada ya council, tuko na regional assembly na ile National Assembly. Ile nationa assembly itakuwa inahudhuriwa na yule mbunge ambapo vile vile atakuwa yeye na chairman wamehudhuria kwa ile regional assembly. Kwa hivyo, yale maoni ama yale yatakuwa yanakiwango cha kupita jimbo lile yatakuwa yanapelekwa kwa National Assembly na mheshimiwa mbunge yule. Ni kwa nini tunasema serikali ya majimbo ndio itatufaa?

Ardhi: Ardhi limekuwa tatizo ya kila pahali na limekuwako tangu hatujapata uhuru na tuko nalo mpaka leo. Tatizo hili linatoka wapi? Mamlaka. Mamlaka ambao amepewa Commissioner ndio tatizo ambao limekuwa likisumbua na litaendelea kusumbua mpaka mamlaka yale yatolewe kwake na mamlaka haya yatakapotolewa kwake yataenda wapi? Mamlaka yale yakitolewa yanatakikana yarudi hapa hapa kwa council. Mambo yote ya ardhi inatakikana yawe kikomo chake ni kwa council na yakizidi pale itakuwa ni kama habili, inaenda kwa regional kwa sababu ni council ambayo iko huko kwa mashinani inajua wananchi wake, wananchi wako karibu nayo. Hivi itakuwa ni rahisi ufiadini wowote kama utatokea hapa kwa council mwananchi wa kawaida ana uwezo wa kuuona mara moja, ana uwezo wa kufika na kuujadili na kupata haki yake. Kwa hivyo, kama ardhi itakuwa inatolewa na council, hii itarahisisha kuona kwamba hakuna ile kwamba mtu ataambiwa Mamburi mpaka Ngomeni, hakuna watu kwa sababu diwani ambaye yuko pale anatoka Ngomeni, anatoka Mamburui na anajua kuna watu. Kwa hivyo, itakuwa ni rahisi kumpatia haki mwananchi yule ambaye anaishi pale.

Serikali ya majimbo – Judiciary. Katika kila jimbo kuwe kuna sehemu ya mahakama ambayo imeanzia kwa district mpaka ikifika kwa jimbo iwe ni kikomo chake. Ikipita pale iwe inaenda Court of Appeal ambayo ndiyo itakuwa inaenda kwa serikali ile ya unitary government. Hii itarahisisha kesi zote ama haki zote ambazo mwananchi ana haki ya kuzipata, atakuwa ni rahisi kuzipata akiwa hapa hapa kwa hii level ya district na inapoondoka hapa inakomea hapo hapo kwa regional ambayo hiyo itakuwa katika jimbo hii. Unaelewa kabisa kwamba kesi yangu ambayo ama kesi ambayo inaambatana na mahitaji ama na vile hali ilivyo katika sehemu hii ni wale ambao wataisikiza ni wale ambao wanajua ile hali halisi ilivyo katika sehemu hii.

Hospitali: Katika serikali ama Katiba ambayo tunataka ambayo itaandikwa wakati huu, tungetaka kuona kwamba mahospitali yetu yote ambayo yatakuwa katika region hii yanatoa matibabu ya bure, na hii itawezekana namna gani? Hii itawezekana kwa sababu katika ile serikali yetu ya majimbo tunaisema kutakuwa kunatoka kiwango kama kumi na tano kwa mia ya mapato yetu yote ndio inaenda kwa serikali kuu. Hii ndio itakuwa ina maintain yale ya serikali kuu. Lakini thamanini na tano kwa mia ile yote ambayo ni mapato yetu itakuwa inabaki hapa hapa na council yetu ambayo itakuwa ndio agent wa kukusanya kodi ile itakuwa ni macho ya karibu ya mwananchi. Kwa hivyo itakuwa ni rahisi kutoa matibabu ya bure kwa sababu ya pesa ziende juu ndio tuletewe kile ambacho wamepanga juu pesa, tatakuwa tunatoa ile asili ambayo inatakikana kwenda juu na ile nyingine inabaki hapa na sisi wenyewe tunapanga vile ambayo tunafanya.

Basi ningependa kumalizia ya kwamba ile serikali kuu mamlaka yake ambayo itabaki nayo ingekuwa ni mamlaka ya foreign affairs na security. Hii kumi na tano kwa mia ambayo tunasema itaenda kwa serikali kuu, hii itakuwa inaangalia mambo ya security na mambo ya foreign affairs. Hii ndio itakuwa iko kwa serikali kuu, zile zingine zote ziwe zinaangaliwa katika stage ya regional. Mwisho ningependa kusema kwamba uchaguzi wa rais uwe wa vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Na wakati ule wa kuchagua rais awe anachaguliwa na running mate wake. Hii itapatia nafasi yule makamu wake kufanya duties sawa sawa ama baada ya zile ambazo anafanya rais kwa njia ya mwafaka kwa sababu yeye hatakuwa hana shaka kwamba kesho anaweza kuondolewa na rais ama kesho kutwa anaondolewa na nani kwa sababu wananchi watakuwa wamemchagua moja kwa moja

kutoka mashinani. Basi, kwa hivyo, nasema ni asante Commissioners na wananchi kwa jumla na Mungu awabarike kwa Katiba yetu mpya.

Com. Riunga: Asante sana tumpate Salim Abdalla, karibu mzee.

Salim Abdalla: Jina langu naitwa Abdala Salim Bokia na ni mkaaji wa hapa Nabomani, hapa nimekuja biashara lakini mji wangu uko Bomani sub-location, Magharini location, Magharini division. Kwa hivyo mimi ninazungumza kama mfanyi biashara na kiongozi wa dini ya kiislamu. Kitu ambacho nataka kukizungumza juu ya Katiba hii nikusema kwamba uwezo wa mtukufu rais ni mkubwa sana, kwa hivyo upunguzwe.

Pili, kitu ambacho nataka kukizungumza ni kwamba katika constituency kama ya Magharini, mimi maoni yangu ninazungumza kwamba mbunge au katika Kenya nzima kwa sababu nikisema Magharini ni hii hii, Kenya nzima mbunge hawezi kuchaguliwa kwa watu elfu hamsini. Pili, tunakuta hivi kwamba uchaguzi unaokuja tuwe na Prime Minister na Vice Prime Minister na rais naye atachaguliwa hivi. Mambo muhimu katika Katiba ya serikali ya muungano mkuu wa serikali. Mkuu wa serikali ya mungaano yaani Federal Government (F.G.) awe ni Prime Minister ambaye amechaguliwa moja kwa moja kwa kura. Kwa kusema hivi ni kusema kuwa mtu yeyote aweza kusimamia kiti cha Prime Minister bila ya kupitia chama chochote. Lakini sikusema kuwa vyama vya siasa havitaweza kutoa mgombeaji uchaguzi yaani candidate wao kwa kusimamia kiti cha Prime Minister.

Ndugu zangu wengine wamesema maneno ya elimu. Wakati tukichagua, tunachagua kwamba sisi tunataka serikali ya muungano ili kusudi kwamba raisi awe uwezo wake uko chini na sisi tuweze kufanya mambo yetu pwani. Na serikali hiyo itakuwa serikali nzuri itakuwa si kama huku kuoneana. Kwa hivyo, sina mengi ya kusema na kushukuru Bwana Commissioner kwa sababu anasema kwamba chumvi nyingi ni mbaya. Ukiwa unataka kula nyama vizu kidogo lakini igizia chumvi, je ni sawa sawa, lakini sasa ukiitia chumvi huenda wakati mwingine ukasema fulani anasafiri kwa sababu ya kupenda chumvi nyingi na wewe umekuja hapa Gongoni na Gongoni chumvi ndiko kwao, umesikia habari za chumvi, kwa hivyo mimi sitaki kutia chumvi nyingi lakini ukirudi usalimie wale wenzangu ambao ni candidates kama mimi. Asante sana.

Com. Riunga: Asante sana mzee Abdala Salim...Shikali Mbathi...nafikiri

Speaker: Ni mimi

Com. Riunga: Haya karibu

Shikali Mbathi: Basi, Bwana Commissioner, Bwana D. O. na viongozi, asanteni sana kwa siku hii ya leo, kutuletea mipangilio ya katiba yetu mpya. Ni jambo ambalo ni la busara na linalo tamanika. Mimi maneno yote yameshazungumzwa na wasemaji

walio tanguliwa. Nitagusia tu mambo machache. Kwani mtu akiwa amefanya kazi katika serikali yetu na ameshamaliza miaka yake na amestaafu, sawa sawa mtu huyo ana haki yakupatiwa tuzo kutoka kwa serikali. Sasa kama ni tuzo la ardhi, mtu huyu aliyestaafu ameoka kwa mfano, Ukambani au Bungoma, mtu akiwa atapatiwa zawadi ya ardhi kwa kuwa amestaafu kwa serikali anastahili apatiwe kule alikozaliwa au apatiwe sehemu nyingine? Basi ni kaiba hii, tunayoitaka sasa, hii ambayo tunayo sasa ishamaliza beach zote za Pwani yetu. Maadui tulionao wakutunyanganya hiyo ardhi na ploti za beach, ni wale viongozi wakubwa wakubwa ndiyo wanagawanya huko, sisi tulio hapa hatuna chetu. Naangalia jambo la kusikitisha, kama umetaka upewe ardhi kwa kuwa umestaafu, kama ngaa lao ni mahali ambapo wewe unataka kuishi. Hai! Jambo kidogo, na kumbe ni upatiwe hiyo ardhi. Hiyo nchi utakayopewa basi uuze upate mamilioni ya pesa, halafu uwanzie wahindi wakae pale, si tunasema ni wewe kumbe ni wahindi ndio ulikuja nao, hio ni haki? Kuna haki hapo? Hakuna haki.

Katiba hii tunayoitaka, hii mpya, iandikwe kwamba mtu akistaafu kutoka kwa serikali akiwa atapatiwa ardhi, apatiwe sehemu aliyotoka. Hiyo ni juu ya uongozi wa serikali vile ambavyo tumnyanyaswa sisi kutoka mambruiu mpaka huko, kutoka huko mpaka huko ni wageni wamekaa, wametajirika, sisi wenyewe hapa tuko vile vile maji mafu. Basi Bwana Commissioner kama wewe umekuja kusikia maoni, maoni yangu yanasema hivi, mtu apatiwe sehemu aliyotoka, hii sehemu ambayo wenzake wanaishi binadamu kama sisi kama yule msemaji aliyesema, na sisi tupatiwe kule hicho cheti cha Title Deed kitatoka wapi, kiko ulaya au kiko hapa Nairobi? Kwa nini sisi hata waliokwisha kulipa haya mashamba hawajapata Title Deed, lakini atokaye kule akija ana Title Deed, unaliona hilo jambo? Hayo ni mipango wa serikali. Uongozi ambao unaendelea kwa serikali hii tulionayo ni neno lililo la uhaini, likifika mbele ya ofisi ya mtumishi wa serikali ligeuzwe liwe pesa, watu wale wapate kufura matumbo, uhaini ubaki vile vile. Hakuna ofisi moja ambayo mtu atakwenda afanyiwe kazi na kirauni. Kirauni imevaliwa kichwani na haina kazi hiyo na kazi ni pesa, sawa au si sawa?

Haya, nitagusia neno lingine ambalo limeguswa na msichana hapa. Sikizeni sana nyinyi wazazazi, mimi ni mzazi mimi. Naingilia mambo ya vijana wetu, wasichana. Kuna kitu kinafanyika, nampeleka mtoto wangu katika shule, msichana. Lengo langu na lake ni aende akasome kwa maana anatakikana elimu iende pamoja, mwanamke na mwanaume. Lakini kwa bahati mbaya huyu mwanangu amefika standard seven, bado mwaka mmoja amalize masomo ya msingi. Tumbo limejaa, sasa maji yamejaa, mwalimu hamtaki, headmaster hamtaki, kamati haimtaki, mzazi naye hamtaki, ana mimba, ana mimba, afukuzwe, afukuzwe yule kijana ana miaka saba amesoma aende nyumbani. Kule nyumbani mzazi naye hamtaki, kitu gani kilichofanyika kibaya sana huyu msichana? Kwani mimba ni ya mwanamke, na mle ndani ni mtoto, na hii mimba hakuichukuwa kwa mke mwenzake, aliyeiweka mimba ni mwanamume. Na hii mimba si mwisho wa maisha ni mwanzo wa maisha. Yule mtoto atakayezaliwa akifika umri wa kwenda shule, anapeleka shuleni anapokelewa. Mama yake amefukuzwa hakupata hata elimu ya ngumbaru. Wazazi wenzangu pamoja na viongozi, hili neno lifikirieni. Sisemi wazidi kufanya mimba na sisemi wafukuzwe, kwa maana mimba ni mtoto ndani na mtoto huyo akizaliwa anataka kulelewa. Tukimfukuza huyo kijana, ni ubaya gani aliyofanya, hii ni accident, hakupanga yeye.

Hiyo mimba ya shule ni accident, hakutaka mimba na yule mwenye kuiweka hiyo mimba hamtaki naye, halafu anafukuzwa huyo

msichana maskini anaenda na kulia, mvulana anaendelea na masomo. Huko juu hafukuzwi, anafanyiwa mipango ajifungue nyumbani, achukue katoto ampe mama yake, afunge kitambara cha kichwa ashike vitabu aende shule. Kesho ndio ma-D.C. tunamletea D.C. mwanamke ana watoto. Huko nyumbani ana watoto na hapa kwetu mpaka mtoto afukuzwe, yule amepatia mimba kwa bahati mbaya, msichana amekuwa kama mwana jeshi. Kwa vile maji yamejaa, anatafuta awe mwana na arudishe usichana usichana, anaenda kupata wengine waalimu, madaktari anapatiwa hizo tembe zinazoitwa vidonge, anakula kidonge ili aurudie usichana wake anapoteza maisha, anakufa. Mimi ninasema hivi, maoni yangu, huyu msichana akipatwa na accident hii, akae nyumbani kitambo kile cha siku za kujifungua, akijifungua arudi shule. Maana huo ni mwanzo wamaisha imejulikana kwamba ndani ana mtoto, na sidhani kama sisi tulio hapa kuna mtu mmoja anataka mwanamke asiyezaa. Hapa kuna mwananamume anataka mwanamke asiyezaa? Wangapi wanataka mwanamke azaaye? Wangapi! Sasa huyu msichana anafukuzwa kwa nini? Basi hayo ni maneneo ambayo sijui na hiyo katiba itachukuwa aje, lakini watoto, wanawake wikipatwa na accident hiyo wasichukuliwe kama wanyama, hao ni binadamu. Na hiyo ndiyo kazi ya Mungu alimpa mwanamke azae na ni kazi yake kabisa kabisa hiyo, hawezi kuikata na anayeweka mimba ni wewe unayemfukuza. Basi nina mengi ya kuzungumza, lakini wakati hauniruhusu.

Nina sema hivi; Katiba ya Kenya inayokuja iwe ya majimbo. Mimi ni mmoja kati ya wale waliopigania uhuru na marehemu Ngala. Nimefuatana na yeye ana kwa ana, nimeona mengi mpaka wakati huu hatujaona uhuru ukifanya kazi hapa kwetu pwani, tunaona tumemuondoa mkoloni. Ngala alisema “tunamuondoa mkoloni mweupe atakuja mkoloni mweusi,” na sasa yule mkoloni ana siri, yeye ana fanana na kale kanyama kanakoitwa Kabwiramainzi. Ukikangalia ni kama inzi, na kumbe si inzi, kanashika yule inzi kanampiga misumari, inzi inakwisha. Sasa huyu mkoloni mweusi ni kama wewe vile ulivyo na kama mimi, ni rafiki yangu ndiyo hana nywele za singa. Nywele zake na zangu ni sawa, lakini ujue yeye ni kabwiramainzi. Tunataka serikali yetu ile ile ya kidemokrasia, na ya majimbo ili Pwani isigawanyiwe watu walio juu huko. Ardhi ya Kenya kila mahali kuna watu wake. Sasa kutoka mamburui mpaka huku, watu wanasumbuliwa sumbuliwa, kutoka Marereni, hiyo Marereni ndiyo mimi imenikasirisha sana. Imepatiwa mtu kule aliyestaafu, anachimba ule waya wakurithi, shimo kubwa ambalo mbuzi akiingia kule anakufa. Wewe binadamu ukienda ukiingia usiku pale unavunjika vunjika, na kumbe anafanya hivyo halafu azuie wahindi aondoke. Kenya ni moja, lakini mbona mnataka na mafuta yetu? Basi asanteni...Wewe Commissioner, ata kama umestaafu ukitaka kupatiwa ardhi, patiwa huko kwenu. Kwani huko hakuna ardhi ya kupatiwa mtu huko, ardhi zote ni Pwani, Beach plot, mnachukua Beach plot nyinyi sisi, basi nashukuru kwa hivyo hata nakupatia salute.

Com. Riunga: Asante sana mzee kwa hayo mawaidha yako na maoni pia. David Karisa eeh Charo Masaa, (AUDIENCE: Masha), Robert Kahindi...ni wewe Bwana....Stephen Kalama, Shauri Peter,Dickens Elweya, Alfred Wasike, Raymond Ngala, Sakophagas Zablon, Bajira Reuben, Kazungu Joseph, Evans Karisa, John Kaindi, Joseph Nzai, Maua (something) Shuu... amakunaye anajua mwenye hilo jina? Francis Ngala, Bwana Furaha Mumba, Joseph Katana, Anthony Mwang'ombe....ako...Safari Katana, Elisha Mzungu, Ali Bora, Elina Ali Bakari, Mohammed Omar, Omar Ali, Kassim Muungaza....karibu basi.

Kassim Muungaza: Kwa majina naitwa Kassim Muungaza, mkaaji wa Marerani. Mengine yameongewa, mengine yamepitiwa kwa redio, kwa magazeti na hata kwa vikundi vya watu. Miminitagusia huenda pengine yale wengine wamesikia kwa redio haya mambo ya equality/usawa. Usawa baina ya wanawake na wanaume ni kitu ambacho kimeleta sasa mzozo mwingine ambao baada ya miaka kumi ijayo au mia moja ijayo itakuja kuleta taabu. Usawa, wanawake wanapigania usawa, usawa gani?

Hicho ni kitu lazima wafikirie. Katiba ya nyumba, tayari ilipangwa na Mungu. Ukisoma Genesis 2:28, mwanamke hakuumbwa awe mpinzani wa mwanaume. Lakini sasa wanawake wamegeuka na kuwa wapinzani. Kile kitu lazima wanalie na kama itapitishwa kuwa na iwe hivyo miaka kumi ijayo ama mia moja ijayo, wanaume mtakuwa barabarani mkifanya maandamano. Tunatengeneza kitu kinaitwa sheria. Nani atafuata hii sheria na nani atatekeleza hii sheria na nani atakuwa anaongoza hii sheria. Katika nyumba, kuna baba, mama, mtoto, kama sote tuko sawa, mimi nalaumu bunge la nane saa hii kwa vile linatoa hoja zingine ama sheria zingine ambazo zinaharibu nchi. Kwa mfano, walisema, “Don’t whip a child” – usipige mtoto. Shuleni hakuna mtoto hachapwi, mumeona matokeo. Kuna mashule yamechomwa kwa ajili ya maneneo kama hayo, lakini wakati kiboko kilikuweco nidhani ilikuwa ya hali ya juu. Bunge la nane lazima liangaliwe, kama kwenda kupitisha hoja, lazima hiyo hoja iwe ni hoja ya kusaidia mwananchi, sio ya kubomoa. Tumekuja, tumeangalia kitu kinaitwa “wamefika pahali”, hii sasa tunarudi upande w wanawake, wamechukua ule uongozi au ile mapenzi yenye wako nayo katika nyumba wanaipeleka katika uongozi. Mwanamke anaweza kuongea ama kupendekeza kitu kwa yaani kwa kujinyenyekea kwake ama kulia kuwa kuonyesha kuwa kweli hunipendi ama hunipendi nifanyeje na ndio unaona ati wanawake wafanye namna gani wajengewe vitu kuwa watakuwa wanafanya namna gani watakuja kupewa vile viti. Hii kitu wachunguze sana kwa vile, nikichukua mfano, kuna waziri mmoja katika kenya hii, Mbunge wa East Africa, ilikuwa imetengewa kiti ya mwanamke, alichukua katika nyumba yake mwenyewe bibi yake na akamweka hapo. Kama hii kiti inakuja kusema tunatenga vya wanawake hata kama mimi mutanipa huo uongozi nitachukua bibi yangu au rafiki yangu. Wanawake ni wapigania, si watengewe.

Mambo ya raisi iko juu zaidi. Leo ameteua huyu kesho amemfuta, tena kwa, na ifanyikwe hivyo hivyo, ile mambo yake ipunguzwe.

Tukij upande wa Judiciary, mambo ya kotini, kuna sheria zingine enya hata machama ile ya juu haiwezi kutatua. Kuna ile mahakama ya zamani, ile mahakama ya wazee. Kesi ikishindikana huko na mtu aombe anataka mahakama ili hiyo kesi yake isikilizwe, kesia nyumbani. Kuna ile kitu kinaitwa pengine kiapo kale kama, hata kuwe na mamilioni yenye nimeunga huko ati pengine wanidhulumu kiapo hakijui. Sasa cases zingine lazima ziangaliwe na zirudishwe nyumbani.

Mambo ya domestic corruption – mambo ya kinyumba – mambo ya kukosana kinyumba. Cases za kukosanakinyumba zirudishwe katika Chief. Chief ndiye anaweza kujua mimi ninatembea namna gani ama hufanya namna gani ama bibi yangu, lakini sa hii nikimchapa bibi yangu kofi anakimbia kwa Coporal. Coporal pengine huenda kumwalia bibi yangu pengine vile anavaa ama vile yuko. Mimi ataniambia angalia kirauni usiangalie mambo mengine angalia kirauni. Sasa huko mbele ninashtakiwa kuwa assault. Tiari tumevunja nyumba, watoto wanateseka, machokora wanazidi. Hii mambo ya domestic corruption ni nini, tutairudisha katika kwa Chief. Chief apewe mamlaka ya nyumbani sio ipelekwe kotini.

Kuna kitu kinaitwa... eh... serikali waangalie kitu...eeh...mzee kuazia miaka sixty (60) sitini kuenda mbele, wale watu sasa hawajiwezi, hao watu wataangaliwa namna gani? Kama ni katiba ipangwe kuwa mtu akifikia miaka sitini awe pengine kuna sehemu atakuwa akipata ili yakumlinda.

Na mambo ya masomo mtoto akifika miaka mitatu ama mitano, awe Nursery school mpaka secondary school iwe free.

Mambo ya hospitali – Mambo ya cost sharing. Cost sharing imeumiza wananchi jamani. Katiba mwangalie mambo ya cost sharing hiyo muondoe. Kama serikali ni kugharamia mambo ya hospitali waangalie watu wao watakaa namna gani. Lakini sasa mama akienda huko hajiwezi hata shilingi tano mfukoni, wnamwambia alete shilingi mia moja pengine ndio jina iandikwe hapo. Cost sharing iondolewe, serikali ndiojue watu wake wanaka namna gani. Kuna mengi ambayo yanaweza kuongewa lakini time nazo ndizo mbaya.

Com. Riunga: Asante sana, jiandikishe hapo. Sasa bahati Shuba, Abdi Hussein, Isaac Manyasi...karibu.

Speaker: Nashukuru sana, kwa majina naitwa Isaac Manyasi Kiketi na kwa niaba ya Commissioner pamoja na mama tunakushukuru kwa kufika hapa Pwani kuchukua mawaidha au mapendekezo kuhusu katiba. Nasema vile munazungumzia kuhusu katiba nyinyi wenyewe mumetuletea vitabu, mumetuandikia maneneo ambayo mumetultea. Haya, mumetuuliza kwamba katiba ni ninin. Hawa wananchi wote sidhani kama wamefundishwa mambo ya katiba ni nini na munatuuliza halafu munatuletea hii kiapo ya kutunga katiba. Itakuwa aje hii? Hii ni kutupoteza akili sisi watu wa Pwani sio kutengeneza. Hata tukiimba majimbo, haitatufaa kwa sababu inamalizika hapa hapa mitini.

Jambo la kwanza, angalia tuseme serikali yetu, ilifanya nini tangu uongozi, angalia iko wapi? Kitu inaitwa shilini imeandikwa juu hapa kwa kirauni. Kirauni imerudihini, ama urongo? Chukua shilingi uangalie. Pesa ziko juu, kazi iko chini, urong? Kwa hivyo kama serikali inataka kutengeneza katiba ifikirie hilo jambo.

La pili, katika serikali yetu ungeliona yoyote hata kama shilingi moja hata ishiini, angalia shilingi inawekwa juu ihirini iko juu, kirauni iko chini. Hakuna haki iko kwa mwananchi...hakuna haki, jaki gani? Sasa kila kazi tunafanyia kwanza nio upate ila kupata shilingi ndio hapati.

Cha pili, katika serikali yetu imechukua siku hizi baada ya kuchukua vijana kuwapa kazi, hata wengine hawajiwezi. Anaenda kuchukua mtoto ambaye hata chongo ukiangalia katika mapolisi hata AP ilikuwa mtu anaangaliwa sawa sawa, lakini ukiangalia hata askari anakaa hivi (demonstrating) kwa sababu ya nini? Ya ile shilingi iko juu, kirauni ichini imekanyagwa. Sheria gani hii? Haya ukiangalia upande wa ulinzi kama polisi; siku hizi nikichukua mali yangu, natua hapa magari nipleke hapa Malindi, natoa hapa Marereni nipeleke Malindi, hapa nimesimamishwa na gunia moja tu hapana mbili...ananiambia simama, hii ni nini? Makaa,

unapeleka wapi? Aah yangu yakupikia tu hapa Malindi, aha, haiwezekani, weka hapa hini...wapi permit... sasa kitu kidogo hivi? Haya, serikali angalieni. Mapolisi kwanza hiyo wizara, ifutwe yote kabisa kaika serikali. Iweke kando, alafu, utafute serikali ijayo kama mwataka kuunda, ianze kwa Local government ndio tutapata serikali tunataka ya majimbo. Na majimbo tutambue itakuja kwa njia gani na tutafanya namna gani ili tuweze kujilinda sisi na watoto wetu ama vizazai vyetu vitakuaje mbele.

Tuangali sheria kwanza. Tushinde majimbo lakini hatuangaliimbele. Hapo 1963, mzee Kenyatta alisema hivi, “angalia ile iti, kale kanyoni kamnguka pal, bado tukaangalia juu ya mti.

Com. Riunga: Kanyoni ni nini?

Speaker: Hujui kanyoni ni nini...ni ndege. Ndege imeanguka juu ya miti., ilipoanguka juu ya miti akasema kula ile mali lakini chungu,”...akaweka hiyo sheria. Mnaona siku hizi mabnki inavunjwa. Mabnki ikifungwa hii ni kuvunja benki, si unaona wezi wamezidi, wanavunja mabnki, wanafanya ni jiwe hapa, kula lakini unajua. Hapa Pwani sisi hatujui kuiba, atujui kufaya lolote. Tukichukua ile miti ndio maua, ndio kahawa, ndio ngano, ndio mahindi, ndio majani hai, ndio miwa hiyo miti... na ukifika hapa nayo miti umeleta nje nikauzie hapa Kongoni wanakuonyeshakidole. Enda nairobi saa hii, Headquarter uon kama vile watu wanalewa. Enda Kisumu saa hii hata jana imetangazwa kwa redio., club imepewa license...kwa redio...ama redio inasema uongo niseme kweli. Enda Bungoma, watu wanalewa kawaida. Lakini hapa kwa ile miti, hauna uhuru kabisa hapa Pwani hata tukiiba miaka mia ijayo...hakuna...asante.

Com. Riunga: Asante sana mzee...eeh...Omar .K. Fondo...Karibu.

Speaker: Kwa jina naitwa Omar .K. Fondo na nakushukuru sana Bwana Commissioner kwa kututembelea na kutelimisha kama mliyvo eleza kwenye kitabu chenye. Mimi yangu si mengi, ni machache sana maana mengi yameshazungumzwa yote. Lakini kitu ambacho utaweza wewe mwenyewe kukitilia maanani ni kil ambacho kimezungumzwa mara kwa mara na watu watakuja kuzungumza hicho hicho.

Mimi nazungumza kanza kuhusu majimbo tuitakayo. Pili,majimbo ya kwamba vile tuitakayo, sio kwamba tunataka majimbo basi tuwe tuna utngano – huyu ndiye aende kwao, la. Sisi tushachanganyikana, kwa hivyo hatuwezi kuwa na utengano wa namna hiyo. Tunataka majimbo tuwe tunajiangalilia mambo yetu sisi wenyewe.

Pili, nakuja mahali pa elimu. Elimu ingewezekana ingekuwa kama pale zamani. Watoto walikuwa wanapata elimu nzuri kutoka standard one mpaka form six, ikaja ikafupishwa, baada ya kufupishwa hlafulu kazi zikapunguzwa sasa elimu ilifupishwa halafu watoto wakamalizwa kwa uwingi halafu kazi nazo hazipatikani kwa uwingi. Sasa ni shida ambapo watoto wangeendelea mpaka form six, ingekuwa sasa huku kuna miradi mngine matajiri wanatengeneza mipango ya kikazi watoto wakimaliza skuli

wanapata kuajiriwa.

Jambo lingine ambalo niliona kwa macho yangu na nikaliona hilo kweli na hata nikajiuliza kama kweli sisi hapa gongo hii tuko Kenya kweli? Hapa chini hapa, watu wanaumia vibaya, ukisikia futi Bwana Commissioner usifikirie ni futi kama ya hapa ni gogngo mpaka kule nahesabiwa ni futi moja hiyo, mtu analipa sijui shilingi mia mbili. Hiyomia mbili hata akivuka hiyo gate imekwisha hiyo, je hukonyumbani atapeleka nini? Na labou yuko hapa Malindi hapa na hawafiki hapa na basi kama hawafiki wanaambiwa nyinyi msije kule sisi tutaonana mahali fulani na ni hiyo tu inayofanyika hiyo ni kama kuwadhulumu. Wanadhulumuwa vibaya akina mama.

Tukitoka hapo tunakuja upande wa ardhi...hata mimi nasem kweli, hata ikawa hiyo serikali inasema huku hakuna watu ni kwanini mtu anakuja hapa anasema hapa hakuna watu kwa nini huwezi ukasema tutakupa mtu wetu sisi akaangalie hapo, kama hakuna watu sisi tutakuja kukupuuzia aha anandikiwa tu, hapo mtu akija hapo kuna watu ana vijukuu na vitukuu, anaambiwa wewe hapa si pako hapa. Usipokubali kufa hapa utafia wapi sasa. Mtu anavitukuu pale yeye anaambiwa hapo si pake sasa aaa... mimi katika katiba hii ambayo itakuja ambayo mnaitafuta kwa sisi raia, ikiwezekana ningetaka hii mambo ya ardhi iangaliwe sana hiyo. Hakuna ruhusa ya mtu kuuziwa kitu kwa kuwa ameka pale kumbe nasema hakuna mtu kumbe kuna watu walioko a wameshazaana na wakazaana. Hapo mahali lazima pawe panaangaliwa mpaka pajulikane kweli hapa pahali hapana watu. Sio mtu kutoka kule na karatasi, tutakuja sema bsi wewe kaa na karatasi na mimi miwache hapa hapa nilipo au sivyo haki ni kufa ndio nijue huko namna gani.

La nne, Bwana Commissioner tunasema uchumi hapana hakuna. Kwa nini Bwana D.O. kama serikali ingetoa matinga kumi, wale ambao hawana pesa, nendeni kwa Bwana D.O. mukajiandikishe baada ya mazao hilo tinga utakatiwa mazao yako hapo, hiyo ni chakula ingepatikana kwa uwingi ajabu, uchumi ungekuwa uko juu zaidi. Sasa kajembe kale, mkifanya kiangaza siku mbili tatu, hapalimiki, halafu munasema uchumi urudi, uchumi umerudi chini kwa sababu chakula hakipatikani. Nina mengi lakini mengi yashazungumzwa na ule wakati ingegfaa niwe wa kwanza ningeona raha sana. Pale ningechukua nusu saa lakini hivi sasa naona hata hivyo naona hata hivi sasa waona nakucheleweshwa. Kwa hivyo nasema asante sana.

Com. Riunga: Asante Bwana Fondoeh hiyo imeandikwa Michole Kimani, Joseph Kariuki, Emmanuel Mbulishi....Karibu.

Speaker: Bwana Commissioner, kwa majina naitwa Emmanuel Ngumbao Mbulushi na mimi nimkaazi wa hapa Gongoni. Katika marekebisho ya katiba, ningetaka kugusia vifungu vifuatavyo;

Kwanza, sheria inzomiliki ardhi hapa nchini Kenya ni mbovu na ambazo kwanza zimepitwa na wakati. Kwa hivyo mamlaka ya kutoa stakabadhi za kumiliki mashamba ningependekeza kwamba zitolewe kutoka kwa Commissioner of Lands na zirudishwe kwa mabaraza ya wilaya. Kuweko katika kila wilaya Commissioner wa adhi ambaye kwayo atawajibika kwa CountyCouncil na hapo iwe ndio stage ya mwisho ya kupatia stakabadhi za kumiliki mashamba.

Kuhusu Local Authority Mr. Commissioner, Sir, kuna mambo ya kuhuzunisha kuhusu baadhi ya mabaraza ya wilaya hapa nchini. Kwayo, kwamba wananchi wamewachagua madiwani wapatao sitini katika baraza lile na hakuna diwani anayewea kusoma angalau mstari mmoja kwa lughe ya kimombo. Kwa hivyo ningependekeza kwamba, kuanzia kwa katiba mpya, madiwani wawe na kisomo cha angalau elimu ya kidato cha nne, mwenye third division na kwenda juu. Machairmen na Mayors wa mabaraza pia nao wawe na kiwango cha O level na wachaguliwe moja kwa moja na wananchi wenyewe, Universal Sapharage na wa serve kipindi cha miaka mitano peke yake.

Case act bwana Commissioner, ningependa, ku-propose marekebisho yafuatayo. Kwanza ofisi ya Assistant Chief isiweko, iondoke, ibaki ofisi ya Chief na Chief naye aripoti moja kwa moja kwa District Commissioner, Bwana District officer aondoke katika katiba mpya. Ofisi ya Provincial Commissioner yaani P.C. ibadilishwe na kuweko Governor atakayechaguliwa na wananchi wenyewe moja kwa moja kutoka mashinani. Huyu ndiye atakayekuwa mwakilishi mkuu katika jimbo.

Kuhusu elimu, ningependekeza kwamba syllabus za schools kuanzia darasa la nne mpaka kiwango cha University level yawekwe na iwe ni lazima kwenye katiba kwamba masomo haya mawili ninayopendekeza yafundishwe; Sheria-yani law na economics. Yafundishwe kutoka arasa la nne mpaka chuo kikuu, kwa sababu kutofahamu sisi sheria ndio imekuwa chanzo cha sisi kugandamizwa na kuketiwa na kunyanyaswa kwa sababu kipenge hiki, kipenge hiki, hii inaletwa na kutojua kwa hivyo tukianza kufundishwa sheria na uchumi hakuna mtu atatuambia uchumi umeenda hivi, umeenda vile, so yeye anapata msaada kwa haraka iwezekanavyo. Muundo wa serikali wa hivi sasa unasababisha sana kwa kiwango kikubwa ufisadi, kwa mfano, barabara zote zinaelekea Nairobi, kwa sababu huko Nairobi ndiko ambako huduma zote za wizara zote za serikali zinapatikana. Hivyo kila ushao watumishi wa uma wanatumia pesa nyingi kabisa za serikali kusafiri Nairobi li wakapate huduma huko. Hata hawa ma-commissioner ambao wako hapa hivi sasa baadaye watatumia pesa nyingi zetu kusafiri kwenda Nairobi kufuata huduma. Je, kama tungepata serikali ya majimbo, kila jimbo lingekuwa liko karibu na mwananchi badala ya kusafiri kwenda Nairobi kutafuta huduma yoyote wanasafiri tu mwendo wa kama kilomita moja mbili wanafika katika ile ofisi ambayo wanataka na huduma inapatikana kwa mwananchi. Watumishi wengi sana wauma wanatumia pesa nyingi wa kutafuta huduma Nairobi. Kama tungekuwa na serikali ya majimbo kungekuwa na majimbo hapa karibu, serikali ingekuwa karibu na sisi na serikali hiyo ya majimbo ina ma-governor ambao wana mabunge yao, mawaziriambao wana wizara mbali mbali na raisi pia ambaye yuko juu anaangalia kazi za wale ma-governor wanaohusika na elimu, ukulima, matibabu na mambo yote kamilifu. Hivyo, mwananchi yuko karibu abisa na serikali yake anapotafuta msaada wowote anaupata bila kupoteza pesa nyingi za kwenda huko Nairobi.

Umaskini unaongezwa na huu muundo wetu wa serikali kwa sababu mamilioni mengi ya pesa yanatumika kwa usafiri wa watumishi wa umma kwenda Nairobi, na wananchi wa kawaida kwenda Nairobi ili kufuata huduma huko. Je, kama huduma hizo zingekuwa karibu na sisi? Katika serikali hii ya majimbo tungepunguza gharama hizo, pengine pesa hizo tukazitumia kwa mambo mengine kuboresha maisha yetu.

Sehemu yingine ningetaka kuikazia mkazo ni haki za ardhi na mali. Wenzangu wamekwisha taja sehemu hiyo lakini ningetaka kuongeza kwamba katika haki ya ardhi na mali, ningetaka kuunga mkono kwamba mwananchi apewe haki ya kumiliki arhi, mgeni apewe lease tu ya kutumia adhi fulani kwa muda kisha baadaye ikiwa lazima aendelee anakwenda anaandikisha tena muda ambao anataka, lakini sio kupewa haki moja kwa moja amiliki na huku mwenyeji hana ardhi. Hii ni dhuluma, ikiwa ni kuwapatia haki ya kumiliki ardhi wageni basi nchi yetu ya Kenya itamalizwa na hawa wageni na sisi wenyeji tutakosa ardhi.

Pia ningetaka kuongeza wamba mwanamke apewe haki, kuwe na ofisi maalum ambako mwanamke anaweza kudai urathi / urithi wake iwapo anaona anadhulumiwa. Ningetaka kueleza hapa kidogo, hapa ninapendekeza kuwa katiba yetu iusajili ndoa zote hata kama watu wataoana huko ndani ni lazima wahakikishe kwamba ndoa yao imesajiliwa na serikali ili wakati wowote ule malalamishi ya urithi yanapoletwa, iwe rahisi kuangalia tatizo hilo lakulisuhulisha ilitujuwe ni nani ambaye ana stahili kupata urithi gani na ni kitu gani.

Pia kwa sababu hapa ninaona kwamba kuna mkabila mengi sana ambao wanawadhulumu wanawake. Wanawake wengi sana hawapati urithi. Urithi unakwenda kwa wanaume pekeyao na wanawake wanaachwa hapo kando. Ingekuwa bora kila mtu hata mwanamke pia apewe haki ya kurithi. Pengine ndoa zinaposajiliwa sehemu hii ingekuwa rahisi kabisa kuishughulikia kwa sababu watu wanapo oana bila kusajiliwa si rahisi kuamua kwamba urithi huu huyu mwanamke anatakikana kupata urithi kadhaa na huyu urithi kadhaa, si rahisi. Lakini ndoa zinaposajiliwa kila ndoa iwapo mume amekubali kuoa mwanamke fulani, iwapo mwanamke amekubali kuolewa na mwanamume fulani wahakikishe ndoa yao imesajiliwa ili kunapotokea matatizo ya urithi yaw yanaweza kushughulikiwa vizuri.

Hapa kuna sehemu fulani ya urithi wa watoto. Mtoto pengine hajafika umri wa kudai haki yake na ikiwa hakuna ofisi maalum ya kusajili ndoa, watoto kama hawa ambao wanatakikiana kurithi mali kutoka kwa wazazi wao pengine wamefariki hawatajulikana kwa urahisi na itakuwa dhuluma. Hivyo, ndoa zikisajiliwa itakuwa rahisi hata mtoto mdogo ambaye ni miaka miwiwli ambaye babake au wazazi wake wamefariki atakuwa anajulikana kwa maandishi na baadaye akawa miaka kumi anaweza kudai urithi wake.

Pia ningetaka kusema kidogo juu ya mahakama. Mwenzangu amesema kuwa ni lazima somo la sheria lifunishwe shuleni, nami ninaunga mkono. Somo la sheria ni lazima lifunishwe mashuleni ili kila mwananchi ajue haki yak. Waamerika, juzi nilizungumza na mwamerika mmoja akasema kwamba kule kwetu huwezi kuingia nyumbani mwa mtu ati kwa sababu yeye ni askai. Ni lazima atoe kitambulisho au sivyo atafukuzwa nje, kwa sababu kila mwananchi anajua haki yake, anajua kionewa na askari yeyote yeye anajua sheria lakini huku sivyo. Askari akiingia hata pengine ni jambazi, sisi tunatetemeka, kwa sababu hatujui sheria. Ni wakati sasa wakuhakikisha kwamba katiba teu ina weka mkazo fundisho la sheria katika kila shule ili kila mmoja ajue sheria na ajue haki yake. Si ajabu kuona mtu anaonewa katika mahakama kwa sababu hajui sheria na ni lazima hii ni haki ya mwananchi kwamba ajue haki zake. Kwa hivyo ninamaliza nikitia mkazo kwamba hili somo la sheria lifundishwe iwe ni lazima

lifundishwe mashuleni. Kwa wakati huu ambapo bado halijafundishwa mashuleni ningependekeza ya kwamba, mawakili wa serikali wawasaidie wale washtakiwa katika mahakama kwa sababu kuna washtakiwa wengine ambao wanaadhibiwa kidhuluma. Pegin hawajui kujitetea mahakamani, na wakitafuta msaada wa wakili wa kujitegemea wanalipishwa pesa nyingi sana ambazo hawezi kuzitoa na hi ni huluma na kwa serikali si vizuri kumwona mwananchi wake akihulumiwa kiasi hicho. Kwa hivyo kabla hili somo la sheria halijafundishwa shuleni, ningependa kuwe na wakili wa kiserikali ambaye hata kama atatutoza sisi lkini kwa bei ambayo inawezekana ili kila mmoja anayeshtakiwa mahakamani apate wakati, mzuri wa kujieleza na hata kama ni adhabu apate ile adhabu ambayo ni ya haki. Asante sana.

Asant sana Bwana Kenga.....eeh....Kaungu Kombe,Dickson Kaindi, Anderson Mbaya, Kazungu Mbaya, Gumbao Katana Karissa charo, Barak Kiwaya, Mwangi Luganzi, Kazungu Karissa, Bajira Bashora, Zoya, Peter Mueni, Abdala salim...hapana mwingine anaitwa hivyo...karibu bwana.

Speaker: Mimi ningependa katiba hii

Com Riunga: Jina lako kwanza

Speaker: Jina langu mimi naitwa Toya Iha . Ningetaka katiba hii itusaidie kulingana na uchumi wetu vile na malipo ytu tulioko tunalipwa huku. Katika viwanda hivi vya chumvi tunafanya kazi lakini hatulipwi malipo kulingana na vile tunataka. Unakuta mtu anafanya futi moja unalipwa mia mbili na arobaini kuliko wale wengine, yaani haistahili alipwe mia mbili arobaini kule kwa tani moja maaana ile taimoja wao anapata pesa nyingi na sisi hatupati zil pesa ambazo tunataka na ukiongea namna hiyo inakuwa wew ni mbaya mpaka unafukuzwa kwa kibarua.

Na jambo lingine tunaendelea kunyanyaswa vile vile. Unakuta wewe huna mamlaka yoyote ya kuweza kuongea mbele ya atu kama wale wewe wamekuajiri ile kibarua....

Com. Riunga: Endelea

Speaker: Mimi sina mengi ni hayo machache.

Com. Riunga: Okay, asante sana....Abdala Salim, Katana Kenga, Mansur Mohamed, Jonathan mangi, Daniel Klondo, Samson Mungela, Kazo Kombe, Agnes Zawadi, Joseph Putokosi, Patrick Kiti, Samwel Nzai, Bonface kazungu, Salabu Kirani, kadenge Ponda, Smwel Katana, Naser saidi, Fkiri Kenga, chalo Keya, Samson Radu

Audience: ako

Com. Riunga: Karibu...hawa watu wamehepa?

Speaker: Kwa majina yangu Samson Radu mkaaji wa Garite hapa chini. Twashukuru sana wageni nyinyi ambao mumekuja kutupendekeza na tupendekeza marekebishohaya. Kwa hakika ni wengi ambao wamepata kunena malalamishi yote ya serikali yetu hii, tumeipenda sana miaka mingi lakini yenyewe haitupendi raia...haitupendi...haitupendi kwa hii...kwa sababu tulikuwa tukitangaziwe ya kwamba Kenya hii ni Kenya huru, lakini sasa uhuru wetu uko wapi...uhuru wetu hatuoni. Maanake uhuru, nikiwa nipata ardhi ambapo nimelelewa pale na nimekaa pale na nimezaa pia, nikiomba kibadhi sipati kabla mahali pakutoa kibadhi hakipatikani, ni jambo la kwanza. Vibali tumelia miaka mingi, tumekuja tukapasuliwa mashamba yetu yote, lakini kibali ni ngumu...tunaambiwa tuende Nairobi tutapata kialii. Ni tikiti, Nairobi hatukujui, tutapita wapi ndio tukapate kibali. Muda mfupi tunaambiwa hapo ulipe ni kwa mkuu fulani kutoka Nairobi mtakuja kutolewa na malinga hapa na hata kwa sasa tunangoja malinga yatakuja...maanaka yatakuja. Wapendwa serikali huru iko wapi?

Com. Riunga: Tafadhali tuwapatie nafasi na tuwaheshimu wale wanazungumza...asante.

Speaker: Tunaomba kama hii katiba inaweza kuendelea na tukapata kupendekeza hiki chama chetu tunachokiomba sasa ndicho kipate kuingia. Tukione nacho kama kitatufanyia kitu gani. Maanake serikali yetu ya kajogoro imetunyanyasa siku nyingi sana. Tazama sasa kwa wakati huu ambapo Pwani hii kutoka Kilifi mpaka huko muti tunayotgemea hapa kapaya Pwani si mnazi pekee yake. Lakini sasa mnazi ni wa serikali tu ndio wanakula sasa badla ya mkilima Serikali inaweza kakula hiyo mnazi, abapo yeye amekuja akiwa anataka kukuwa kama msaidizi wakusaidia watu wa hapa amekuwa mlaji sasa anakula hiyo nazi ya raia. Maanake akikut umeegema hapo juu, ukishuka chini na hiyo pomb, mar moja uitoe pesa. Mkirudi ndio atakuja kuichukua hiyo pombe kupeleka kusudi kesho aje na pesa, hiyo naye atanda kushikwa hapo njiani, na hayo akishikwa akienda kule kwa Chifu hutayakuta yakimwagwa, na hiyo ni sumu haruhusiwi iuzwe, kwa nini haionekani imemwagwa, inapelekwa wapi? Inapelekwa wapi? Tazameni sana serikali yetu ya kajogoro inasema ya kwamba, ukiwa wewe ni mgema hivi nivyo sema hapa, leo nimepeleka shilingi mia mbili ofisini, ofisi ya polisi kusudi wasije wakasumbua wagama wangu nyumbani. Usipo fanya hiyo, mtoto wako hatakula, baba yako ambaye hajiwezi hatakula kwa sababu umelima hiyo ukiju kwamba watoto utawalea na hii. Sa fanya uwe na serikali, serikali gani? Uhuru gani uko hapa sasa? Tunaomba uju uhuru wetu ni nini, twende tukavunje maduka tuigwe marisasi? Ama twende tukavunje mabenki tunyongwe? Nimetegemea mnazi pek yake, ni kw nini serikali imandikwa nani pesa analipwa? Ni kwanini hakuja kunichaji pesa mimi maskini ambaye sina kitu? Hiyo mpango iondolewe na ikiwa ni kama mapolisi, ikiwa hiyo ndio itakuwa sheria, hiyo sheria itolewe. Maanake hata Bwana D.O. yuko hapa. Ni kwanini hiyo ripoti, tunalia siku kucha, polisi wanakuja barabarani, sita ama saba wanakuija kusimama barabarani, unabeba nini pombe, pombe hii, huwezi kuondoka hapa, Ita shilingi mia tano, shilingi mia tano itafika wapi, tunataka kujua ofisi ya , ya hiyo mia tano inaingia wapi hapo. Hakuna ofisi inayoenda hiyo pesa. Nitchiliwa hapo, akifika hapa katikati waskari wako. Wewe unabeba nini? Pombe, hii pombe shilingi mia nane. Sina mia nane, twende. Akifika pale ile baiskeli shilingi elfu moja kutoka pale umebeba ile pombe, zile maboya zitabaki pale pale, kesho hutakuta mahali imenuka pombe imemwagwa pombe, imenda wapi? Inatafutiwa yule customer wao, wana ma-customer kamili hapa, anapewa hiyo usiku, usiku ananda kuuza pesa zinarudi kule.

Nani mla mnazi na baki bue, uhuru wetu uko wapi? Uhuru wetu uko wapi? Na mmi nina lima ikijua ya kwamba hii itanisaidia, watoto wangu wata soma kwa ajili ya ile mnazi. Saa hii serikali ina kuja kuninyemelea, tule pamoja na pahali kanusu acre moja tu, nusu ya acre ni mimi pamoja na serikali. Nikule, naikiwa sitafanya hivyo, wata kuja nyumbani na watakuja kunimbia nimepokea mgeni sasa hivi na baiskeli, nilimwekea pale, ile deskini itashikwa sasa na itaenda polisi na hitoki kule mpaka shillingi elfu moja, hata ikiwa ni kufunga ng'ombe, nitaeza kuchukuwa pombe ingine nifungwebaiskeli yangu nahiyo mgendi iende polisi. Tuko huru namna gani? Hii Kenya yetu kweli ni huru kweli ni? Hii ndio uhuru? Tunaomba katiba jamani. Hichi chama tunachokililia kila mmoja akisimama hapa anataja hiki chama, kije tena haraka, tukiaangalia kama hicho chama kinaweza utusaidia. Tuje kama hakiwezi kuja, tujuwe mnacho tu kiandika hapalagini hakitakuja mturuhisho tufanye nini pamoja na hawa watu, manake hao wameandikwa, wakiwa hawa wameandikwa wanalipwa pesa. Mimi ni mkulima hafatali mimi nimeandikwa ni mkulima. Mimi ni mkulima jembe, huchukuwa minazi miaka sita ndio unaaza kuzaa,zikiaanza kuzaa , tamaa yangu ni mgema atoe maji pale ampe mtu aende atengeneze mpango yake huko, kwini asikwe yule mlevi ambaye akili yake ni mbaya. Maanake wale wakubwa na wakwa,wakimaliza kazi wanaenda kuketi chini n kukunywa beer beer haiuweki siya kwaida kama pombe, yale ambaye uwatenda mabaya, aende akahukumwiwe yule ambaye matendo yake ni mazuri ni sawa. Na mimi nipate cha kulew yngu, nipte chochote ambacho n wez kuomesha mwangu, manake yani yote hii kutoka huko mpako huku ni mnazi tuu mpeke yake.wapendwa tutasema sana zaidi ni kwamba mjaribu sana kutuaangalia serikali jaribu sana kutuangualia,hii mpango ya hawa ma-askari wetu,wajao huku hata bwana D.O awapate kuwauwa hawa watu wakiwa kwa kiagara chenu,mjue hiki ni kiagari kibaya.Bwana D.O rekebisha watu wako,wanatumiza sisi raia wako.Bwana D.O hawa askari wako.Wanatumiza sana bwana D.O hawa watu.Wanatukaje kuja barabarani kiwa wewe hujui bwana D.O?Wawe wanatoka ofisi kwako hawa,baada ya siku mbili wanasimama barabarani wanakusanya wakinamama ambao hata wengine hana waume,wanafuga watoto wao,wanasomesha watoto wao kwa ajali ya boya.Anashikwa anatoa elfu tano juu ya boya moja,mia tano au mia sita atatoa ,atakula nini, watoto watasoma na kitu gani?Commissioner,hii mpango ya hiki chama tunacho kililia kije tunakiomba kwa sababu ya shida kama hizi kajogolo tumeibeleza siku nyingi lakini hakuna msada wowote tunaupata.Tunanyanyaswa ,utusaidie hii chama ije.Bwana D.O tusaidie,waskari wanatuonea,wanatuonea.Na hata wakija kwako nyumbani hakuna heshima

Hata kama umekaa na bibi yako utapigwa teke.Uhuru uko wapi?Nanataka uhuru uko wapi?Tukiwa tunatangaziwa Kenya uhuru ,uhuru uko wapi?Bwana D.O nakuomba,macommissioner wote ambao wamekuja hapa,hii marekebisho tujue polisi wetu wamebaki mdomo wazi zaidi,kwa sababu wao ndio wanakula mapesa na wakifika miazini wametajirika siku mbili akija akisimama hapa,hapa kribu ngomena hapa gongoni akiwa yeye ni mkubwa haki y Mungu utakuta tumbo tayari, sababu ya mapesa ya watu wa pombe, ikiwa ni pombe haitakwi ifutwe kabisa lakini ukiwa ni magendo pia tujue ya kwamba hawa watuwanatafutwa kwanini na wao anapokea na sisis tunategemeka hio. Na hayo ni mchache, Mungu awabariki.

Ningetaka kutangulia kwa jina ili nipate kuulikana, jina langu naitwa John Sulubu. Nimkaaji wa hapa Mpingoni. Mimi nataka ni-change maoni yangu ambayo ninayo. Nimesikia wengi wamechanga maoni mbayo hiyo nataka niseme na mimi. Langu la kwanza oni langu ningetaka katiba hii serikali ijayo iwe itakuwa serikali ya majimbo kwa sababu, kusema ule ukweli ni kwamba hakuna serikali nyingine ambayo unaweza kulta haki isipokuwa tu ni ya majimbo. Na ningetaka kutoa mfano mzuri sana ambapo kama ingewzekana mfano huu ningetaka hata kule ambako itaenda ah oh pia ungeandikwa. Baba akiwa na watoto kama saba na akawaoza na wakazaa, wamekuwa wala miji, hakuna haja baba yule awe na lazia ya kwamba wote walime hiyoshamba moja kwa sababu huo wa sasa wakati uliofika nikila mmoja ajiendeleze, yaani kuwe kutakuweko na kama ushindani katika haki za uchumi.Kwa hivyo kufikia sasa nataka niseme serikali ya Kenya. Kusema ul ukweili kila upande umekuwa na elimu. Huko juu kuna ek\limu, kwani kuna elimu hakuna haja ya kwamba lazima iwe itawekwa serikali moja na iwe ni moja. Hapana kusema ule ukweli kabisa ingegawanywa kwa majimbo ili kila jimbo likaweza kushindania jimbo lingin hivyo ingeweza kulta yaani hii Kenya ikawa ile inaita sijui ni umaskini ungeluweza kuondoka kwa sababu kusema ul ukweli, katika mimi siwezi kuzungumza mambo ya nje kwa sababu nimkaaji wa Pwani, kusema ukweli upande wa Pwani kuna mali nyingi sana, an]mbayo kama hiyo mali ilivyosemwa kama ikiwa serikali ni ya majimbo itakuweko na kama asilimia tuseme thamani na tano zitabaki hapa. Kusema ul ukweli uchumi hapo utaiionuka na hii ni kusema kwanba ukweli huu ukifanyika, hakuna hata zaidi ya miaka kumi utakuta hata mashambani pia kutakuwa na magorofa, kwa sababu kutakuweko na pesa zitakuweko zikizunguka hapa.

Shida ni kwamba serikali hii moj aiko hivi , mali zote nikizungumzia haswa mali ya Coast, zinapovunwa ukiwa ni Kilindini, Chumvini, kila kitu kinapelekwa huko juu, hatuna ndugu yetu, wale ni wale mimi nimaamini kusema ule ukweli hatuwezi kuendelea kinamna hiyo, sio kwamba tunakata, ama twataka ukabila, la. Lakini kusema ule ukweli kabisa, serikali ijayo, ingetaka ingewekwa vizuri yaani kuwa serikali ya amani, na ikiwa kweli serikali inahitaji kwamba umaskini uondoke, igegawanywa iwe majimbo, na isiwe majimbo ya kukataana kwa sababu sisi sote ni wakenya, ni ndugu lakini sivyo ilivofungwa hata Mungu amepanga hivyo. Mimi ikifika jioni nitakwenda kwangu nyumbani, na wewe utakwenda kwako nyumbani lakini kesho tutakutania hapa tuzungumze namna hiyo. Kwa hiyo majimbo haliwezi kupingwa kwa sababu ukiaangalia ule ukweli, ni mpango wa Mungu katiba Mungu ameanzisha majimbo,na kama ni lawama alaumiwe Mungu. Kwa hivyo nataka niseme serikali ijayo ikiwa itakuwa ya majimbo itakuwa na amani na italetu uchumi na maendeleo kwa kiola mija na ninataka niseme ikiwa hivyo hawa watu wote baada ya miaka michahe watatembea na magari na watakuwa matajiri kwa sababu kuna mli nyingi za potea kusema ukweli, ningetaka kuzungumza pia kutoa maoni kuhusu upande wa akina mama. Nimeona katika hali ya jinsi wakina mama wanvyo changa, nimesikia michango mingi sana, ningetaka kuchanga maoni yangu kwa serikali ijayo ama kwa katiba hii mpya. Kusema ule ukweli, serikali hii imekuwa ya kwanza kuleta ucha..uuu....yaani kama ni machokoraa serikali

imehusika kuleta uchokoraa. Nataka kueleza sababu ya kutosha, utakuta ziko kesi ambazo, kusema ule ukweli kama zingelizungumza kimijini, maanake hatuwezi kutaka vile Mungu alivyoanzisha. Nimesikia kutoka kwa mandugu wengine kuhusu habari za dini ya Kiislamu. Ukweli kabisa mambo ya nyumbani mwao, mambo ya kidini aachiwe ikakate mambo ya kulengana.

Mambo ya wanawake kama hiyo dini ina simamia hii mambo ya Mungu isiingiliwe maanake hiyo pia she...ni mpango ya Mungu. Sisi wananchi tupnge yetu tunayoyaweza lakini mambo ya Mungu tusiyavunje. Kama nilivyosikia kutoka kwa mnenaji mwingine kuna Genesis ambaye anaelezea kuhusu hatari za mwanamke, tangu na mwanzo Mungu akiumba watu wawili, tunamwona mwanake si kama Mungu alimwonea lakini alikuwa chini ya mwanaume, na siyo yakwamba ni dhambi, ni sio kwamba kusema hivyo ni kupiga wanawake, kwanza kaa na wale wanopiga wanawake ni vibaya sana kwa sababu kumpiga mwanamkw si njia nzuri. Hata mimi nataka kuchanga maoni serikali ijayo kuwa na katiba izungumzie kumpiga mwanamke si njia nzuri na mwanamume akimpiga mwanamke iwe hatia itakuweko achukuliwe lakini mwanamke kuwa chini ya mamlaka ya bwana, hiyo ni kawaida na hata akikataa basi nataka niseme labda tuseme hivi, katiba ijayo wanawake wasiolewe manake yale mahari uayolipiwa wewe bibi ndiye yanakufanya wewe under control, kwa hivyo hiyo nataka kuepuka kwamba yaani usije...sio kwamba uko chini huko chini. Lakini ukitaka kabisa, manake nimeona kuna vitu twanyanyaswa, twataka kuwa sawa na wanaume, hii haitawezekana. Maanake ukiangalia ukweli ni ya kwamba Mungu ameumba,amefanya ameshafanya na havezi badilisha. Mi sioni kwamba tungekasirikia Mungu kwa hivyo kitu ambacho ningetaka nitoe maoni kuhusu katiba ijayo kuhusu mambo ya wanawake ambayo ya nyumbani haswa. Haya mambo wale wakristomambo yangezungumziwa kule kanisani manake kuna sheria kule ambazo za mhukumu bibi na bwana na zinawaendesha na hasa mambo....mambo ya wale ambao hawana dini. Kuna ile mila na kusema ule ukweli nataka niseme, iko mila ya kukataliwa na iko mila lazima ikataliwe manake ukiaka wewe ndiwe utakaye rukaniwa mambo yako yatakuharibikia, manake wale sio kwamba walikosa elimu wakawa hawana, lakini utapata Mungu aliwatumia vizuri sana. Kwa hivyo sheria za kin mama haswa wale wasio na makanisa mila itumike kule na mila pia si mbaya manake utaikuta inafanya kitu kuwa kizuri na hivyo ingkuwa vizuri sana kwa sababu naona hayo madai yanaendelea. Basi baada ya miaka ijayo wanawake hawatakuwa ni kama wanaume hata watatoa maanake sala zikiwa nyingi zikiwaweza kumfunga mwanaumw au kumtesa, au kumtesa mwanamke, basi tatashika mardhi kwamba hakuna haja ya kuoja sasa, yaani tuishi tu. Mimi nataka niseme ingekuwa vizuri kwamba mambo ya katiba ijayo kuhusu mambo ya nyumbani ingeliwekwa, ingerudishwa kama ni makanisa ijadiliwe kimakanisani na kama ni kinyumbani...na kama ni...sijui watu ambao hawana makanisa lakini mila zinafanya kazi hiyo huko, hiyo nataka niseme ingewekwa vizuri kusudi kama hivi.

Lingine ambalo ningetaka kuzungumza kama oni langu la mwisho, kusema ule ukweli Kenya hii tulio sasa kila kitu kimeshaporwa. Sijui kama hivi leo tutahalalisha kwa sababu naona, ningetaka kusema hivi, katiba ijayo kuwe na sheria yakwamba baada tukishapiga kura zijazo, sheria iwe katiba, kuna sheria inasema ya kwamba, kila mali ya mtu kutakuwako na kuchunguzwa, kwa sababu kusema ule ukweli ziko mali zimepotea sasa na hata kama tumesema ufiadi haya lakini hizi balaa hatutarudishiwa. Basi still, tutakuwa hakuna chochoye kimepatikana manake kwamba Beach zote zishaenda na kila kitu kishaenda sasa. Kwa hivyo katiba ijayo iwe na sheria inasema hivi ya kwamba, kila mali itachunguzwa. Nimesikia mambo ya rudisho kabisa karibu kabisa county council hata mimi naunga mkono katiba ifikirie ni wapi lakini kisiwe ni kipengeleo kinacho soma hivi,kutakuwako baada ya kura zijazo kuwe...kuwe na sheria kuchunguzwa haki zote, hata kama Moi akipatikana kuna

haki nyingine sio yake irudishwe upesi mara moja, hii ni safi kabisa. Lakini sio kwamba hivi sasa tuwe twalalisha twende basi twendako hakuna mahali maanake kama ni kwetu sisi chumvi yote ni ya wahindi. Lakini sasa itakuwako kutakuwako na kipengele cha kudai haki tutakuja kusema kufikia sasa sisi watu wa Gongoni kwa ninin ardhi hii yote hatuwezi kupewa na sisi majhali pa kufanya chumvi hii kama ni haki tutapata kipande lakini ikiwa ni kwamba hakutakuwako hivyo basi hata tuingie maserikali hiyo lakini tutakuwa still yote yameshanyanganywa na hakuna wakati. Mimi ninataka kuwe na kipengele ambayo kinasema haki zitachunguzwa na haki ikionekana si haki itarudishwa mara moja kwa mwananchi.

La mwisho ni hivi, mwananchi kusema ule ukweli ni jambo la kusikitisha sana kwa sababu yeye huchagua mbunge akirudi anakuwa hana maana. Yeye...eeh...kila kitu mwananchi hata hivyo tumeitishwa hapa hivyo kama wananchi tunaunda hizi sheria, baadaye, sheria hizi hazitatumika ama pengine zitumike. Lakini wale watakao kuwa kule mbele watatumia zile zile kutupiga sisi. Hivi inaonekana imekuwa wananchi ni kama mahali pa kukimbilia . Mimi ningetaka kusema hivi, ikiwa wananchi sisi ndio serikali ningetaka kuwe na nafasi moja hii. Dakika hii kama nina shida na ni ya kweli nikikimbia kwa Chifu nikienda nataka nikwambie hakuna go-ahead nitaambiwa ni siasa urudi huko. Lakini hata serikali ijayo yaani itoe nafasi ya kwamba ninaweza kukimbilia ofisi yoyote nikalalamike na kutakuweko na...na kuweko kuna na kuna...kuna uwezo kuwa na hali ya lile tatizo ambalo nimenda kuli-report kwamba lichukuliwe mahali kwingine. Hivyo ni kwamba nionekane nimelalamika ukweli ama si kulalamika ukweli. Kwa sababu utakuta sasa wananchi wanalamika lakini kila unapoenda hakuna mlango, rudi huko unasumbua sana. Lakini sasa katiba ijayo kuwe na sheria, mwananchi wakati wowote kama anatatizo lolote anaweza kukimbilia ofisi kwa chief na akalichukua kama tatizo na akalipeleka mbele mpaka ukweli utakapo hakikisha ni ukweli au si ukweli halafu hapo ndio ni sawa lakini nataka niseme hivi ya kwamba mara nyingi tumekimbia kwa ...kwa wanaohusika lakini tumeonekana kama waendawazimu na hii ni kweli kabisa kwa hivyo sheria ijayo ikuwe tutakuweko na mahali ambapo nikiwakimbilia, nikipiga ripoti hatua itachukuliwa nakuhakikisha ni uwongo au ni ikweli. Nataka democracy ambayo naweza kusimama hata sokoni nikasema serikali hii ni mbaya kwa sababu ya hii na hii na hii tena askari asiniingilie manake nazungumza ukweli na hii nio democracy. Nikiwa nazungumzia ukweli, mimi nina ubaya gani? Kwa hivyo nataka niseme hii democracy ifike mahali ambapo itaruhusu mtu kuzungumza popote pale ikiwa serikali ina fanya makosa na iwe sheria itakayo haiwezi kumhukulia kwa manaake ni mkweli. Kitu kma hiyo pia ningomba. Basi kufikia hapo nataka kusema ya kwamba mimi langu ni kwamba serikali ijayo ingekuwa vizuri ingekuwa ya majimbo kwa sababu watu wa Pwani tume elimika kila mkoa tumeelimika.

Kusema kweli tena uraisi uzungushe ulivyo semekana. Uraisu usiwe ukabaki mahali pamoja, na raisi ukipatikana mahali pa kwanza mara moja, na pili. Sehemu ya tatu hatapatikana pale, tena kuwe na sheria ya kwamba tena kusiende ule urahisi. Kwa sababu hiyo litakuwa ni hiyo. Jambo la mwisho ni kwamba kwa nini serikali inazidi kuonekana ya kwamba inakubali ufiada? Rais mwenye akianza kupigania kura yukotayari kupoteza mabilioni kununua maleso hapa yeye na wanawake. Hii ni kuonyesha uongozi mzuri kwa wananchi ama ni kutaka kununua haki zao kwa njia gani? Hii nimeona hata kwa wabunge tunaowapigania mara nyingi ningetaka,...eh....eh.....katiba ijayo kiongozi yeyote aiganie kwa kutumia msemu na vitendo vyake anavyofanya. Lakini akitumia pesa ningekuwa nataka niseme hivi, ingekuwa sheria mtu yeyote anayetaka kupigania kiti akipatikana anatumia pesa achishwe kupigania ama hata ikiwezekana ashtakiwe ili afanyiwe kesi. Hiyo pia ninaomba sasa.

Lingine ni kuhusu habari za elimu. Nimesikia ya kwamba wengine wanasema ya kwamba...eh...wale wanaofaa kuchaguliwa ni wale tu ambao wamesoma hasa kufika kidato che nne. Mimi ninataka kutoa maoni haya, waliopigania uhuru walikua hawana elimu, wakapigania uhuru mpakawakailita hiyo uhuru. Nataka niseme hata haya mabadiliko, utakuta hata huku kwetu wanaopigania ni wale abao hawana elimu. Wale wnye elimu wamebaki kukaa kuangalia. Nataka niseme uongzi mzuri hauko juu ya elimu ama juu ya kusoma sana. Tumechagua wa university, still hawakufanyachochote. Mimi nataka niseme mtu achaguliwe kulinganana vile anavyoonekanakama kingozi. Kwa sababu kuna wengine kama wengine ukwakuta hawana elimu ya kutosha, lakini wana...wanafa, maanake ni wakili, maanake uongozi lazima uwe mkali. Baba, mji wako ukitaka uwe na heshima, lazima uwe na ukali, kwa hivyo ningetaka

(tape 6)

Com. Riungu: Asante sana John. Nzingo Ngamba, Josephat Mutiki, Emma Mundu, Nzai Henry Kombe, karibu.

Henry Kombe: Macommissioners, wote ambao muko hapa. Ninaitwa Henry Nzai Kombe, mwenyeji wa sehemu hii ambaye ninafuraha kwamba na mimi pia nitatoa maoni yangu sababu leo ni siku ya kuzungumza mambo ambayo yatawafaa watu baada ya siku za usoni zinazokuja. Mimi ninaatanza na uraia. Uraia mara nyingi huwa unatuletea shida, mtu anapozaliwa huwa amezaliwa ni mkenya halisi, lakini mara nyingi huwa kuna shida ya uandikishaji hata wakati mwengine unakuta kuna wenzetu ambao huwa wanasumbuliwa sana kuhusu mipango ya kitambulisho ikiwa wao pia ni wenyeji wa Kenya wataulizwa maswali mengi. Lakini haswa kuna kuna kipengee cha katiba ambacho kinawazuilia watu fulani kwamba hawafai kupata kutambulisho, basi iangaliwe kuanzia mpakani. Ikiwa mtu ashaingia hapa bila idhini ya serikali na ni mgeni, basi huyo achunguzwe mara moja na atolewe, lakini akimaliza muda wa miaka zaidi ya kumi, anastahili na yeye awe raia sawasawa. Ninaona kuna shida nyingi sana inayotekea wakati huu kwamba kuna baathi ya vijana wengi sana huwa hawapati vitambulisho vya uraia.

Na mara nyingi, hata kuna shida ingine ambayo hutokea. Kuna hawa watu wa nje ambayo wakioa mabibi, kama ni wazungu, wajerumani hivi, wataliani, akioa bibi akizaa watoto na bibi amemuo ni mkenya, watoto wale anaeza enda nao. Na hiyo haichunguzwi kwamba ni kwa sababu gani nayo ni wamezaliwa Kenya na hawabaki Kenya kwa sababu tunaonekana ni wadhaifu. Basi kwa sababu ya udhaifu, ichukuliwe haki kwa kila upande, ikiwa ni mtoto amezaliwa Kenya, na kuna mali fulani ambazo anaweza kupatiwa kutoka nje basi aleetwe hapa hapa Kenya kusudi mali zile ziwe zinaweza kunufaisha wakenya.

Haki za kimsingi. Haki za kimsingi kwa kusema ukweli kuna watu huwa wanazungumza kwamba ukabila hakuna. Lakini kwa kweli sisi kwa sisi mara nyingi huwa kuna wengine wanabagua wengine na wengine wanachukua wengine kuwaweka katika laini nzuri. Ukabila huwa unaingia katika mtu anayemchukua mtu ni huyu hana hisia za kufanana na mtu fulani ni ukabila tayari unaingia. Hapa sasa hapa sisi tukizungumza, tunasema tunataka majimbo. Tukisema tunataka majimbo halafu tunaingiza neno kwamba watu fulani wawe wataenda kwao, lakini nikisema hivyo tunaunga mkono ukabila lakini tunavyotaka sisi ikiwa ni serikali ya majimbo kwa sababu kila mmoja hata mimi ninaunga mkono kwamba serikali iwe ya majimbo. Lakini ikiwa ni

serikali ya majimbo kitu ambacho kiko, tuungane mkono ikiwa ni kila kabila ambaye amefika hapa mradi apate vile vipengee vinavyomfanya mtu anaweza kuishi na wenzake kisawa sawa.

Arthi. Arthi wakati mwingi tunakepengee ambacho huwa ambacho kinatumiwa sana kwamba serikali imetoa amri ya kwamba kila mmoja alindwe na mali yake. Basi kwa kusema ukweli sheria hiyo imewaumiza wengine sababu una title deed ambazo zilipatikana muda mrefu sana zaidi na wakiwa wenyewe ni wale ambao hawako, si waishiji wakenya haswa. Na kwa sababu sheria inasema kila moja alindwe na mali yake, wakati anapokuja na karatasi inayeitwa title deed, hata kama ni ya zamani gani, huyo mtu anasemekana alindwe mara moja na mali yake. Halafu wale ambao wako katika sehemu ile kwa muda mrefu zama zile mwenyewe alikubali kwamba watu wale waishi katika sehemu hiyo akiwa ametuma ma agent wake kwa muda mrefu zaidi ya miaka hamsini iliyopita. Sasa hivi wale waliokuwa wakichukua pesa walizokuwa wakiziita ijara wakati ule, wameenda hata wao nao wengine wamekufa, halafu wale waliokuwa wakichukuliwa ijara wakati huo, wamekuwa ni wenyeji wamepanda miti yamekuwa mikubwa kama hii mti, na sasa hivi wakaitwa ni masquatter. Tunaomba, Katiba iangalie katika title deed zile ambazo zina zaidi ya miaka hamsini, sitini ambazo zinaonekana mtu yuko na title deed na kwenye ground hana chochote abacho kiko, basi mtu huyo anastahili title deed ile iwe itakuwa nullified. Kwa sababu huyo sio mwenyeji wa sehemu hiyo, anadaiwa ni mwenyeji kwa sababu ana kitambulisho cha miaka sabini iliyopita. Halafu yeye mwenyewe hayuko katika sehemu hiyo. Hilo ni jambo limewakumba wakenya wa coast kwanzia mpaka wa Tanzani mpaka mpaka wa Somalia. Jambo hili limewakumba wakenya wengi sana na kuna jambo lingine hufanyika, watu huwa wanapatiwa ma title deed kule bila ya kuangalia chini. Mtu anapatiwa title deed ukifika huku hiyo sehemu ambayo amepewa title deed kuna majumba na kila kitu, halafu kwa sababu wale ambao wamempeana huku, hawakuja wakaangalia huku chini. Tunataka title deed kwa wakati huu zitolewe kuanzia kiwango cha location, kutoka kwa locatin ulizwe kwamba katika watu wanaoketi kwa sehemu hii, ni wakina nani na wanaostahili kupata title deed ni akina nani. Maanake ikiwa itategemewa vile kwamba mtu aondoke hapa akienda kufika kwa ardhi house, kila chochote atachofanya kirudi hapa aje awaambie watu wewe uko hapa unakaratasi, la mimi nimepata. Na kusema kweli tumeona mambo hayo yakitatiza sisi wanainchi wa kawaida kwa sababu wengi wanaoshi sehemu hii wanapo onyeshwa karatasi hiyo tayari wameshtuka na kwa kweli uwezo huo huna ofisi unaweza kuenda na ukafaulu kwa sababu kwanzia chief, DO, mpaka DC, PC, wakiona hicho kibali, wewe huna haki, unastahili uondoke kwa sababu amepata kibali. Na vibali vingi huwa si vya haki kwa sababu wengi wanaokuja wanafanya hivi hapa wapewe title deed halafu wanachora michoro yao anaenda kule anapewa kwa sababu hiyo sehemu wenyeji huko bado walikuwa hawajaomba. Kwa hivyo tungeomba, ardhi kwanzia kipindi kinachokuja cha Katiba mpya tunayotazamia, marekebisho yakifanywa, kipengee kile kirekebishe kwamba waanze kuulizwa kwanzia wazee wa vijiji mpaka machief waeleze kwamba wanaokaa sehemu hii ni wakina nani na wao wanaofaa urithi wa ardhi hiyo.

Kuhusu urithi wa akina mama. Wakina mama wakisema wapate urithi wa baba ambaye alikuwa bwana yake ni sawa kabisa, lakini ninataka kuuliza jambo ambalo ninataka lirekebishwe kuna mambo ya talaka. Hii mambo ya talaka imeumiza sana wakina mama wenyewe bado hawajui, na hiyo ndio imechangia sana watu wengi wanasema chokora wameletwa na serikali, hashu. Chokora wameletwa na wakina mama wenyewe kwa kukata kuishi vizuri na bwanake. Kwa hivyo, kuchangia machokora

imeletwa na hii matalaka mengi, kwa hivyo akina mama wazingatie sana haki zao wakikataa mambo ya matalaka. Hatusemi hiyo infanyika kwa dini gani ama gani maanake ni dini zote, mwanamke anaolewa halafu anaacha bwanake, anabaki hivyo, haswa wakati mwingi ni wale anamuona bwana hana uwezo, bibi yuko na uwezo, mara moja talaka inaingia pale. Kwa hivyo tungependa tukitaka wakati unaokuja mambo yawe mazuri hizi talaka za kikawaida ziwe zimekwisha, watu wote waelewane na tukifunga ndoa ihimarike vizuri na kulea watoto wetu, serikali yetu itakuwa mzuri sana inayokuja.

Utamaduni. Kwa kusema ukweli, wakati wa nyuma kule tuliopita kulikuwa na utamaduni wa kisawa sawa. Watu walikuwa wanaheshima na kuheshimiana vizuri, lakini siku hizi, tumebadilisha mienendo, na ikiwa kwa kweli tunataka Katiba mpya ama irekebishwe, tuangalie hata hali ya utamaduni wetu. Waliokuwa wakiishi na heshima zao na mienendo mzuri toka zamani, waangalie tulikuwa tukiishi namna gani na warudie maisha sababu siku hizi tumegeuza, tumeigiza mienendo ya wazalendo wa nje, sisi uzalendo wetu tumewacha. Kwa hivyo tukitaka uzalendo wetu tuufatilize turudie utamaduni wetu, tukirudia utamaduni wetu mambo yetu yatarudi sawa sawa. Hapo tutuakuwa tumezingatia umuhimu na Katiba itakuwa mzuri. Sitakuwa na mengi kwa sababu mengi yalizungumzwa na yalikuwa yakupendeza. Mimi nitabakia hapo. (clapping)

Com. Riungu: Asante sana. Daniel K. Kirimo, Samuel Kenga, Katana Kenga, Shee Ali.

Shee Ali: Ninashukuru kunipa nafasi hii. Langu mimi kama kweli Katiba hii ya kitafanya ukweli wa haki wa kibinadamu, na kuanza tunataka katika wananchi wote wawe na makao yao maalum kila mtu alikuwa na mahali pake, bila ya kuondolewa. Kwa vile, hii Katiba tuliyo nayo sasa si Katiba ya kisawa tumepata uhuru sitini na tatu mpaka sasa hatujaona raia yeyote mwenye furaha wala kuwa ana makao yake maalum. Langu mimi ninasema kwa imani kama Katiba hii itafanya imani na itakuwa ya ukweli, ya mwafrika, mwananchi awe na makao yake pale alipo bila ya kuondolewa na mwananchi yeyote ili aishi paleo makao yake na mashamba yawe yote amliki mwenyewe mwananchi. Hapo mimi nitaamini kama Katiba hiyo itafanya kazi. Mambo yangu mimi na maoni ni matatu.

Na la pili ni mambo ya shule. Twataka wazazi wenyewe wapunguziwe uzito ulioko sasa. Toka sitini na tatu mzazi hana nafasi kwa sababu anabidii ya kumsomesha mtoto wake shule lakini hana nafasi kwa umasikini. Kwa sababu akipilekwa shule mtoto anaambiwa arudi hana fee na hana njia ya kufanya mzazi isipokuwa sasa amwambie mtoto basi wewe kaa na akikaa ndio yule atamwambia ni chokora, chokora ni nini, ndio huyu. Atakwenda popote aone mahali au aone kwenye gari, aone mtu amevaa nguo mzuri na achukue kinyasi anataka kumtia nacho amwagie ili apate ile pesa ya chakula. Hii ni shida inatoka kwa sababu serikali yenyewe bado haijakuwa, ni ile ile ya ukolono ilioko mpaka sasa. Twataka hii koloni hii iondoke, mzazi awe na nafasi ajue mtoto wake anaendelea vizuri, kwanza ninataka iwe ni ya bure kutoa Katiba hii, ili mzazi apate nafasi naye ampee pumzi maanake mzito sana aliyo nayo.

La tatu, ni hospitali. Unaweza kuchukua mgonjwa wako hapa unaenda na yeye hospitali na pale alipo hospitali ni mwafrika mwenzako anayefanya kazi pale na ukienda pale mgonjwa ni mahututi na akifaka pale wataka kumweka pale apate matibabu

kama hana pesa anaambiwa ondoka maanake huna pesa. Na yule yule alikwambia ni mwafrika mwenzako, si muhindi wala si mzungu. Hii Katiba ichunguze sana jambo kama hilo, iwe raia akienda pale hospitali, asipate dhiki yeyote na asipate taabu yeyote, aendele vizuri ili akija nyumbani ajue mgonjwa wake yuko kisawa. Sina zaidi katika hayo matatu lakini Katiba hiyo kama ni ya ukweli na ya haki, jambo haya matatu niliyosema, iondoshwe uzito wa mzazi kwa makao, kwa hospitali na kwa shule. Asante.

Com. Riungu: Asante sana. Karisa Kisao, Safari Cheo, Kazungu Jonathan, Musa Salim, Zibron Baya, Franklyn Faraj, James Safari, Francis Tsuma, Onesmus Karisa, Daniel Karisa, Felix Chalo, Kazungu Francis, Jonathan Kenga, Kingi Chalo, Salim Omar, karibu mzee.

Salim Omar: Asanteni sana Commissioners. Mengi yashazungumzwa, na mini nishahudhuria vikao kama hizi vingi sana. Kitu muhimu ni Katiba ikiwa ni ile ya zamani au ni mpya itakayo undwa ifanyishwe kazi kama vile ilivyo. Jambo lingine mwenzangu ashazungumza kuhusu vitambulisho. Jambo lingine niliokuwa nalo ni kuhusu dini kwa vile serikali yetu imetupatia uhuru wa kuabudu sisi wananchi tusiingiliane kidini. Kila moja afuate ile dini anayetaka sawa sawa, bila matusi bila kuingiliana kwa jambo lolote. Kwa hayo tu asanteni sana.

Com. Riungu: Asante sana mzee. Kandau Kalama, Joseph Kazungu, Katana Mbaluk, Achola Otieno, Emmanuel Mwateta, Douglas Odudi, Maitha Lennox, karibu.

Maitha Lennox: Jina langu ni Maitha Lennox, ni mkaazi wa hapa Gongoni. Niko na maoni yafuatayo. Kwanza, kuhusu mambo ya elimu. Wananchi huwa wanatoa kodi kwa kila kitu wanachonunua huwa anatoa kodi hata ukinunua peremende, kuna ndururu inaenda kwa serikali, ukienda dukani kununua nguo, kuna pesa fulani inaenda kwa serikali. Maoni yangu ni kwamba, kwa sababu tunalipa kodi nyingi sana kwa serikali, elimu iwe ya bure tena ya lazima. Watoto wote ni lazima wapelekwe skuli na wasome, wale wazee ambao hawataki kupeleka watoto skuli, waweze kulazimishwa na sheria ili watoto waweze kusoma. (clapping)

Jambo la pili, kuhusiana na mambo ya employment. Vijana wetu wengi hawa kazi, utakuta kwamba wanaranda randa hovyoo halafu mwishowe inabidii wakakae mahali kujiburudisha labda na mnazi ama bangi, anafanya uhalifu kwa sababu hana kazi. Maoni yangu ni kwamba serikali ikaweze kuundisha mpango maalum kuhusiana na vijana wetu ambao hawana kazi, kwa mfano, mahali kama Uganda serikali imechukua pesa fulani katika zile zile zinazotolewa na wananchi katika kodi ikawaanzishie mradi fulani halafu wakawa wale vijana wanafanya kazi katika mradi ule ule wakipatia mapato yao. Wameanzishiwa kule, wamenunuliwa boda boda kila mmoja amepewa piki piki anaweka kwa stage, mtu akifika anatoa shilingi ishirini anampeleka kwa mahali fulani. Ule ulikuwa mradi fulani wa serikali, hawa wetu pia wa hapa Kenya tungetaka waanzishiwe mradi kama hii na serikali kwa sababu wanatoa pesa fulani katika mipango ya kodi. (clapping)

Katika mambo ya uhuru ya kuabudu, dini. Sheria hivi sasa inasema ya kwamba uko uhuru wa kuabudu, lakini nini? Hili ndilo swali, uhuru wa kuabudi nini? Maoni yangu yanasema hivi, ieleze wazi wazi kabisa kwamba uko uhuru wa kuabudu Mungu, sio kuabudu shetani au kuenda kuabudu mambo mengini halafu ati ni uhuru tu wa kuabudu. Nikiongea mambo ya land. Hii imekuwa ni mwiba wa watu wa hapa pwani. Umesikia wanaongea kwa uchungu hata mimi nikianza kuongea mambo ya land inakuwa ni kama sumu, nimesikia vibaya mwili inatetemeka kidogo. Unakuta kwamba miaka thelathini wewe umeishi pale katika eneo fulani, umelelewa pale na babako mpaka umekuwa mtu mzima mzee, ati mtu anakuja sasa na karatasi yake anasema hapa ni kwangu sijui hii nimenunua niko na title deed. Tunataka kila mmoja yule ameishi mahali fulani kwa miaka zaidi ya sita, apewe mwenyewe hakuna mambo ya kwamba ati kuna mtu ana title deed. Kwanza, wakati wa uhuru mwaka wa 1963 wakati tulipigana vita na wale wakoloni, baada ya wakoloni wale wakikuyu kule bara, waliteta wakasema lazima tupewe mashamba yetu na serikali ikatoa pesa, ikanunua mashamba yote yale ya settlers, wakagawanyiwa wakikuyu wote kila mtu akapewe cheti chake. Kwa nini sisi wakati tulipopata uhuru hapa sultan alikuwa yuko hapa hapa, yeye alikuwa amepatiwa 10 miles coastal strip hii yote, serikali ilikuwa ina haki ya kumlipa pesa zake sultan na hii land yote watu wetu wa pwani wagawanyiwe wenyewe. Kwa nini serikali haijamlipa sultani mpaka leo, ati sasa kunakuja mtu mwarabu na title deed ni tangu ya 1830, unakuja kuonyeshwa hapa ni kwangu, ni kwa mjomba wangu, mjomba wake ndio alikuwa yeye ndi alikuwa mwenye hapa, hizi ni hadithi ambazo hatutaki kuzisikia. Na hata hivi sasa hapa pwani tunasema mtu akija na karatasi kama ile akuambie kwamba ati hii land ni yangu, unaingia ndani unachukua mshale na unamfuma, hakuna maneno tunaka kuongea hapa mambo ya land. Serikali ni lazima itoe pesa inunue hii mashamba zetu zote ambazo zilikuwa za waarabu na tugawanyiwe wenyewe na hatuondoki tena hapa, hatutaki na hatutaondoka.

Ufisadi. Watu wengi wamekuwa wakiongea hapa kwa uchugu unasikia bwana DO anasema askari wako, yote hii sio kulalamikia mambo ya askari au ukaenda kulalamikia chief. Unasema ukienda kwa chief, bwana DO, unataka permit tu ya kuenda kuzika mtu wako, chief wako anasema ni mpaka utoe mia ndio nikuandikie permit, angalia wewe. Ni huzuni uliyo nayo vipi wewe, umefiwa tena unaambiwa ile permit tu angalau ya kwenda kuandikiwa ya kuenda kumzika mtu wako ni mpaka shilingi mia mbili kwanza, hebu fikiria wewe. Lakini sio ati shida, shida yenyewe sio hapo, shida yenyewe ni kwamba serikali inafanya vibaya wafanyi kazi wa serikali hawalipwi mishahara ya kutosha. (clapping) Kama serikali ingeliwapatia pesa za kutosha maDO, wangeliwapatia pesa za kutosha waalimu, wangelipatia pesa za kutosha askari, hawangetafuta kitu kidogo. Kwa hivyo kuundwe kama ni shirika ni tume fulani inagalia mishahara ya wafanyi kazi wote wa serikali katika gazeti ya leo ati minister anaongeza wafanyi kazi shilingi mia mbili na thelathini. Itamsaidia nini askari, ama itaenda kumsaidia nini mtu mfanyaji kazi yeye yuko na familia na kila kitu. Hapa kuna mbunge analipwa shilingi nusu milioni, yuko na watoto wawili na wewe uko na watoto sita. Kwa hivyo mambo ya ufisadi ni mbaya sana, yote imeletwa na kwa sababu mishahara midogo ya wafanyi kazi. Mfanye kitu, waongezewe kitu pesa kidogo ili tuweze kupata mambo ya mshahara.

Rasilimali zetu. Sisi hapa tuko na bahati, tuko na bahari hapa, tuko na minazi hapa, tuko na mikoroshu, tuko na chumvi, tuko na mchanga, lakini hebu fikiria imetusaidia namna gani mambo haya yote. Sheria ya sasa haiongei ni jinsi gani watu hawa watasaidiwa na vitu vyao. Ikiwa ni chumvi inatoka hapa, tunataka percentange fulani iwasaidie watu wa hawa, ikiwa ni mambo

ni mnazi, mnazi ile inatoka pale, mbona kule bara, kahawa serikali inawaundia, a certain board inachukua bidhaa zao zote wanaenda kuuziwa ulaya halafu wanakuja kugawanyiwa pesa zao, sisi kwa nini hawawezi kuchukua vitu vyetu na kwenda kuuza mbali kule. Tunataka serikali iwezi kufikiria swala hii kwamba kila mmoja akaweze kulinda rasilimali zake na pia a certain percentage ikaweze kuwafaidisha watu hawa ambao wanatoka katika eneo lile.

Kuhusiana na mambo ya utawala, tunataka kuondoa, hatutaki mambo ya sub-chief tena. Mambo ya chief, ondoa kabisa hiyo, ile tunataka ni mtu atakayesimamia sehemu hii yote ya hapa kama ni location, tuwe tutachagua wenyewe, tunamtaka mzee fulani asimamie hii sehemu ya hapa, tumpigie kura na ikiwa hafanyi vile tunataka. Sio ati sheria ingoje mpaka miaka tano au serikali iseme nini ndio atolewe, hapana, ikiwa hawezi the maximum vile wananchi wanataka mara moja atolewe, sio kungoja ati miaka mitano kama vile ya wabunge, hafai, na unagonjea mpaka miaka mitano na unaendelea kuvaa wewe pesa zako unalipa kodi kila siku, anapata mshahara na hupati chochote. Sisi ndio tunawalipa hawa wafanyaji kazi wa serikali ni lazima watupatie huduma kama hawatupatii huduma ondoa, weka mwingine, hii ndio tunataka hatutaki mambo ya kungojea ngojea mpaka saa fulani. (clapping)

Kuhusiana na mambo ya mahakama. Mahakama ni mbaya sana. Hapa iko nyani na hapa iko monkey. Ile ningetaka kuongea ni kwamba wewe huwezi kwenda kumhukumu mtu ambaye amekuandika kazi. Mimi nimeandikwa kazw na bwana Madei halafu bwana Madei nimpate yuko na makosa, yeye ndio aliniandika kazi jana, mimi nitaenda kumuingiza jela huyu bwana Madei? Hiyo haiwezekani. Ni lazima nitawafanyia favour fulani kwa sababu bwana madei ndio aliniandika kazi. Hii ndio jinsi ilivyo hivi sasa, majaji wote wamekuwa appointed by the president, unakuta kwamba hawawezi kufuata ile sheria sawa sawa kabisa, ametiwa ndani kwa sababu ya murder huyu bwana, sasa judge hawezi kutoa ruling mpaka itoke kwa Attorney General atoe consent kwamba sasa huyo ni aenda kwa kinyongo. Na ukumbuke AG naye ni lazima awe amemuuliza mzee, 'mzee sasa huyu kijana tufanya namna gani', aambiwe na mzee, 'sasa huyu ni kijana wangu si wachana na yeye'. Unaona, sasa unakuta sheria haiwezi kuongozwa tena, inabidi ni mtu ndio anafwatithiwa. Kile tunataka ni kwamba kuundwe a separate body ambaye itakuwa iko kando kabisa, sio ya serikali kazi yake inaangilia, je inafanya kazi yake, ikwa ni wafanyi kazi wa serikali, je wanafanya kazi yao, ikiwa ni polisi, wanafanya kazi yao, ikiwa ni mambo ya mahakama, je wanafanyaa kazi yao ya mahakama? Sio wale wale, utakuta tumekuwa na Commission ngapi? Unasikia wakina Harun Mwau kwa mfano, wamechaguliwa, wakaanza kuangalia mambo ya ufisadi mara kidogo alipoingia kwa wale ambao waliomchagua kufanya kazi, akaambiwa wewe huna haja na kibarua, nenda. Pesa zetu zinaendelea kupotea tu ukumbuke, wewe ndio unalipa pesa, unalipa kodi, kodi ile ndio inawalipa pesa hizi zote. Kwa hvyo vile tunataka kusema hapa ni kwamba mambo ya mahakama, kuwe na separate body itakayo isimamia mambo hayo.

Kuhusiana na mambo ya ugawanyaji wa vitu, iwe sawa. Sio kwamba ati hizi university ni nyingi huko, huku pwani hakuna kitu. Angalia kwa mfano mambo ya utalii, tumekosa hata uwanja wa ndege hapa, kule zimejaa uwanja zandegede.

Milioni hii ishirini na zimetoka hapa kwenye chumvi ambao sisi ndio tunavunja chumvi, sisi ndio tunafanya kila kitu kwa hii

chumbi yetu. County Council ikumbuke angalao watu wa Gongoni ndio wanatuletea pesa hizi zote milioni ishirini wacha tuwaeke mfereji wa maji angalau mpaka Ngongoni. Wamefanya nini county Council, hii pesa tunalipa kila siku kodi tu, watut tu wakila matumbo, hatuna haja hatutaki tena. Kwa hii Katiba ingine hatuna haja na County Council, itoke iende kabisa, hatuna haja nayo tena. Na kama ni diwani tutamchagua hapa, na tuwe na wale viongozi wetu, tumesema hatuna haja na machief, kuwe na mzee ambaye tumemchagua mwenyewe awe hapa, anajibu yeye kila kitu mambo yote. Tunateseka watu hapa na kila siku tunalipa pesa, hii ni mbaya sana. Hatuna haja.

Mwisho, haya yote ninajaribu kuzungumza hapa yhameletwa kwa sababu ya central government. Kila kitu ni huko, kama ni nini mpaka Nairobi, mzee moja alikuwa anasema hapa, itabidi siku ingine kama unataka kuchimba choo, mpaka uapply Nairobi pia.

(clapping) Kila moja apewe uwezo katika district yake, pale pale, ikiwa ni mambo ya mashamba Commissioner wetu awe hapa Malindi, awe anajua pale mahali inasemekana huko kuna mayonda, ni ukweli, huyu mzee Katana Kacharo ameishi hapa miaka thelathini, basi ninaambiwa hapa kuna mayonda, is it true? Anajua kwa sababu yeye yuko grassroot huku. Kwa hivyo tunataka majimbo, hatutaki mambo ya hii serikali kama ambavyo imekua inafanya, tunataka yaje, ili tujitawale wenywe. Ikiwa ni chief wetu au mzee wa kijiji awe ni wetu mwenyewe tunamjua sisi pale, akianza kwenda kombo kombo tunamwambia, mzee ni sisi tunakupatia kazi, ni sisi ndio tunakulipa, tunaweza kukun'goa, hatutaki mchezo. Kwa hivyo ile Katiba inafuata, tunataka kila kitu kiwe katika mambo ya majimbo, utawala uwe ni sisi wenyewe, tukiharibu tunaharibu wenyewe, tukifaulu ni sisi wenyewe. Asante sana.

Com. Riungu: Asante. Nitamwita mzee moja nilikuwa nimemuambia angoje hapa, karibu.

Emmanuel Mwatata: Ninasema ni asante, kwa sababu mengi yameshakwisha zungumzwa, singependa nipitie kwa yale yamesha kwisha zungumzwa, lakini ninataka niongee juu ya Katiba kuhusu serkali natakayo iwe ina nguvu katika dini kwa sababu dini ndio inayoleta heshima katika wanandamu wanaoishi. Tukiangalia ya kwamba katika hali ya dini inatuongoza hata hali za mavazi, katika hali ya kibdinadam kumetokea mavazi mengi ambayo ni ya kiheshima, na mengine ambayo hayana heshima. Lakini kwa sababu hii hatuna maongozo wa dini, tunakaa na mavazi ambayo hayana heshima, watu wanasema 'see me through'. Mavazi ambayo unakaa na msichana wako ambaye labda munaheshimiana, lakini kwa sababu hakuna muongozo wa dini, hakuna nithamu, hakuna heshima, anakuvalia 'see me though' kama ni 'hail maria', anakuonyesha hata ile ya ndani na wewe unakaa na yeye hapa ati mumendelea kiutalii. Huu ni uchafu katika nidhamu ya kiuafrika. Kwa hivyo hii tunasema kila kitu hata kama ni Katiba mpya iwekwe na heshima katika hali ya mavazi, na tena inarudia katika hali ya kuendelea ati kujistarehesha. Kuna machafu ambayo yanaendelea ambayo ni matusi kama kuangalia runinga, kuna picha zingine ambazo ni za matusi. Lakini badala ya kuwa mtu ameshiba anataka kwenda kulala, kuna kanda kwa runinga zinawekwa kwa kimatusi ambazo zinaruhusiwa na serikali. Mtu amevaa anaungalia hali za kimapenzi na watoto wake, mara msisimua anaingia, mtoto wa skuli anaharibika iwapo, ni mume na msichana kwa sababu wa msisimuko wa kuangalia hayo maruninga yanayoendelea. Isitoshe, katika sherehe tofauti tofauti tuseme kunakuwa ni kama show, sehemu fulani zimetengwa zimeruhusiwa za mchezo watu kucheza tupu tupu, eti kupatikane Miss Kenya. Hapo kuna watoto wa skui wanaingia, wavulana na wasichana wapo,

